Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

**Kikao cha Ishirini na Saba – Tarehe 18 Julai, 2008**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana Kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2008/2009.

**MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:**

Taarifa ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na maoni ya Upinzani kuhusu makadirio ya matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2008/2009.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 237

**Ukuta Uliojengwa Pembezoni Mwa Mto Pangani**

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH** aliuliza:-

Kwa kuwa Mji wa Pangani ni moja kati ya Miji Mikongwe hapa nchini ambao umejengwa kando kando ya Mto Pangani na kwa kuwa umejengewa ukuta pembezoni mwa Mto Pangani ili kuzuia Mji wa Pangani usifunikwe na maji ya Mto huo na Bahari na kwa kuwa ukuta huo umejengwa wakati wa ukoloni tangu enzi za Mjerumani na umejengwa kwa teknolojia ya zamani kwa mawe ya Tumbawe na hivi sasa inahatarisha maisha ya wakazi wa Mji wa Pangani kwa kuwa umechakaa:-

(a) Je, Serikali itatenga fedha za kutosha kuujenga upya ukuta huo?

(b) Pamoja na Kamati ya Miundombinu kutembelea eneo hilo na kuunga mkono hoja ya kutaka zitengwe fedha kwa ajili ya kuujenga ukuta huo. Je, nini mikakati ya Serikali kutekeleza jambo hilo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mbunge wa Pangani lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwa ukuta huo ni wa zamani na umechakaa, hali ambayo inaashiria kuhatarisha maisha ya wakazi wa Mji wa Pangani. Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Pangani imekuwa ikiufanyia ukuta huo matengenezo madogo madogo kwa kutumia bajeti ya Halmashauri, lakini matengenezo haya hayakidhi haja ya kuuweka ukuta huu katika hali ya usalama kutokana na uchakavu wake.

Mnamo mwezi Januari 2008 aliyekuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya (sasa Waziri wa Maji na Mifugo) alitembelea ukuta huo.

Kutokana na uchakavu aliagiza Halmashauri ya Pangani kufanya upembuzi yakinifu ili kubaini gharama zinazohitajika kuufanyia ukarabati mkubwa ukuta huo. Tayari Halmashauri imekwishakamilika upembuzi huo na kubaini kuwa kiasi cha shilingi 531,441,900 zinahitajika kufanya ukabarati huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeshapokea upembuzi huo kwa ajili ya kuona uwezekano wa kutenga wa kutenga fedha za ukarabati mkubwa katika bajeti ya mwaka 2009/2010. Ofisi yangu itashirikiana na Ofisi ya Makamu ya Rais mazingira kuangalia namna bora zaidi ya kunusuru ukuta huo. Kwa sasa Serikali inaihimiza Halmashauri ya Wilaya ya Pangani kuendelea kuufanyia matengenezo madogo katika maeneo hatari ya ukuta huo wakati ikisubiri fedha za ukarabati mkubwa kutoka Serikalini.

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile siku hili lilikuwa la siku nyingi zaidi ya mwaka na nilipoona kimya ndiyo nikamwarifu Mheshimiwa Profesa Mwandosya wakati ule Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Rais na akatekeleza maombi ambayo wananchi wa Pangani wameomba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali ni kwamba muda sasa unapita na kutokana mabadiliko ya hali ya hewa, bahati inajaa kila wakati kutokana na tunavyozungumzia global warming. Je, Waziri haoni kwamba bila kutoa taarifa ya muda specific ya kupanga bajeti ya kutekeleza ukuta huo ujengwe itakuwa ni tatizo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu naomba yawe mafupi najua umeshajibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli kwamba muda unakwenda na kwa sababu ya hizi global warming na nini na ndiyo katika jibu la msingi hapa tumesema kwamba tunaitaka Halmashauri ya Wilaya Pangani Ihakikishe kwamba inafanya marekebisho ya hapa na pale kidogo kidogo wakati tunaendelea kushirikiana na Wizara ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira ili kuona kwamba tunaondokana na jambo hili.

Si rahisi sasa mimi kusema hapa kwa sababu bajeti imeshapita hapa na sasa position ya Serikali kuhusu bajeti iko pale tayari. Ninachoweza kusema hapa ni kwamba tunaiona concern ya Mbunge na tunakupongeza kwa hilo tutaendelea kushirikiana na wewe ili tuone kwamba tatizo hili linaondolewa.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuongezea majibu ya swali hili, swali muhimu sana kuhusu Pangani pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Ukuta wa Pangani umeharibika sana na ulijengwa nyakati za Ujerumani. Niseme tu kwamba mwezi Desemba, mwaka 2007 Jumuisha ya Kimataifa ilianzisha mfuko wa kuhimili mabadiliko ya hali ya hewa wakati wa mkutano wake uliofanyika pale Bahli.

Sasa katika mfuko huo matarajio yetu ni kwamba huu mradi wa Pangani ni mmoja kati ya miradi ambayo inakidhi vigezo vyote vilivyokwe na mfuko huo na Serikali itaomba matumizi ya fedha za mfuko katika kusaidia pale ambapo patakuwa na

gape katika kutengeneza matengenezo makubwa ya ukuta huu wa Pangani. Nashukuru. (*Makofi*)

Na. 238

**Ahadi ya Gari na Nguo – Mufindi**

**MHE. BENITO W. MALANGALILA** aliuliza:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuwa Naibu Waziri wa TAMISEMI aliahidi kuwa Serikali itapeleka gari la kubeba wagonjwa pamoja na kutoa nguo za watoto wachanga kwenye kituo cha Afya cha Kasanga Wilaya Mufindi, ahadi aliyoitoa wakati wa kufungua jengo la wazazi kwenye kituo hicho:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MIKOA** aliuliza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Benito William Malangalila, Mbunge wa Mufindi Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli mnao tarehe 3/9/2003 Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuwa Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, aliahidi kuwa Serikali itapeleka gari la kubeba wagonjwa katika kituo cha Afya Kasanga katika Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi.

Vile vile Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati huo akiwa Naibu Waziri, wakati anafungua jengo la wazazi kwenye Kituo cha Afya cha Kasanga aliahidi kutoa nguo za watoto wachanga wa kwenye kituo cha afya cha Kasanga aliahidi kutoa nguo za watoto wachanga wa mwanzo ambao wazazi wao watakuwa wamejifungulia katika kituo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ufinyu wa bajeti, Serikali imekuwa ikinunua magari ya kubeba wagonjwa kwa awamu. Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi ni miongoni mwa Halmashauri 33 zilizopata magari ya kubeba wagonjwa (*ambulance*) katika mwaka wa fedha 2006/2007.

Gari hili kutumika kwenda kuchukua wagonjwa kutoka kwenye vituo vya afya ikiwa ni pamoja na Kituo cha Afya cha Kasanga ama majumbani na kuwapeleka Hospitali ya Wilaya na Mkoa. Serikali haijaweza kuwa na uwezo wa kifedha wa kutosha kununua magari ya wagonjwa katika kila kituo kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu watoto wa mwanzo kuzaliwa katika kituo cha afya cha Kasanga Serikali kupitia Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi

imekwishatekeleza ahadi iliyotolewa kwa kuwapatia vifaa mbalimbali kama vile nguo, sabuni, mafuta, sukari, taulo na doti tatu za vitenge kwa ajili ya akina mama au walezi. Kwa kumbukumbu tulizonazo watoto watatu wa kwanza kuzaliwa katika kituo cha afya Kasanga walizaliwa tarehe 7/9/2003 mama mzazi Malikia Ngoda toka Kijiji cha Ihomasa, tarehe 14/9/2003 mama mzazi Florida Fungo kutoka kijijji cha Kasanga – kwa sasa ni marehemu mtoto yupo hai na tarehe 18/9/2003 mama mzazi Honorata Msele toka kijiji cha Kilolo.

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini napenda muelewa kwamba Waziri Mkuu alifika pale alivyokuwa Naibu Waziri wa TAMISEMI na aliahidi. Lakini kwa sababu ya ufinyu wa bajeti kama alivyosema nataka nimuulize ni kweli kwamba Serikali bado inaahidi kwamba itatoa gari katika kile kituo cha Kasanga kama Waziri Mkuu alivyoahidi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tumekiri hapa kwamba ni kweli kabisa Mheshimiwa Waziri Mkuu alikwenda kwenye kituo na aliahidi hivyo.

Kilichofanyika hapa na kama jana mlisikiliza jibu ambalo alitoa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, ni kwamba kwa mwaka 2006/2007 zilinunuliwa *ambulance 30.* Mwaka 2007/2008 zikanunuliwa ambulance 33 mahitaji katika nchi hii ni *ambulance 300* tulichosema hapa ni kwamba gari hili tumeona kwamba ni muhimu tulipeleke katika makao makuu ya Wilaya ili liweze kusaidia vituo vya afya vingi vilivyoko katika lile eneo.

Tungeweza kabisa hapa tukaamue gari lile tulichukue moja kwa moja tukalipeleka katika Kituo cha Kisanga lakini hii ingekuwa ni problem kwa vile vituo vingine ambavyo navyo vinahitaji huduma kama hii. Ni kweli kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu aliahidi hivyo, gari, lilipelekwa lakini likapelekwa katika makao makuu ya Wilaya. Muda utakaporuhusu tutaona uwezekano wa kupeleka katika kituo hicho kama anavyosema lakini kwa sasa hivi tulifikiri tufanye hivyo. (*Makofi*)

Na. 239

**Idara ya utumishi wa walimu TSD**

**MHE. AHMED ALLY SALUM** aliuliza:-

Kwa kuwa idara ya Utumishi wa Walimu *(TSD)* ni muhimu sana kwani inawahudumia watumishi, walimu wengi sana kwenye Halmashauri ya Shinyanga Vijijini na kwa kuwa fedha zinazotolewa toka Serikali Kuu ni kidogo sana na hivyo utendaji kazi wa idara hiyo kuwa mgumu sana licha ya kwamba wamekuwa wakitegemea msaada kutoka kwenye Halmashauri ili waweze kukamilisha majukumu yao vizuri:-

(a)Je, kwa nini Serikali isiwaongezee fedha za kutosha ili waweze kufanya kazi zao vizuri na kupunguza mzigo kwenye Halmashauri ya Shinyanga Vijijini:-

(b)Je, ni lini Serikali itawapelekea vyombo vya usafiri kama vile gari, pikipiki na kadhalika ili waweze kukamilisha majukumu yao kwa wakati?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA** aliuliza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mbunge wa Solwa lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, idara ya Utumishi wa Walimu ni moja kati ya idara tano za Tume ya Utumishi wa Umma. Hivyo kiwango cha fedha zinazotengwa kwenye bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Tume ya Utumishi wa Umma kinatokana na majukumu ya tume hiyo na uwezo wa Tume hiyo na uwezo Serikali kiuchumi.

Aidha, mgawanyo wa fedha za tume kwenye idara zake ikiwamo idara ya utumishi wa walimu ni jukumu la tume kutegemea bajeti inayotolewa na Serikali kuendesha shughuli za Tume.

(b)Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa vyombo vya usafiri kama vile gari, pikipiki n.k. pia hutegemea uwezo wa Bajeti. Kwa kuwa Tume inafanya kazi na Halmashauri za Wilaya ni vyema Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini na Wilaya nyingine zikasaidiana nayo kwani ipo kwa ajili ya watumishi wa Serikali kuu na Serikali za Mitaa.

**MHE. AHMED ALLY SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kutotenga fedha za kutosha katika Idara hii haioni kuwa inasababisha uwezo mdogo katika idara hii walimu, wao pamoja na walimu kutokuwa na uwezo mzuri wa kutoa huduma ipasavyo?

Kwa kuwa Halmashauri zenye uwezo mdogo wa mapato ya fedha inakuwa ni mzigo mkubwa kwao kuhudumia idara hii. Je, Serikali haioni umuhimu sasa kutoa kipaumbele katika Idara hii kutenga fedha za kutosha ili isiwe mkubwa katika Halmashauri zote nchini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoelezea katika jibu langu la msingi kwamba idara ya utumishi wa walimu inatengewa fedha kutokana na uwezo wa Serikali pamoja na majukumu ya idara hiyo. Idara hiyo katika Wilaya ina watumishi 6 tu ambao watatu mmoja ni Katibu wa Tume, mmoja Afisa wa Maadili na mwingine ni Afisa wa Ajira.

Kwa asili ya kazi zao ni watu wa kukaa ofisini ni mara chache sana ambapo wanahitaji vyombo vya usafiri kutoka nje ya ofisi zao. Kwa hiyo, ninaiomba Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini pale linapotokea suala la kuhitajika watumishi watoke

nje ya ofisi basi wawasaidie. Lakini Serikali tunalipokea, uwezo wa Serikali ukiongezeka basi na idara tutaiongezea fedha za kufanyia kazi. Lakini kwa sasa fedha tunazozitoa tunaamini kabisa kwamba zinaweza kumudu majukumu ambayo idara imekabidhiwa.

Na. 240

**Uhitaji wa Soko la Mazao ya Kilimo Namtumbo**

**MHE. VITA R. KAWAWA** aliuliza:-

Kwa kuwa masoko ni eneo muhimu sana katika sera ya kilimo kwa kuinua kipato cha mkulima kwa kuchochea uzalishaji na hivyo kuboresha maisha ya wakulima.

Je, Serikali inaweza kutenga fedha maalum kwa ajili ya kujenga soko moja Wilayani Namtumbo kwa ajili ya mazao ya kilimo ili kuwa na uhakika wa soko na bei nzuri na halali kwa wakulima?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JEREMIAH S. SUMARI K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO)** aliuliza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Vita Kawawa kuwa soko Wilayani Namtumbo litakuwa kiunganisho muhimu sana katika kujenga kilimo endelevu kitakacho chochea uzalishaji zaidi, bei nzuri ya mazao, kipato cha chakula cha uhakika na hivyo kuchangia katika kukuza uchumi na kuleta maisha bora kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kuibua na kutekeleza miradi ya maendeleo unafanywa na wananchi kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya kwa kuingiza miradi hiyo katika mipango ya Wilaya.

Serikali nayo inalo jukumu la kushiriki pamoja na kuweka mazingira bora ya kuvutia uwekezaji na kutoa ushauri kuhusu mapendekezo ya miradi hii. Serikali itatimiza wajibu wake ili azma ya Mheshimiwa Mbunge Vita Kawawa na wananchi wa Namtumbo itimie. Kwa kuzingatia maelezo niliyotoa hapo juu, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge kwenye Halmashauri zetu kuwa mstari wa mbele kuhakikisha kwamba Halmashauri za Wilaya zinaibua miradi ya ujenzi wa masoko ya kisasa na kubuni njia mbalimbali za kujenga na kuendeleza masoko hayo kupitia bajeti zao za Halmashauri au vyanzo vingine vya fedha.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

(a)Kwa kuwa, mwaka 2006 Programu ya *MSDP* iliahidi kujenga soko katika Wilaya ya Namtumbo, na kwa bahati mbaya programu hiyo ilifikia ukomo kabla ya kutekeleza ahadi hiyo. Je, Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko ipo tayari kuweka Mpango Mkakati wa kusaidia kuweka soko au viwanda vidogo vidogo katika Wilaya yetu ya Namtumbo?

(b)Kwa kuwa, mwaka 2007/2008 Halmashauri ya Namtumbo ilipeleka ombi maalum Hazina la mradi wa ujenzi wa soko, lakini Hazina haikuitenga fedha na mkakati wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo ni kuendelea kupeleka maombi hayo Hazina ili kutengewa fedha. Je, Serikali ipo tayari kulisaidia hili ili tutimize azma yetu?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JEREMIAH S. SUMARI K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Vita Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa *MSDP* ulianza mwezi Januari, mwaka 2003 ni mpango wa miaka saba unakwisha mwezi Desemba mwaka ujao. Sasa mpango huu mpaka sasa umekwishawahusisha Wilaya 36, na kwa bahati Namtumbo haikuwa mmoja ya Wilaya hizo. Lakini kuna tathmini ambayo inaendelea kufanyika, na imeonyesha kwamba Mpango huu ambao unafadhiliwa na Serikali yenyewe na *IFAD* pamoja na *ADB* umekuwa ni wa mafanikio makubwa. Kwa hiyo, Serikali inaangalia uwezekano wa kuwa na awamu nyingine baada ya kumalizika kwa awamu hii ya sasa, na endapo hiyo itatokea basi matumaini yangu na maombi kwa Mheshimiwa ndugu yangu Mheshimiwa Vita Kawawa ni kwamba Namtumbo itawekwa kwenye Mpango huo utakaofuata. Lakini kwa hili la kupeleka maombi Hazina hilo linatuwia vigumu kidogo kutekeleza kwa sababu sisi tungetegemea kwamba maombi yale yangepelekwa kupitia TAMISEMI na kule TAMISEMI wangeona kwamba mpango huo ungekuwa wa kipaumbele, basi ungewekwa kwenye utaratibu wa kuupatia fedha za kuukamilisha. Kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba tafadhali wapeleke maombi hayo kupitia TAMISEMI na kutoka kule basi itatazamwa kama ni vizuri kuuweka kwenye utekelezaji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tumekuelewa. Swali la nyongeza Mheshimiwa Lekukle Laizer.

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, Mji wa Namanga una matatizo kama Mji wa Namtumbo; na kwa kuwa Mji wa Namanga uliopo mpakani una soko ndogo na mazao yanatoka katika Mikoa mbalimbali na kupitishwa hapo Namanga. Je, Serikali inaweza kujenga soko kubwa la Kimataifa ili mazao yasiende Kenya na Wakenya waje kununua mazao yale pale Namanga kuliko kuwapelekea huko Kenya?

**NAIBU SPIKA:** Swali lingine hilo. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu. Lakini naomba ujibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JEREMIAH S. SUMARI k.n.y WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba kama nilivyosema naomba Mheshimiwa Mbunge ashiriki kwenye kuweka ujenzi wa soko pale Namanga kwenye Mipango ya Halmashauri ya Wilaya ya Longido; na kwa kuwa, yeye ni Mjumbe kwenye Baraza la Madiwani, basi ninaamini ana uwezo wa kuweza kujenga hoja ya kupewa kipaumbele na ujenzi wa soko hilo ukatekelezwa.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Viwanda na Biashara mwaka 2004 walitoa ahadi hapa Bungeni kwamba watajenga soko la kimataifa Laela Sumbawanga kwa ajili ya kuunganisha biashara kati ya Tanzania na nchi ya Zambia. Je, ahadi hiyo itatekelezwa lini?

**NAIBU SPIKA:** Huyu wala si Waziri mwenyewe. Mheshimiwa Naibu Waziri jibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JEREMIAH S. SUMARI K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO):** Mheshimiwa Naibu Spika, hilo tutalifikisha kwa wahusika na kama ilikuwa ahadi ya Serikali kwa kawaida Serikali hairudi nyuma kwenye ahadi zake isipokuwa inaweka kwenye utaratibu wa utekelezaji na ninaamini siku ya siku hilo soko litajengwa.

Na. 241

**Malipo ya Wazee Waliostaafu**

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali inatambua umuhimu wa wazee na mchango wao katika ujenzi wa Taifa letu, kwa mujibu wa Ibara ya 105(b) ya Ilani ya Uchaguzi wa CCM ya 2005 na kwa kuwa, Serikali imetawala kwa takribani miaka miwili na nusu sasa:-

(a) Je, utaratibu wa kuwekwa kima cha chini cha malipo ya pensheni kwa wazee wastaafu kinachozingatia mabadiliko ya kiuchumi kulingana na gharama za maisha ya sasa ulianza lini na unakadiriwa kukamilika lini?

(b) Je, kwa kutumia Kanuni inavyozingatia dhana iliyodhanimiwa katika Ilani hiyo, mzee aliyestaafu kwa muibu wa Sheria mwezi Januari, 1996 akiwa na mshahara wa Shs.250,000/= kwa mwezi angestahili kulipwa kiasi gani kwa mwezi kuanzia Januari, 2008?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Clemence Beatus Lyamba, Mbunge wa Jimbo la Mikumi lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu unaotumika kuongeza kima cha chini cha pensheni kwa wastaafu ni kwa kuangalia uwezo wa Serikali wa kukusanya mapato yake ya ndani na kwa hiyo uwezo wa kulipa pensheni. Kila mara Serikali inapoona kuwa ina uwezo wa kupandisha kima cha chini cha pensheni inafanya hivyo.

Aidha, ukizingatia gharama za maisha pamoja na kutambua mahitaji ya wastaafu, Serikali inatathmini jinsi ya kujenga uwezo wa kuwaongezea wastaafu pensheni ikiwa ni pamoja na kuangalia uwezekano wa kupandisha kwa kuhusisha kima cha chini cha pensheni cha pensheni na kima cha chini cha mishahara ya sekta ya Umma na kwa kuzingatia ongezeko la gharama za maisha.

(bMheshimiwa Naibu Spika, malipo ya mafao ya pensheni hukokotolewa kwa kutumia vigezo na fomula maalum ambayo inahuisha pamoja na mshahara wa mtumishi na miaka aliyokuwa amefanya kazi. Na, ili ukokotoaji wa mafao hayo uweze kufanyika, kuna mambo mengine ya msingi ambayo ni lazima yahakikiwe. Baadhi ya mambo hayo ni:-(i)Mstaafu awe ametimiza masharti ya pensheni;(ii)Mtiririko wa ajira ya ustaafu uridhishe, aina ya ajira ya mstaafu kama vile (iii)Kuajiriwa katika masharti ya muda na ikiwa (iv)Mstaafu aliwahi kuchukua likizo bila malipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kuwa hatukupatiwa taarifa hizi, haiwezekani kukokotoa kiasi cha pensheni kwa mwezi, kwa mstaafu aliyestaafu kwa mujibu wa sheria Januari, 1996, akiwa na mshahara wa shilingi 250,000/= kwa mwezi.

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya kiufundi sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa suala la malipo ya pensheni kwa wastaafu limekuwa likidorora kwa miaka nenda miaka rudi kwa kipindi kirefu sana na kila mara Serikali imekuwa ijibu, jibu kama ililolitoa sasa hivi Mheshimiwa Naibu Waziri.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kulieleza Bunge lako tukufu sasa ni lini hatimaye mapendekezo ya kuongezeka kwa pensheni kutafanyika ili tufahamu mwisho wa suala hili?

Pili, kwa kuwa wastaafu thamani yao na mtaji wao wakati wakiwa kazini ndiyo ambao ni endelevu mpaka sasa kwa mifuko mbalimbali ambayo ndiyo inaendelea kutunishwa na wafanyakazi wa sasa hivi lakini chimbuko na msingi ni wale waliostaafu miaka ya nyuma.

Kuna kigugumizi gani cha Serikali kuangalia uwezekano wa kunyofoa baadhi ya fedha zinazotumika na mifuko ya pensheni ku-*invest* katika majengo makubwa mengi na miradi kadha wa kadha ili kuwanusuru wastaafu ambao kwa kweli hali zao za maisha zinazidi kuwa duni? Na hali ya maisha inazidi kuwa ngumu wakati wafanyakazi wa kawaida nao wamekuwa wakiongezewa mishahara huku wao wakibaki wakidorora? Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niseme kwamba Serikali haijakaa kimya kuhusu kima cha pensheni kwa wastaafu wake. Kutokea mwaka wa 99 mwaka hadi mwaka kila mwaka pensheni za wastaafu zimekuwa zikiongezwa.

Lakini ninakiri kwamba sio kwa kiasi ambacho kimeweza kumudu hali ya maisha na gharama za maisha za miaka hii. Ndiyo maana nimesema sasa kwa dhati kabisa Serikali imeamua kutazama kwa upya viwango hivi na jinsi pensheni hizi zinavyolipwa. Na nimesema katika jibu langu la msingi kwamba moja ya mambo yanayotazamwa ni jinsi ambavyo inawezekana kuainisha kiasi cha pensheni wanacholipwa wastaafu na kima cha chini cha mshahara. Kuna vigezo vingine ambavyo vinatazamwa kwa mfano *inflation rate* na vingine.

Kwa mimi kusimama hapa na kusema kwamba tathmini hiyo itakuwa tayari na kwa hiyo viwango vipya vya pensheni vitaanza mwakani, haitakuwa jambo la busara. Lakini nataka kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwamba Serikali ina dhamira thabiti na inaliangalia jambo hili kwa upya na muda si mrefu ninaamini kwamba Serikali itakuja na jawabu jipya.

Sasa kuhusu mifuko ya pensheni, hii mifuko iko chini ya Sheria. Kila mfuko una Sheria yake na una fomula unazotumia kwa ajili ya kulipa pensheni za wale ambao watakuwa wamechangia wanachama wale na kwa hiyo siyo jambo linalowezekana kuanza kutoa maagizo ya wao kuanza kulipa pensheni kwa mfumo mwingine ama kwa viwango vingine ambavyo kwa sasa hivi wamejipangia. Lakini ninajua kwamba na wenyewe mifuko hii wanarekebisha viwango vya pensheni mara kwa mara. *(Makofi)*

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo sana la nyongeza. Kwa kuwa wazee wastaafu wanapata pensheni ambayo Waziri vile vile hapa ametuthibitishia kwamba ni kidogo na hivyo wanashindwa kumudu gharama zao mbalimbali kama za matibabu na kadhalika.

Kwa kuwa sera ya sasa inawabagua wazee wenye uwezo, wazee wenye uwezo wanaambiwa waendelee kutoa fedha kwa ajili ya kupata huduma za sasa.

Je, Serikali kwa nini sasa isione kwamba mchango walioutoa hawa wazee waliostaafu kwamba ni muhimu zaidi na ikawaacha kabisa kuwabughudhi katika kuwalipisha tena huduma mbalimbali kama za afya na kadhalika? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nikasema kwamba Serikali kwa kutambua kwamba kima cha chini cha shilingi 21,601 kwa mwezi ni kidogo basi kwa makusudi kabisa Serikali imeamua kutathmini kwa upya kiwango hiki na kutafuta jinsi ambavyo tunaweza kuweka mfumo ambao utarekebisho kiwango hiki cha pensheni na ili wazee hawa waweze kupata kiasi ambacho kitakidhi gharama za maisha yao.

Lakini si kweli kwamba wazee hawa wanabaguliwa. Chini ya Sera ya Wazee, Mtazania yoyote ambaye yuko zaidi ya miaka 60 na kuendelea anatakiwa apate matibabu ya bure kwenye vituo vya afya vya Serikali na hiyo inaonyesha dhamira ya Serikali ya kuendelea kuwatunza wazee wetu hawa. *(Makofi)*

Na. 242

**Huduma za Kibenki Wilayani Mkinga**

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH (K.n.y. MHE. MBAROUK K. MWANDORO)** aliuliza:-

Kwa kuwa huduma za kibenki ni muhimu sana kwa maendeleo ya wananchi, na kwa kuwa Wilaya mpya ya Mkinga haina kabisa huduma za kibenki na badala yake wananchi na taasisi mbalimbali Wilayani Mkinga hupata huduma za kibenki kupitia benki zilizopo Muheza:-

(a) Je, Serikali itawasaidiaje wananchi na taasisi za Wilaya ya Mkinga kwa kuzishawishi Benki za *NBC* na *NMB* na nyingine kufungua huduma za kibenki?

(b) Je, ni kwa nini benki ya NMB inaendelea kuhudumia Wilaya ya Mkinga kupitia tawi lake lililoko Muheza badala ya kutumia tawi la Tanga ambalo liko karibu zaidi na Mkinga kuliko Muheza na kwamba akaunti ya Wilaya ya Mkinga iko *NMB Tanga* na sio Muheza?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mbarouk Kassim Mwandoro, Mbunge wa Mkinga kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa huduma za kibenki katika maendeleo ya wananchi. Hata hivyo, baada ya Serikali kujitoa katika uendeshaji wa moja kwa moja wa shughuli za kibenki nchini, uanzishaji wa huduma za kibenki hutegemea, mipango na tathmini zinazofanywa na mabenki yenyewe. Ufunguzi wa Tawi unazingatia na uwezekano wa kupata faida ambayo hutegemea mwenendo na mazingira ya biashara na uchumi katika eneo linalohusika.

Kwa kuzingatia hilo Serikali itaendelea na hatua za kuimarisha uchumi wa maeneo mbalimbali ya nchi kwa lengo la kuweka mazingira ambayo yatakayovutia mabenki kuanzisha huduma za kibenki kwa ajili ya wananchi na taasisi mbalimbali zilizomo ndani ya Wilaya zetu.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, suala la benki ya NMB kutumia tawi la Muheza kuhudumia Wilaya ya Mkinga wakati akaunti ya Wilaya hiyo iko tawi la Tanga ni la kiutendaji ndani ya benki na ni la uhusiano kati ya benki na mteja ambalo Serikali haiwezi kuingilia. Tunamuomba Mheshimiwa Mbunge kushauriana na uongozi wa Wilaya ya Mkinga na taasisi zake kufanya mazungumzo na *NMB* ili kutatua hili kama linaonekana ni tatizo kubwa.

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuuliza swali moja la nyongeza baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa Wilaya ya Mkinga ni Wilaya mpya na inahitaji msukumo mkubwa ili iweze kuinuka kiuchumi. Moja ya kigezo hicho ni kuwa na benki katika Wilaya hiyo. Je, Mheshimiwa Waziri pamoja na kwamba ni taasisi ambayo inajitegemea. Serikali itakuwa iko tayari kuishinikiza kwa utaratibu nzuri waone umuhimu wa kufungua benki katika Wilaya ya Mkinga?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Rished kama ifuatavyo. Nakubali kwamba Mkinga ni Wilaya mpya na kwamba wanahitaji kweli msukumo wa kipekee wa kutoa huduma za kifedha na kibenki ili maendeleo ya wananchi wale yaweze na yenyewe kuwa ya kasi zaidi.

Lakini naomba nimwambie kwamba Serikali haiwezi kushinikiza benki yoyote kufungua Tawi lolote nchini. Serikali inachoweza kufanya ni kuzungumza na tunafanya hivyo na mabenki yenyewe yanaelewe, yenyewe yako kwenye mazingira ya ushindani na yanafungua matawi pale wanapoona kwamba pana tija na pana umuhimu wa kufungua tawi.

Lakini niseme kwamba kwa Mkinga pamoja na sehemu zingine za nchi, *issue* siyo kufungua tawi la benki. La msingi ni kwamba wananchi wapate huduma za kifedha.

Kwa Mkinga kuna taasisi za kifedha ambazo zinatoa huduma za kifedha na kibenki. Kwa mfano kuna *SCALT* ambao Serikali imeipa shilingi miliioni 100 kama kianzio cha kuwapa wananchi wa Mkinga mikopo chini ya utaratibu wa uwezeshaji wananchi na kukuza ajira.

Kwa hiyo nasema wakati Serikali haitashinikiza benki kufungua matawi. Lakini hapo hapo tutaendelea kuzungumza nao na kujenga hoja ya umuhimu wa kufungua matawi mbalimbali za nchi yetu.

Na. 243

**Kilio cha Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari**

**MHE. YONO S. KEVELA** aliuliza:-

Kwa kuwa kilio kikubwa cha Walimu wa shule za msingi na za sekondari ni kucheleweshwa kupandishwa vyeo na kurekebishiwa mishahara yao baada ya kupandishwa daraja/vyeo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kulitatua tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yono Stanley Kevela, Mbunge wa Njombe Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Serikali wa kutatua tatizo la kuchelewesha kupandishwa vyeo ni kuwapandisha walimu kwa mserereko Walimu wote waliokaa muda mrefu bila kupanda madaraja. Katika Sheria Na. 8 ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2002, Mamlaka ya kupandisha vyeo Walimu ni Idara ya Huduma kwa Walimu *(TSD)*. Katika mwaka 2007/2008, kibali kilitolewa cha kupandisha jumla ya Walimu 38,000 wakiwemo 10,486 wa sekondari, vyuo vya ualimu na wakaguzi na walimu 27,514 shule za msingi waliokuwa hawajapanda madaraja kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliwasilisha *(TSD)* mapendekezo ya Walimu wa sekondari, vyuo vya ualimu na wakaguzi wa shule ambao tayari wamepandishwa madaraja na watumishi 6,230 wamerekebishiwa mishahara yao kulingana na vyeo walivyopewa. Aidha, Wizara inaendelea kurekebisha mishahara kadri barua za kupandishwa madaraja zinavyopokelewa.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Pamoja na majibu mazuri ambayo bado sijaridhika vizuri, naomba nimwulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri anakiri kuwa kuna udhaifu, je, Serikali haioni kwamba ni aibu na ni fedheha kuwa kwa kipndi cha miaka 8 Serikali haikushughulikia kuwapandisha walimu madaraja na

kusababisha mlundikano wa walimu katika kundi moja yaani daraja moja? Hili ni swali namba moja.

Namba mbili. Kwa kuwa sasa hili swali namba moja nina mfano hai kuna mwalimu wa Igereja anaitwa Aneti Mdong'ala ana zaidi ya miaka mitano amepandishwa daraja lakini marekebisho yake ni matatizo sana. Hii shule ya Igereja iko Njombe kwenye jimbo langu. Kwa kuwa kurekebisha mishahara ya walimu 6,000 tu kati ya walimu 52,000 ni sawa sawa na kutofanya lolote. Kwa sababu ni kama asilimia 12 ni kidogo sana. Je, kwa nini Serikali yaani namahanisha Idara ya Huduma kwa Walimu TSD isitengeneze programu maalum kwa kila inapofika muda maalum walimu wapandishwe kwa kutumia njia ya kompyuta kama nchi zingine zinavyofanya?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA (K.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI):** Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuwapandisha vyeo walimu tumekuwa tukilishughulikia tangu mwaka 2006/2007 na tumekuwa tukiendelea nalo. Hata mwaka 2007/2008 kama alivyojibu Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba tulipandisha walimu 38,000 kwa nchi nzima ambapo wakiwemo na walimu wa sekondari na walimu wa shule za msingi. Lakini kama alivyosema tumegundua kidogo kulikuwa na ucheleweshaji wa aina fulani kutokana na uchache wa watumishi katika Idara ya Utumishi wa walimu na katika kukabiliana na tatizo hilo tuliamua kuwahusisha Wakurugenzi wa Halmashauri ili kuweza kuharikisha zoezi zima, kwa sababu baadhi ya watumishi wa Idara ya Ualimu walikuwa hawafahamu hata walimu wao wako wapi. Kwa hiyo walimu wanapandishwa vyeo barua zao wanachelewa kuzipata. Kwa hiyo, katika kuliharakisha mwaka huu tuliamua baadhi ya walimu kurekebishia mishahara yao hata kabla hatujawapatia barua. Tume ya Utumishi wa Umma imeamua kutoa mapendekezo ambayo yatatusaidia katika kuharakisha masuala mazima ya kuwapandisha vyeo walimu ikiwa ni pamoja na kuangalia muundo wao. Kwa hiyo, hilo suala tunalifanyia kazi na tutatoa mapendekezo ili kuondokana kabisa na kero ambazo walimu wanazipata.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuniruhusu kupata nafasi ili niulize swali la nyongeza. Katika jibu la msingi na jibu la jibu la pili wamesema wamepandisha walimu 38,000. Lakini katika uchambuzi wetu katika Chama Cha Walimu walimu waliopaswa kupanda ni walimu 70,000. Sasa hawa walimu waliobaki ambao hawakupandishwa kuna utaratibu gani na haoni kwamba ni kuwakatisha tamaa hao ambao walistahili kupanda na hawakuweza kupanda? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA (K.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika chama cha walimu walileta mapendekezo ya walimu zaidi ya 70,000 ambao walipendekeza wapandishwe. Lakini baada ya uchambuzi walionekana kwamba kweli wana sifa za kuweza kupandishwa ni hao 38,000 ambao kwa kweli tumewapandisha na hata hao 38,000 ambao tuliona wanastahili kupandishwa walivyopelekewa barua zao walimu karibu 5,000 hawakuwepo kabisa.

Kwa hiyo, kuonyesha kabisa kwamba hata hao 38,000 ambao sisi tulikubali walimu 5,000 wameshindwa kabisa kuonekana wako wapi.

Na. 244

**Wananchi wa Pangani kununuliwa kivuko kipya**

**MHE. JUMA S. OMAR (K.n.y. MHE. RIZIKI O. JUMA)** aliuliza:-

Kwa kuwa kivuko cha Pangani ni kibovu na kinawasababishia wananchi wa Pangani usumbufu wa usafiri na kuhatarisha maisha yao:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwanunulia kivuko kipya wananchi hao ili kunusuru maisha yao?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Kivuko cha Pangani kinachotumika kwa sasa kilinunuliwa na Serikali mwaka 1972 na kina uwezo wa kubeba tani 35. Wizara kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) imekuwa ikikifanyia matengenezo ya mara kwa mara kivuko hicho ili kiweze kutoa huduma ya kuvusha abiria wakati wote. Kivuko kilisimamishwa tarehe 2 Mei, 2008 kwa ajili ya kufanyiwa ukarabati mkubwa wa bodi, milango, na mifumo ya umeme na kuweka mabomba mapya. Kazi hii imekamilika na kivuko kimeanza kazi tena tarehe 14 Julai, 2008. Pamoja na juhudi hizo za kukiimarisha kivuko cha zamani, Wizara ya Miundombinu kupitia Wakala wake wa Barabara, *TANROADS* imekamilisha taratibu za ununuzi wa kivuko kipya cha Pangani chenye uwezo wa kubeba tani 50, yaani magari madogo 8 na abiria 130. Mkataba wa kununua kivuko hiki ulisainiwa tarehe 27/05/2008 kati ya *TANROADS* na kampuni iliyoshinda zabuni ya Jons Gram Hanssen AS ya Denmark kwa gharama ya *Euro* 1,055,000 sawa na shilingi bilioni 2. Muda wa kuleta kivuko hiki ni miezi 12 baada ya kusaini mkataba.

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kwanza kabisa nataka nichukue nafasi hii kuwashukuru wale wote ambao walituletea salamu za rambi rambi kwa maafa ya kuzama mtumbwi katika sehemu ya Kitanga Ukerewe ambako tumepoteza watoto kati ya miaka 12 na mwaka mmoja wapatao 11. Namshukuru zaidi Waziri Mkuu tulizipata salamu zako.

Swali la nyongeza ni kwamba nakubaliana na muuliza swali kwamba ni usumbufu lakini mimi naongeza kwamba pia ni hatari kwa maisha ya wananchi wakati hakuna usafiri wa kuaminika. Swali langu ni kwamba kwa kuwa katika Visiwa hivi vya

Ukerewe tumekuwa na tatizo kama hili ambalo linawapata wenzetu katika eneo la Pangani na kila mara tunapata maafa ya kupoteza maisha ya wananchi kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo za kijiografia lakini pia zikiwemo na sababu za kutokuwa na vyombo vya usafiri vya kuaminika. Je, Serikali inaweza kuwaahidi wananchi wa Ukerewe kwamba tupate kivuko kingine katika sehemu ya magharibi ya Kisiwa cha Ukerewe kwa kuunganisha na visiwa vingine vipavyo 30 ambavyo havina usafiri wa kuaminika?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami niungane na wananchi wa Ukerewe kutoa rambi rambi kwa msiba huu ambao umetokea katika Ziwa Victoria karibuni na Serikali yote kwa ujumla inasononeka sana wakati kunatokea misiba hii kwenye vyombo vyetu vya usafiri. Upande wa vivuko kwa Ukurewe sasa hivi tuna vivuko viwili ambavyo vinafanya kazi vizuri ni kile cha Kisoi-Lugezi, Visabasaba na MV Nyerere kinachofanya kazi Bugorola na Ukala.

Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kama vile katika maeneo mengine ya Ziwa Victoria na katika Ziwa Nyasa, Ziwa Tanganyika, tutaendelea, Serikali itaendelea kufanya juhudi kuhakikisha kwamba tunapata vivuko madhubuti na vyenye usalama ili vikidhi haja ya kuwavusha wananchi katika maeneo hayo kwa uhakika.

Na. 245

**Vifaa vya Kisasa Kutolewa kwa Hospitali Teule**

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA (K.n.y.MHE. MWANNE I. MCHEMBA) a**liuliza:-

Kwa kuwa, baadhi ya Wilaya mpya zilizoanzishwa hazina hospitali za Serikali ila hutumia hospitali teule ambazo mara nyingi ni za mashirika ya dini, *NGO's* na watu binafsi; na kwa kuwa Serikali kwenye mpango wa kuboresha hospitali hutoa vifaa vya kisasa kama vile *x-ray, ultra sound* na mashine za kupimia *HIV/AIDS.* Je, vifaa vitatolewa lini kwa hospitali hizo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII a**jibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba katika wilaya ambazo hakuna hospitali za Serikali, Wizara huteuwa na kutoa kibali kwa hospitali za mashirika ya dini katika maeneo husika ili hospitali hizo ziweze kutoa huduma za afya kama hospitali za wilaya.

Vile vile, ni kweli kwamba katika mpango wa kuboresha huduma za uchunguzi Wizara huzipatia hospitali zote zikiwemo zote hospitali teule, vifaa vya kisasa kama vile *x-rays* na *ultra sound.*

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa jumla ya hospitali teule 18 kati ya 24 tayari zimekwishapatiwa vifaa hivyo.

Aidha, hospitali teule ya Murugwanza – Ngara ilipatiwa mashine ya *ultra sound* tu kwa kuwa ilikuwa na mashine ya *x-ray* inayofanya kazi. Hospitali ambazo bado hazijapatiwa vifaa hivyo, zimeingizwa katika awamu ya pili ya mradi wa *ORET* ambao unatarajiwa kuanza mwaka 2008/2009. Ni matarajio yetu kuwa utekelezaji wa mradi huo utawezesha hospitali zote za Serikali na teule kupata vifaa vya kisasa ili kuboresha huduma za uchunguzi wa magonjwa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mashine za kupimia *VVU/UKIMWI* yaani *CD4 counts* zimegawiwa katika hospitali zote za rufaa na mikoa. Aidha juhudi zinaendelea ili kuhakikisha hospitali zote za wilaya zinapatiwa mashine hizi.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipatia nafasi ili niweze kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Vifaa katika hospitali ndiyo muhimu zaidi ili kuhakikisha mtu anaumwa nini. Je, Serikali inatambua sasa kuna tatizo pale Moi la *CT SCAN* ambayo ni mbovu?

La pili, je ni lini sasa hizo hospitali 6 ambazo amesema kwamba bado hawajapeleka hizi *X-Ray* na *ultra sound* lina hospitali hizo zitapalekewa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *CT scan* ambayo ni mbovu pale Moi, sasahivi Serikali inalifanyia kazi hilo na tatizo lilikuwa ni *printer* ambayo sasahivi inashugulikiwa iweze kununuliwa na itakapokuwa tayari itafungwa pale na itaendelea kufanya kazi. Na kuhusu suala la *x-ray* kama nilivyosema katika jibu langu la msingi nimesema kwamba wilaya ambazo bado hazijapatiwa *x-ray* huu mradi wa *ORE* ambao tunategemea kuunza mwaka huu wa fedha 2008/2009 utakapokuwa tayari basi tutaweza kuzipatia zile hospitali ambazo hazina *x-ray* pamoja na *ultra sound,* asante sana.

**MHE. JUMA S. NHUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwa kuwa, chombo cha *CT scan* ni chombo muhimu na Muhimbili ni kimoja tu.

Je, Serikali haioni kwamba sasa kuna haja ya kuwa na *set scan* nyingine mpya pale Muhimbili?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII (MHE. DR. AISHA O. KIGODA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nhunga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba kifaa cha *CT scan* ni muhimu si kwa Muhimbili tu lakini katika hospitali zote za rufaa na ingewezekana hata tungeweka katika hospitali za mikoa. Lakini kutokana na ufinyu wa Bajeti hiyo tuliyonayo, hiyo ndio ambayo kwanza inafanya kazi, baadaye tukipata pesa tutanunua na nyingine na tukiweza pia tuweze kupeleka katika maeneo mengine ya rufaa ili watu waweze kupata huduma hii.

Na. 246

**Matumizi ya Chupa za Plastiki Kuuzia Juisi na Maziwa**

**MHE. KHADIJA SALUM ALLY AL-QASSMY K.N.Y. MWAJUMA HASSAN KHAMIS** aliuliza:-

Kwa kuwa, baadhi ya wafanya biashara ya kuuza juisi na maziwa hutumia chupa za plastiki zilizokwisha tumika kwa kuuzia maji ya kunywa:-

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII – MHE. DR. AISHA O. KIGODA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naoma kujibu swali la Mheshimiwa Mwajuma Hassan Hamisi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo. Lakini kabla ya kujibu swali lake naomba nitoe maelezo mafupi sana ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, vifungashio ni nyenzo muhimu katika shughuli za usindikaji vyakula na kila kifungashio kinaweza kutumika kwa aina fulani tu ya bidhaa. Vifungashio husaidia kuhifadhi chakula kiwe salama kwa kukikinga kiwe salama dhidi ya uchafuzi wa kemikali, vimelea vya magonjwa na uchafu mwingine na hivyo kukifanya kiwe na muda mrefu wa mafumizi yaani *shelf life.* Kutokana na hali hii miongoni mwa hatua zinazochukuliwa wakati wa usajili wa vyakula unaofanywa na Mamlaka ya Chakula na Dawa ni kufanya tathmini kama kifungashio hicho kinafaa kwa matumizi ya chakula kilichofungashwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo mafupi sasa napenda kumjibu Mheshimiwa Mbunge, kama ifatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kurudia matumizi ya vifungashio unaweza kutumika pale tu ambapo kuna mitambo maalum na mfumo wa usafishaji na udhibiti wa ubora wa bidhaa, yaani *Quality control,* ambayo hutoa uhakika wa kiwango cha usafi na usalama wa vifungashio kabla ya kutumika tena kufungashia chakula, maji, juisi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya marudio ya chupa za plastiki zilizokwishatumika yanayofanywa na wafanyabiashara wadogo wa juisi na maziwa hayatoi uhakika wa usalama kwa sababu:-

(i) Kuna uwezekano wa uchafuzi wa chupa kutokana na kemikali, vimelea vya magonjwa na uchafu mwingine kutokana na kukosekana vifaa na mfumo mzuri wa usafishaji chupa na vifuniko na ugumu wa usafishaji kutokana na umbile la chupa.

(ii) Matumizi ya chupa hizo bila kutambua ikiwa chupa hizo zinafaa kwa matumizi ya aina ya chakula yanaweza kusababisha kemikali za chupa kuingia kwenye chakula na kukifanya kisiwe salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo ni kutokana na hali hiyo ndiyo sababu Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii inakataza matumizi ya aina hiyo ya chupa kwa sababu ni hatari kwa afya za watumiaji.

**MHE. KHADIJA SALUM ALLY AL-QASSMY:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Naibu Waziri, kimsingi amejibu kwamba chupa za plastiki zinaleta madhara makubwa na kwa kuwa, kwa kupitia Bunge hili ametoa angalizo kwa watumiaji kwamba wasitumie. Sasa kwa kuwa, watu wengi vijijini ndio hasa ambao wanatumia, je, Serikali haioni sasahivi kwamba kuna umuhimu wa kutoa elimu ya kutosha ili wananchi wasije wakadhurika?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII – MHE. DR. AISHA O. KIGODA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Al-Qassmy, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi. Ni kweli kabisa kwamba chupa za *plastic* zinaporudiwa, kama hazikuhudumiwa vizuri ili ziweze kutumiwa mara ya pili, zinaleta madhara. Kwa maana hiyo sasa ni kwamba Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, kwa kutumia wataalamu wake walioko kule Tawala za Mikoa, wahakikishe kwamba wanawafundisha na kuwaelekeza wananchi kwamba kutumia chupa katika mazingira machafu yanaendeleza kuchafua *juice* na maziwa ambayo tunauza kule lakini vilevile inahatarisha maisha ya wananchi. Kwahiyo elimu hii kweli ni muhimu, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Maswali yamekwisha na muda umekwisha. Waheshimiwa nina taarifa ya msiba, Mheshimiwa Mwenzetu Severina, amefiwa na mototo wake. Nadhani watoto wale tuliwatambulisha hapa juzi walikuwa wamefika hapa wanarudi shuleni Dar-es-Salaam.

Hapo Gairo yule binti yake na Mheshimiwa Severina Mwijage, amefariki. Na katika safari hiyo pia walikuwa na watoto wa Mheshimiwa Merci, sasa wengine ni wagonjwa sana wako hapo Gairo.

Kwahiyo Ofisi na Kiongozi ya Kambi ya Upinzani, wanakwenda kuona cha kuweza kufanya, kwahiyo ni leo hii asubuhi, kwahiyo tuna masikitiko hayo tunamsiba. Taarifa zaidi tutawapa baadaye mchana, poleni sana jamani.

Kwa hiyo, tunao wageni hapa, Wageni ambao tulionao hapa kwanza ni wageni wa Mheshimiwa *Professor* Juma Kapuya, Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, unajua tena Wizara yake. Yupo Mke wake pamoja na familia yake wasimame, asante sana.

Kwahiyo Wizara yake pia imeleta watendaji wengi hapa Bungeni wakiongozwa na Katibu Mkuu Dokta Komba na kwa sababu maalum yuko na huyo Naibu Katibu Mkuu, huyo *Mrs.* Magesho.

Kwa hiyo, wapo Wakuu wa Idara wote na wengine watendaji wote wako wengi. Tuna wageni wa Mheshimiwa *Captain* John Chiligati, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ni wanafunzi 60 na walimu kutoka shule ya *Amani Girls Secondary School* ya Manyoni Mjini, naomba wasimame walipo pamoja na walimu wao. Asanteni sana karibuni sana, tunawatakia masomo mema.

Halafu tuna mgeni wa Mheshimiwa Ruth Msafiri, yeye ni Bwana Benjamin Msafiri, yaani ni mototo wake huyu, yeye anasoma sekondari huko *Green Acres Secondary School Dar-es-Salaam.* Yuko wapi Benjamin? Haya asante sana. *(Makofi).*

Tuna wageni wa Mheshimiwa Cosmass Masolwa na Mheshimiwa Othman Ally, wao ni Makatibu wa Matawi matano, matawi mengi sana. Wageni hao Waheshimiwa wasimame wote waliko. Asanteni sana, karibuni sana, ni wageni wanahusika na chama na huko Majimboni kwao.

Tuna wageni wa Mheshimiwa *Professor* Raphael Mwalyosi, hawa ni waheshimiwa Madiwani, wasimame walipo?

Hao hawapo Pamoja na hao tuna wageni wa Mheshimiwa Mohamed Missanga, ni wanafunzi 90 na walimu wao kutoka *Paloti Girls Secondary School,* Sayuni Wilaya ya Singida Vijijini wakiongozwa na Mwalimu Assey na Mwalimu Tungaraza.

Naomba wasimame walipo na walimu, ooh, wamependeza sana. Karibuni sana tumefurahi sana kuwa na ninyi na mukazane kusoma kusudi murithi viti hivi vilivyomo humu ndani. Halafu tuna wageni wa Mheshimiwa Dr. Mzindakaya.

Hawa ni *Mr.* Ashraf *and a Secretary Ministry of Foreign Affairs* na *Mr.* Amra Ahmed, *Director General of Onasis Company* ya Misri. *Welcome to our house and conference, thank you very much. (Makofi).*

Tena tuna wageni wa Mheshimiwa Shah, naomba wasimame walipo. Tuna *SHINAWATA,* Shiririka la Vyama Vya Watu Wenye Ulemavu wako 25, wako humu ndani? Walipo wasimame nadhani watakuwa kwenye *basement.* Kuna wageni wa Mheshimiwa Idd Azzan Zungu, hawa ni ndugu Agustino M. Tefu, Katibu Mkuu wa Chama Cha Wanafunzi wa Sekondari Tanzania na Katibu Mkuu wa *UVCC* Dar-es-Salaam, Kata ya Mabibo tawi la Matokeo, lipo wapi sijui? Karibu sana.

Waheshimiwa pia, naomba nitangaze shughuli za kazi. Dokta Harrison Mwakyembe, Makamu Mwenyekiti Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati hiyo kukutana leo tarehe 18 saa 4.30, nadhani baada ya hapa katika ukumbi chumba namba 227.

Kuna Mheshimiwa John Cheyo, Mwenyekiti Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali, anaomba niwatangazie wajumbe wake kuwa wakutane leo saa 7.00 mchana katika ukumbi chumba namba 231.

Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya *UKIMWI* anaomba niwatangazie wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya masuala ya *UKIMWI* kwamba kesho, Jumamosi tarehe 19 Julai, 2008 watakuwa na kikao na watendaji wa *Human Development Trust* kuanzia saa 4.00 asubuhi katika ukumbi wa chumba namba 227 jengo la Utawala. Hawa ni kesho saa 4.00 chumba namba 227.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo tunaendelea na ratibu. Katibu, endelea na *Order Paper.*

## MAELEZO BINAFSI YA WABUNGE

### UFAFANUZ I WA MATAMSHI YAHUSUYO TAARIFA YA SEKTA YA MADINI

**MHE. DR. JOHN S. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa maelezo binafsi Bungeni, chini ya kanuni ya 50 fasili ya (1) na (2) ya kanuni za kudumu za Bunge, toleo la mwaka 2007. Maelezo ninayotaka kuyatoa yanalenga kufafanua kuhusu matamshi niliyoyatoa hapa Bungeni, Jumatano tarehe 9 Julai, 2008 wakati wa mjadala wa Makadirio na mapato ya matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka 2008/2009. Matamshi ambayo baadhi ya magazeti yameamua kuyapotosha au kuyapa tafsiri ya kichochezi kwa makusudi mazima. *(Makofi).*

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kwamba asubuhi ya tarehe 8 Julai mwaka 2008, Waziri wa NIshati na Madini, Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, aliwasilisha mezani hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Nishati na Madini kwa mwaka 2008/2009 sambamba na taarifa ya madini ya Kamati ya Rais, ya kuishauri Serikali kuhusu usimamizi na sekta ya madini.

Kutokana na umuhimu wa taarifa hiyo na kwa mustakabali wan chi yetu, ukweli kwamba Waheshimiwa Wabunge, hawakupewa fursa mapema nay a kutosha kuisoma na kuielewa taarifa hiyo yenye kurasa 172 na juzuu la viambatanisho lwenye kurasa 85. Ili waweze kutoa michango ya maana Bungeni na ugumu kwa Waheshimiwa Wabunge, kuchangia kuhusu hotuba ya Waziri, na taarifa ya madini kwa pamoja katika muda mfupi wa dakika 15, nikaona niombe mwongozo wako ili kama inawezekana taarifa ya madini itafutiwe muda maalum wa kuijadili. *(Makofi).*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu hilo ambalo lilipokelewa vizuri sana na Waheshimiwa Wabunge na wewe mwenyewe kuliridhia kwa maelezo kuwa suala la madini lina maslahi ya Taifa limetafsiriwa na baadhi ya vyombo vya habari kiuchochezi kuwa ilikuwa na lengo la kuitega Serikali ya *CCM.* Huu ni upotoshaji mkubwa wa nia nzuri niliyokuwa nayo ya kuliwezesha Bunge, kuijadili taarifa hiyo kwa kina ili taifa lipate sera na sheria bora za Wizara ya Madini. *(Makofi).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, aliunda Kamati ya Rais ya Madini, kwa nia njema sana ya kuitafutia sekta ya madini ufumbuzi wa kudumu wa matatizo mbalimbali ya kisera na kisheria mabayo ni matatizo yaliyoko Wizarani.

Aidha uundaji huo wa Kamati ya Madini ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya *CCM* ambayo katika ukurasa wa 42 inatamka wazi kuwa Serikali ya *CCM* itapitia upya sera ya madini kwa lengo la kuiboresha katika maeneo mbalimbali. Uamuzi ulioutoa wa kulipa suala hili muda maalum wa kulijadili ni mzuri na wenye tija kwa Taifa letu.

Hizi tafsiri za kwamba hatua hii ni mtego kwa serikali ni porojo na upotoshaji wa kitoto usio na nia njema kwa nchi yetu ambao niliona niutolee maelezo katika Bunge lako Tukufu siku ya leo. *(Makofi).*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru tena kwa kunipa nafasi hii adimu na adhimu. Asante. *(Makofi).*

**NAIBU SPIKA:** Asante. Hapa kuna Mheshimiwa Zitto, anasema hii taarifa ilitakiwa iwe kwenye *adjourn motion* sasa nitakueleza baadaye kwasababu ziko hoja mbili. Iko hii hoja ambayo Mbunge anataka kujieleza mwenyewe, wala hamuulizi mtu amjibu hapa wala haulizi Serikali, ndio hii ya Mheshimiwa.

Hii inapata *priority,* kama kungekuwa na Kauli ya Waziri, ingekuwa ya kwanza halafu hii ingefuata.

Hii unayozungumza *adjourning motion* ni kwamba Mbunge, hajaridhishwa na Serikali kwa jambo lolote lililomo humu ndani ama lililosemwa humu ndani ama kauli yoyote ya Serikali, basi Mbunge anasema hivi kusudi ajibiwe. Sasa kanuni yake nitakupa baadaye, sasa hizi sina saa hizi, kwahiyo iko *in order.* Katibu. *(Makofi).*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2008/2009 - Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na Taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii inayohusu Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, na kwa kuzingatia Taarifa hiyo, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali kujadili mpango wa kazi na kupitisha makadirio ya matumizi ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi, *Commision of Mediation and Arbitration,* kwa mwaka wa fedha wa 2008/09.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda nitumie fursa hii na ya kipekee kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Nchi za Afrika. Kuchaguliwa kwake kunadhihirisha uwezo na imani kubwa waliyo nayo viongozi wa nchi za Afrika kwake binafsi na Taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru pia na kwa namna ya pekee kabisa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani yake na heshima kubwa aliyonipa kwa kuniteua mimi kuiongoza Wizara hii muhimu sana kwa maendeleo na ustawi wa Watanzania. Aidha napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda Mbunge wa Mpanda Mashariki kwa kuteuliwa kwake na hatimaye kuthibitishwa kwa

kura nyingi na Bunge hili Tukufu kuwa Waziri Mkuu wa 10 wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Benidict Ole Nang'oro, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mbunge wa Kiteto. Ushindi wake ni kielelezo tosha cha kuonesha imani na matumaini makubwa waliyonayo wananchi wa Tanzania kwa Chama chao cha Mapinduzi. Aidha, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Hajat Al-Shaymar Kwegyir, kwa kuteuliwa kwake kuwa Mbunge lakini vilevile nampongeza sana Mchungaji Dokta Getrude Lwakatare kwa kuwa Mbunge wa Viti Maalum kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa napenda kujiunga na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole za dhati kwa jamaa na familia za Wabunge wenzetu waliofariki dunia katika kipindi hiki cha mwaka mmoja, marehemu Mheshimiwa Salome Joseph Mbatia ambaye hadi anafariki alikuwa Naibu Waziri, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na marehemu Mheshimiwa Benedict Losurutia aliyekuwa Mbunge wa Kiteto. Tunamwomba Mwenyezi Mungu awajalie ndugu wa marehemu mioyo ya subira na azilaze roho za marehemu hao mahali pema peponi - Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii pia kuwakumbuka na kuwaombea kwa Mungu ndugu waliofariki katika ajali iliyonipata 24/09/2007 wakiwemo Ndugu Twaha Ramadhani Ngosso aliyekuwa Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Urambo, Mheshimiwa Haruna Shamshery aliyekuwa Diwani Kata ya Ushokola, *Private* Khalfan Zakaria Kiroko na *Private* Ramadhan Waziri Mwengere waliokuwa ni Askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Aidha natoa pole kwa wale wote walioumia au walionusurika kwenye ajali mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Peter Kayanza Pinda, Waziri wa Fedha na Uchumi Mheshimiwa Mustafa Haridi Mkulo na Mawaziri wote walionitangulia kwa hotuba zao nzuri zilizoelezea vyema mipango ya Serikali katika mwaka wa fedha wa 2008/2009. Napenda kutumia fursa hii pia kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho na Makamu Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Haroub Masoud Mbunge wa Koani, iliyojadili na kuyakubali makadirio ya matumizi ya Wizara yangu tarehe 25 Juni, 2008. Hotuba hii imezingatia ushauri uliotolewa na Kamati ambao tunaamini utaiwezesha Wizara kuongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu yake katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Majukumu ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana yamegawanyika katika sehemu kuu tatu:-

(a) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera na Sheria za Kazi .

(b) Kuzuia migogoro ya kikazi, kwa kufanya kaguzi na kutoa elimu katika sehemu za kazi.

(c) Kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria na mikakati ya ukuzaji wa ajira nchini, hususan upatikanaji wa ajira mpya zisizopungua milioni moja ifikapo mwaka 2010.

(d) Kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Uchumi kuratibu Mpango wa uwezeshaji wananchi kiuchumi na kukuza ajira, hususan mpango wa mikopo yeneye masharti nafuu kwa wajasiriamali wadogo na wa kati.

(e) Kuratibu na kusimamia mipango ya maendeleo ya vijana kiuchumi, kisiasa na kijamii.

(f) Kuratibu na kusimamia shughuli za mbio za Mwenge wa uhuru nchini.

(g) Kuratibu shughuli za vyama vya wafanyakazi na vyama vya waajiri.

(h) Kusimamia mipango ya usalama na afya za wafanyakazi mahali pa kazi, *Occupational Health and Safety,* kupitia Wakala wa Usalama na Afya Mahala pa kazi, *OSHA.*

(i) Kusimamia mipango ya uboreshaji wa tija na ufanisi kazini kupitia Shirika la Tija la Taifa, *NIP.*

(j) Kutoa miongozo ya uendeshaji na kusimamia kazi za wakala na taasisi zifuatazo:-

(i) Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii, *NSSF*, linalohusika na ukusanyaji wa michango, uwekezaji na utoaji wa mafao kwa wanachama wake.

(ii) Shirika la Tija la Taifa, *NIP*, linalohusika na uboreshaji wa tija na ufanisi kazini.

(iii) Wakala wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi, *Occupation of Safety and Healthy Authority,* linalohusika na ukaguzi na kuhakikisha kuwa Waajiri wanazingatia viwango vya usalama na afya sehemu za kazi.

(iv) Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania, *Tanzania Employment Services Agenchy,* unaohusika na kuunganisha watafuta kazi na waajiri ili kukuza ajira kwa kusaidia kuhakikisha wafanya kazi wanapata kazi wanazostahili.

(v) Tume ya Usuluhishi na Uamuzi, *Commission of Mediation and Arbitration*, inayohusika na utatuzi wa migogoro inayotokea sehemu za kazi kwa njia ya usuluhishi na kutoa uamuzi wenye nguvu ya kisheria.

(vi) Ofisi ya Msajili wa Vyama Huru vya Wafanyakazi na Waajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kusimamia utekelezaji wa majukumu haya Wizara inaongozwa na Sheria, sera na Miongozo ifuatayo:-

(a)Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025.

(b)Mkakati wa kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Tanzania, *MKUKUTA.*

(c)Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2005 – 2010.

(d)Malengo ya Maendeleo ya Milenia, *MDGs.*

(e)Sera ya Taifa ya Ajira ya mwaka 2008.

(f)Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2007.

(g)Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii ya Mwaka 2003.

(h)Sheria za Kazi Na. 6 ya mwaka 2004 ya ajira na Mahusiano Kazini na Na.7 ya mwaka 2004 ya Taasisi za kazi.

(i)Sheria ya Malipo ya Fidia ya Wafanyakazi wanaoumia kazini ya mwaka 1949, *Worker's Compensation Act.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Kazi kwa Mwaka 2007/2008 na Malengo ya Mwaka 2008/2009. Katika mwaka 2007/08 Wizara yangu iliendelea na utekelezaji wa Sheria mpya ya kazi, yaani Sheria Na. 6 ya mwaka 2004 ya Ajira na Mahusiano Kazini na Na.7 ya mwaka 2004 ya Taasisi za Kazi.

Madhumuni ya sheria hizi ni kutoa haki na wajibu kwa wafanyakazi na waajiri ili kuongeza tija, ufanisi na uhusiano mwema katika sehemu za kazi. Hivi ni vigezo muhimu katika kukuza uchumi na ajira kwani vinavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi. Kazi moja kubwa iliyofanywa katika kipindi hiki ni kuunda Tume ya Usuluhishi na Uamuzi, *CMA,* kwa mujibu wa Sheria ya Taasisi za Kazi, na Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania, *TAESA.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi nyingine iliyofanywa na wizara yangu katika kipindi hiki ni maandalizi ya sera, programu na mikakati ya kukuza ajira nchini, ambayo itakuwa ndiyo dira ya kuongoza mapambano dhidi ya tatizo la ukosefu wa ajira na hasa miongoni mwa vijana. Katika kuandaa mipango hii, sera ya Maendeleo ya vijana ya 2007 iliandaliwa na kuanza kutumika kwenye kipindi hicho. Wizara ilishirikisha wadau mbalimbali zikiwemo Wizara zote, Serikali za Mitaa, viongozi wa sekta binafsi, Vyama vya Wafanyakazi, Chama Cha Waajiri, *NGOs,* na Waheshimiwa Wabunge ambao

walipata kutoa maoni kupitia fursa na nafasi mbalimbali. Aidha waraka ulianzishwa wa kuratibu na kusimamia masuala yote ya kuwasajili na kuwaunganisha waajiri na watafuta kazi, *Tanzania Employment Services Agenchy – TAESA.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sura kamili ya kazi zilizofanywa na Wizara yangu katika kipindi cha mwaka 2007/08 ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, A: Maendeleo Ya Usimamizi Kazi na Huduma za Ukaguzi. Kwa kusimamia sheria za kazi kumekuwepo mahusiano mazuri katika maeneo mengi ya kazi na hivyo kuleta amani na utulivu kazini ambayo ni moja ya vivutio muhimu kwa wawekezaji. Kwa sababu hiyo katika kipindi hiki palitokea migogoro michache ambayo ilipatiwa ufumbuzi, ukiwemo mgogoro wa Kiwanda cha kuzalisha sukari Moshi, *TPC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2007/2008. Katika kipindi cha mwaka 2007/2008 Wizara ilitekeleza malengo yafuatayo:-

(a) Marejeo na marekebisho ya sheria za kazi na ajira awamu ya pili yaliendelea kufanywa. Sheria ya Hifadhi ya Jamii, *Social Security Regulatory Act*, imepitishwa kwenye kiako cha Bunge cha mwezi april 2008. Sheria ambazo bado ziko kwenye hatua mbalimbali za marekebisho ni pamoja na Sheria ya Usalama na Afya mahali pa kazi na sheria ya huduma na kukuza ajira.

(b)Imeendelea kuratibu shughuli za Baraza la kazi, Uchumi na Jamii, *LESCO,* kwa kufanya vikao vitano vilivyojadili mambo mbalimbali yahusuyo kazi. Miongoni mwa ushauri uliotolewa na *LESCO* ni mapendekezo ya marekebisho ya Sheria za kazi.

(c)Imefanya kaguzi 1,274 katika sekta binafsi na Mashirika ya Umma. Kusimamia majadiliano baina ya wafanyakazi na waajiri kwenye Taasisi 34 ambapo 3 kati ya hizo ni za watu binafsi.

(d)Imewezesha Bodi 8 za mishahara za kisekta kukamilisha zoezi la awali la kupanga vima vya chini vya mishahara katika sekta binafsi na hatimaye kutangazwa rasmi Novemba, 2007.

(e)Imemteuwa mshauri mwelekezi, *consultant,* ili kufanya utafiti kuhusu uwezo wa kulipa na athari za viwango vipya vya mishahara katika sekta binafsi.

(f)Migogoro 85 ilipokelewa kutoka kwa waajiri na wafanyakazi. Aidha migogoro 92 ikiwemo ile ya nyuma na iliyopokelewa imeshughulikiwa na kuwasilishwa Mahakama ya kazi kwa uamuzi.

(g)Kiasi cha shilingi 21,600,000/= zimelipwa kama fidia kwa wafanyakazi 200 walioumia au kupata madhara wakiwa kazini.

(h) Katika kuimarisha ushirikishwaji wa wafanyakazi katika sehemu za kazi, majadiliano baina ya wafanyakazi na waajiri yamesimamiwa katika Taasisi 34 kati yake 3 ni za watu binafsi.

(i) Imekamilisha utayarishaji wa mwongozo wa kubaini na kuwaondoa watoto katika ajira mbaya.

(j) Imeshiriki katika mikutano inayohusu masuala ya kazi ya *SADC, AU, EAC* na *ILO*. Kufuatia ushiriki huo, Tanzania imechaguliwa kuwa mjumbe wa Baraza la Utawala la *ILO,* yaani (*ILO Governing Body,* kuanzia Juni 2008 hadi 2011.
Malengo yatakayotekelezwa mwaka 2008/2009. Katika mwaka 2008/09, pamoja na shughuli za kawaida Wizara itafanya yafuatayo:-

(a) Kufanya kaguzi za kazi 2,000 katika sehemu za kazi.

(b) Kuendelea kusimamia majadiliano baina ya waajiri na wafanyakazi.

(c) Kukamilisha utafiti kuhusu athari za viwango vipya vya mishahara katika sekta binafsi, vilivyoanza kutumika Januari 2008, na kutekeleza mapendekezo yatakayoonekana yanafaa kutokana na utafiti huo kwa kuzingatia nguzo yetu ya utatu.

(d) Kuratibu na kusimamia Sera na Sheria za kupambana na Ajira mbaya ya mtoto.

(e) Kukamilisha maandalizi ya Muswada wa Sheria mpya ya fidia kwa wafanyakazi

(f) Kukamilisha maandalizi ya utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii, ikiwa ni pamoja na uundwaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, *Social Security Regulatory Authority*.

(g) Kuednelea kuajiri watumishi zaidi kwa lengo la kukidhi mahitaji halisi.

(h) Kuendelea kushughulikia malipo ya fidia kwa wafanyakazi wanaoumia au kupata madhara wakiwa kazini.

(i) Kuendelea kushughulikia rufaa zilizowasilishwa Wizarani na kushughulikia mashauri yaliyopo katika Mabaraza ya usuluhishi.

(j) Kuendelea kuratibu shughuli za Baraza la Usuluhishi la Kazi, Uchumi na jamii, *LESCO.*

(k) Kukamilisha uchapishaji na pia kutafsiri katika lugha ya Kiswahili kitabu cha "*HIV/AIDS Code of Conduct*".

Mheshimiwa Naibu Spika, B: Ukuzaji wa Ajira Nchini. Katika mwaka wa fedha 2007/08 Wizara yangu imeendelea kuratibu shughuli za ukuzaji wa ajira nchini hususan utekelezaji wa azma ya Serikali ya kuongeza ajira mpya milioni moja ifikapo mwaka 2010. Kwa taarifa zilizopatikana hadi mwezi Juni 2008 jumla ya ajira mpya 437,205 zilikuwa zimezalishwa katika sekta mbalimbali kuanzia Januari 2006 hadi Desemba 2007, sawa na asilimia 43.7 ya lengo la milioni moja hadi mwaka 2010.

Hata hivyo sekta ya kilimo ambayo huchukua zaidi ya asilimia 70 ya watu wanaoingia kwenye soko la ajira kila mwaka, haikuhusishwa katika hesabu hizo. Kiambatisho I, kinaonesha kwa undani zaidi. Takwimu hizi zinaonesha kuwa sekta binafsi inaongoza katika ukuzaji wa ajira nchini. Kwa kuwa suala la ukuzaji wa ajira ni mtambuka hivyo basi ni jukumu la kila mdau kushiriki kikamilifu katika shughuli za ukuzaji wa ajira na kupambana na umasikinui.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2007/2008. Katika kipindi cha mwaka 2007/08, Wizara ilitekeleza kazi zifuatazo:-

(a) Kwa kushirikiana na wadau mbalimbali yamefanywa marekebisho ya Sera ya Taifa ya Ajira ya mwaka 1997 na kupata Sera ya Taifa ya Ajira ya mwaka 2008 iliyopitishwa rasmi na Baraza la Mawaziri mwezi Machi 2008.

(b) Programu ya kukuza ajira imezinduliwa mwezi Agosti 2007 ambayo imeendelea kutekelezwa na wadau mbalimbali katika ngazi zote. Programu hii inalenga kafikia lengo la Serikali la kuzalisha ajira zaidi ya milioni moja ifikapo mwaka 2010. hata hivyo programu hii imebainisha uwezekano wa upatikanaji wa ajira karibu milioni tano endapo itatekelezwa na wadau kikamilifu.

Wizara pia imekamilisha rasimu ya mkakati wa kukuza ajira unaolenga kutekeleza sera ya taifa ya ajira ya mwaka 2008. Sambamba na hili mfumo wa kitaasisi wa kutekeleza mkakati wa kukuza ajira umeainishwa na sasa wizara yangu inaandaa mwongozo kwa ajili ya kuanzisha dawati la kukuza ajira katika ofisi za mikoa na halmashauri zote nchini.

(c) Mpango wa Mafunzo ya kuwezesha wananchi kujiajiri, kuongeza tija na kupunguza umaskini, *Demand driven skills training programme,* umeendelea kutekelezwa kwa kuwapatia mafunzo wajasiriamali wapatao 231 katika Wilaya 9 nchini ambazo ni Karagwe, Ukerewe, Bukombe, Kilindi, Uyui, Babati Vijijini, Arusha, Kilolo na Mbarali.

Mafunzo haya hutolewa katika fani mbalimbali ikiwa ni pamoja na kilimo, ufugaji, ushonaji, elimu ya biashara, utengenezaji wa batiki na ujenzi. Kiambatisho Na.II, kinaonesha ufafanuzi huo kwa kina.

(d) Kushughulikia maombi ya vibali vya kazi kwa wageni. Jumla ya maombi 4,414 yalipokelewa, kati ya hayo 2,555 ni maombi mapya na 1,437 ni maombi ya kuongezewa muda. Jumla ya maombi yaliyokubaliwa ni 3,460. Maombi yaliyokataliwa ni 532. Aidha, Kituo cha Uwekezaji *(TIC)* kilipokea maombi 2,737. Kati ya maombi hayo, maombi 2,647 yalikubaliwa na maombi 47 yalikataliwa kwa sababu mbalimbali zikiwemo za wataalamu husika kupatikana katika soko la ndani la ajira. Maombi 43 yanaendelea kushughulikiwa kwa kuwa yalisitishwa kwa sababu mbalimbali ikwemo ukaguzi. *(Makofi)*

(e) Jumla ya kaguzi 59 zilifanyika sehemu za kazi ili kubaini wageni wenye vibali na wasio na vibali vya ajira *(Work Permits)* nchini.

(f) Iliendelea kuratibu fedha za Mfuko wa Dhamana (*Revolving Loan Fund)* wa Mradi wa Usawa wa Jinsia na Ajira Bora kwa Wanawake. Jumla ya mikopo yenye thamani ya shilingi 888,000,000/= ilitolewa kwa wajasiriamali 3,800 nchini. Mfuko una dhamana ya dola za Kimarekani 261,336.06/=. *(Makofi)*

(g) Kuandaa Rasimu ya Muswada wa Sheria ya Huduma za Ajira ambayo itawasilishwa kwenye Baraza la Mawaziri kwa maamuzi.

(h) Kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, Wizara ya Fedha na Uchumi, Benki Kuu ya Tanzania, pamoja na Baraza la Taifa la Uwezeshaji, Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Kukuza Ajira ambapo katika awamu ya kwanza, hadi Mei 30, 2008 benki za *CRDB* na *NMB* zilikuwa zimetoa mikopo yenye thamani ya shilingi 33,506,494,114 kwa wajasiriamali 44,256. Utekelezaji kimkoa ni kama unavyoonekana kwenye Kiambatisho III.

Aidha, Wizara imepata kutoka Benki Kuu majina yote ya waliokopeshwa na kiasi walichopata kupitia Benki za *CRDB* na *NMB* kwa kila Mkoa na kila Wilaya. Serikali pia imeanza kutekeleza awamu ya pili ya mpango huu kupitia benki na asasi ndogo ndogo 14 za fedha.

Mpango huu umeanza kutekelezwa katika Wilaya 21 zilizokosa mikopo na 46 zilizopata chini ya kiwango katika awamu ya kwanza. Hadi Juni 30, 2008 jumla ya shillingi 2,703,698,650 zilikuwa zimetolewa katika *SACCOS* 132 na wajasiriamali mmoja mmoja 110 katika Wilaya husika. *(Makofi)*

Katika awamu ya kwanza, mpango huu umewezesha wajasiriamali kwa kawaida wasingepata kwa kupitia utaratibu wa kawaida wa benki. Mpango huu pia umehamasisha na kuimarisha dhana ya vyama vya kuweka na kukopa *(SACCOS).*

Aidha, mpango huu umewezesha kufufua miradi ya kilimo iliyokuwa imefifia kwa mfano mradi wa wakulima wa korosho Newala, Tandahimba, (Mtwara), Ruangwa (Lindi) na wakulima wa mpunga na tangawizi Ndugu (Same). Mifano zaidi ya mafaikio na changamoto imeelezwa kwenye kiambatisho Na. V. *(Makofi)*

(i) Iliratibu ushiriki wa wajasiriamali wadogo wadogo katika sekta isiyo rasmi katika maonyesho ya tisa ya nguvukazi/juakali ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yaliyofanyika Nairobi, Kenya kuanzia tarehe 13 - 21 Oktoba 2007. Jumla ya wajasiriamali wa sekta isiyo rasmi 209 walishiriki ambapo wajasiriamali 24 kutoka Zanzibar na 185 walitoka katika mikoa 19 ya Tanzania Bara.

Maonyesho haya yalizihusisha nchi za Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi. *(Makofi)*

(j) Vituo vya *Labour Exchange Centres* viliendelea kutoa huduma kwa wananchi. Hadi Mei 31, 2008 Kituo cha Ajira Dar es Salaam kilikuwa kimeandikisha watafuta kazi 685 ambapo kati yao wanawake walikuwa 206 na wanaume 479. Watafuta kazi waliounganishwa na waajiri ni 285 wanawake wakiwa 107 na wanaume 178. *(Makofi)*

Aidha, Kituo cha Afjira cha Mwanza kilikuwa imeandikisha watafuta kazi 359 wanawake wakiwa 118 na wanaume 241. Watafuta kazi 233 waliunganishwa na waajiri, wanawake wakiwa 34 na wanaume 199. *(Makofi)*

(k) Imeandaa mchakato wa kuifanyia marekebisho Kamusi ya Kazi *(Tanzania Classification of Occupations – TASCO)* ili kuboresha na kuifanya iendane na wakati. *(Makofi)*

(l) Imeandaa mpango kabambe wa kukusanya takwimu za seta ya kazi na ajira na kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu.

(m) Imeendelea na mchakato wa kuimarisha shughuli za kitengo cha kuwaungaisha watafuta kazi nje ya nchi na kuwavutia Watanzania walio nje ya nchi kurudi nchini kuchukua kazi zinazohitaji ujuzi wa kipekee.

Aidha, iliendelea kupokea maoni ya wadau na kubainisha utaratibu wa namna ya kuwaunganisha Watanzania wanaotafuta kazi nje ya nchi. Sanjari na hatua hii mawasiilano na nchi na nchi mbalimbali zikiwemo Falme za Kiarabu ambazo zimeonyesha mahitaji ya wafanyakazi kutoka Tanzania yamefanyika.

Mawasiliano hayo ni pamoja nakufanya uchunguzi wa kina juu ya masuala mbalimbali yahusuyo sheria za kazi na ajira katika nchi hizo, uhalisia na aina ya waajri wanaohitaji wafanyakazi pamoja na mahusiano ya kazi katika nchi husika ili kuwa na uhakika wa usalama wa watu wetu kabla ya kuingia mikataba na nchi husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo yatakayotekelezwa katika kipindi cha mwaka 2008/2009, pamoja na kuendelea kutekeleza shughuli zilizoanza mwaka uliopita na zile za kawaida, majukumu yatakayotekelezwa na Wizara ni pamoja na:-

(a) Kusimamia utekelezaji wa sera ya Taifa ya ajira ya mwaka 2008 na mkakati wa Taifa wa kukuza ajira pamoja na mpango wake baada ya kupitishwa na Serikali.

(b) Kuweka mfumo wa kitaasisi wa kutekeleza sera ya taifa ya ajira ikwemo uanzishwaji wa dawati la ajira katika ngazi za mikoa na Wilaya kwa lengo la kuratibu shughuli za kukuza ajira katika ngazi husika.

(c) Kuendelea kukusanya, kuchambua na kutoa taarifa juu ya hali ya soko la ajira na ukuaji wa ajira nchini.

(d) Kuratibu vikao vya utatu kujadili maombi ya vibali vya wageni vya kufanya kazi nchini.

(e) Kufanya kaguzi mara kww mara za vibali vya kazi kwa wagni wanaofanya kazi nchiji.

(f) Kuimarisha wakala wa huduma za ajira *(TaESA)* kwa kuitangaza na kuelimisha umma kuhusu huduma zake.

(g) Kuratibu utoaji wa huduma za ajira ndani na nje ya nchi kwa kutujia kitengo cha *Cross border placement.*

(i) Kukamilisha muswada wa Sheria ya kukuza ajira na huduma za ajira *(National Employement promotion* na *Service Bill)* Sheria hii ndiyo itakayotoa mwongozo wa Kisheria hii ndiyo itakayotoa mwongozo wa kisheria wa kutekeleza Sera ya Taifa ya Ajira ya mwaka 2008.

(j) Kwa kushirikiana na ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI Wizara ya Fedha na Uchumi, Benki Kuu ya Tanzania pamoja na Baraza la Taifa la la Uwezeshaji, kuendelea kutaribu utekelezaji wa mpango wa uwezeshaji wananchi kiuchimi na kukuza ajira wa wastani wa shilingi bilioni moja kila mkoa.

(k) Kufanikisha ushiriki wa wajasiliamali wadogowadogo wa Tanzania katika maonyesho ya kumi ya Nguvu Kazi/Jua Kali yatakayofanyika Kigali nchini Rwanda kuanzia tarehe 29 Novemba, 2008 mpaka 07 Desemba, 2008.

(l) Kupanua wigo wa utekelezaji wa mradi wa kujenga usawa wa jinsia na ajira bora kwa wanawake.

(m) Kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani *(ILO)* kuanza utekelezaji wa vipengele vya ajira nchini ya mpango wa *One UN Joint Programme,* ikiwa ni pamoja na kufanya utafiri wa sekta isiyo rasmi na kuboresha mfumo wa upatikanaji aw taarifa na takwimu za ajira mpya kwa kuanzia mikoa ya Lindi na Mtwara.

(n) Kukusanya, kuchambua na kutoa taarifa juu ya hali halisi ya soko la ajira na ukuaji wa ajira nchini.

(o) Kufanya kaguzi mara kwa mara za vibali vya kazi kwa wageni wanaofanya kazi nchini ili kubaini na kuwachukulia hatua wale ambao wanafanya kazi kinyume na sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maendeleo ya vijana. Katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kuratibu shughuli zifuatazo muhimu zinazowahusu vijana:-

(a) Kuratibu Mbio za Mwenge wa Uhuru, sherehe za kilele na Wiki ya Vijana kwa mwaka 2007 na uzinduzi wa Mbio hizo kwa mwaka 2008. Kilele cha Mbio za Mwenge wa Uhuru 2007 kilifanyika Mkoani Arusha tarehe 14 Oktoba. Kwa mwaka huo, jumla ya miradi 1,542 yenye thamani ya shilingi 80,533,647,310.17 ilizinduliwa, kufunguliwa na kuwekewa mawe ya msingi. Ujumbe wa Mwenge wa mwaka 2007 ulihusu Mapambano dhidi ya Rushwa, Dawa za Kulevya na Ugonjwa wa UKIMWI.

Aidha vijana kutoka Mikoa mbalimbali walishiriki katika Wiki ya Vijana na maonesho kwa siku saba. Mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2008 zilizinduliwa na Waziri Mkuu Mheshimiwa Mizengo Pinda katika kijiji cha Msoga Mkoani Pwani. Ujumbe wa Mwenge kwa mwaka 2008 ni Hifadhi ya Maji, Mapambano dhidi ya Rushwa, Dawa za Kulevya na Ugonjwa wa UKIMWI. Kilele cha Mbio za Mwenge na Wiki ya Vijana kitafanyika Mkoani Tanga tarehe 14 Oktoba 2008.

(b) Kwa kushirikiana na wadau wa vijana na vijana wenyewe Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2007 iliandaliwa, kuzinduliwa na kusambazwa kwa wadau mbalimbali. *(Makofi)*

(c) Katika kuwajengea vijana uwezo wa kukua kiuchumi na hasa kujiajiri katika sekta isiyo rasmi, Wizara iliendelea kutenga fedha za kuwakopesha vijana na kufuatilia urejeshaji wa fedha hizo. Jumla ya Wilaya 97 zilikopeshwa jumla ya shilingi 364,591,208, na jumla ya shilingi 115,738,246.99 zimerejeshwa wakati jumla ya shilingi 267,082,521.41 bado zinadaiwa (Kiambatisho Na.VI).

Kutokana na hali isiyoridhisha ya urejeshaji wa fedha za mfuko, Wizara imebuni utaratibu wa kuwakopesha Vijana kupitia katika vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo *(SACCOS)*. Ili kutekeleza mpango huu Mikoa iliombwa kuteua na kuwasilisha wizarani majina ya *SACCOS* zinazoweza kutumika. Mpaka sasa jumla ya Mikoa 20 kati ya 21 imewasilisha orodha ya *SACCOS* hizo kama zinavyoonekana kwenye Kiambatisho Na.VII.

(d) Kuendesha mafunzo kwa vijana katika Kituo cha Sasanda Mbeya katika fani ya uongozi, ujasiriamali, utunzaji wa hesabu za fedha na stoo, uanzishaji na uendeshaji wa miradi, uanzishaji na uendeshaji wa vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo *(SACCOS)* kwa vijana 30 kutoka Mikoa ya Iringa, Mbeya na Rukwa.

(e) Mafunzo ya kuwapatia vijana teknolojia ya kutengeneza mkaa kwa kutumia masalia ya mazao na nyasi yamefanyika kwa vijana 40 kutoka Morogoro katika Kituo

cha Vijana Ilonga kwa kushirikiana na wataalamu kutoka *Appropriate Rural Technology Institute (ARTI-TZ).* Lengo la mafunzo haya ni kuwawezesha vijana kujiajiri. *(Makofi)*

(f) Vijana zaidi ya 400 walipatiwa elimu kuhusu VVU/UKIMWI na afya ya uzazi katika Wiki ya Vijana Arusha. Sambamba na mafunzo hayo, vijana 589 walijitokeza kupima virusi vya UKIMWI na kati yao wanaume walikuwa 384 na wanawake walikuwa 205. Waliokutwa wameathirika na VVU/UKIMWI walikuwa ni 18 (sawa na asilimia 3), ambapo wanaume walikuwa ni 8 na wanawake walikuwa ni 10.

(g) Kwa kushirikiana na Taasisi ya Vijana ya UVIKIUTA, kambi kazi mbili za vijana zilifanyika huko Manyoni, Singida na Mto wa Mbu, Monduli, Arusha. Jumla ya vijana 325 kutoka Tanzania, Australia, Slovenia, Ujerumani, Hispania, Uholanzi, Korea Kusini, Ubelgiji, Marekani, Ufaransa, Ireland, Canada, Uingereza na Japan walishiriki katika kambi kazi hizo ambapo vijana waliweza kuchangia nguvu zao katika ujenzi wa madarasa, zahanati na usafi wa mazingira. *(Makofi)*

(h) Kuendelea na mchakato wa kuanzisha Baraza la Vijana Tanzania (BAVITA).

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, vikao viwili vilivyowahusisha vijana, viongozi wa vijana kutoka vyama vyote vya siasa na wawakilishi kutoka taasisi mbalimbali za Serikali na zisizo za Serikali vilifanyika kwa lengo la kuweka mikakati bora zaidi ya kuunda Baraza la Vijana. Washiriki walipendekeza ushirikishwaji zaidi wa wadau hasa kutoka vijijini na wilayani ufanyike kabla ya hatua zaidi za uundaji huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo yatakayotekelezwa mwaka 2008/2009 na Wizara yangu pamoja na kuendelea na shughuli za kawaida. Wizara itatekeleza shughuli zifuatazo:-

(a) Kwa kushirikiana na wadau wa masuala ya vijana na vijana wenyewe utaandaliwa mkakati wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana na kuusambaza kwa walengwa na wadau wote.

(b) Kukamilisha mchakato wa kisheria wa kuanzisha Baraza la Vijana Tanzania (BAVITA) kwa kushirikisha vijana, wadau hasa wa vijijini na Wilayani pamoja na wataalamu mbalimbali.

(c ) Kuimarisha vikundi vya vijana vya uzalishaji mali kwa kutoa mafunzo mbalimbali yanayohusu uanzishaji, usimamizi na uendeshaji wa shughuli za biashara na miradi kwa vijana wajasiriamali kupitia vituo vya vijana.

(d) Kuimarisha mfumo wa mawasiliano na upashanaji wa habari kwa vijana ikiwa ni pamoja na tovuti ya vijana Ilonga.

(e) Kuwajengea uwezo maofisa vijana na watumishi katika Idara na Vituo vya Vijana ili watoe huduma kwa ufanisi zaidi kwa njia ya mafunzo.

(f) Kujenga uwezo wa kusimamia utekelezaji wa kazi za vijana kwa kuwawezesha kushiriki katika mikutano mbalimbali ikiwa ni pamoja na mkutano wa Mawaziri wa Vijana na mkutano wa watendaji na washauri wa kazi za vijana katika nchi za Jumuiya ya Madola *(CYP),* Kamisheni ya Umoja wa Mataifa ya Maendeleo ya Jamii *(CSD),* Mtandao wa Ajira kwa Vijana Duniani *(YES),* makongamano ya siku ya UKIMWI duniani, siku ya Wanaojitolea Duniani na matukio mengine ya Kitaifa kama yatakavyojitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, usajili wa vyama vya wafanyakazi na waajiri. Katika kipindi cha mwaka 2007/2008 pamoja na kazi za kawaida za kuratibu na kushughulikia maombi ya usajili wa vyama vya wafanyakazi na waajiri, Wizara yangu kupitia Ofisi ya Msajili wa Vyama ilifanya yafuatayo:-

(a) Kuelimisha watendaji 130 wa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri juu ya Sheria Mpya za Kazi pamoja na majukumu yao kwa mujibu wa Sheria hizi.

(b) Kufanya kaguzi za kumbukumbu za wanachama 16 kwenye mikoa mitatu (Arusha, Kilimanjaro na Iringa). Katika zoezi hili ilibainika kuwa wapo waajiri wanaokataa kutambua uwepo wa Vyama vya Wafanyakazi katika sehemu zao za kazi na wafanyakazi walielekezwa namna ya kuchukua hatua za Kisheria wanapokumbana na vikwazo vya aina hiyo.

(c) Kutoa mafunzo kuhusu mwelekeo mpya wa Sheria za Kazi Na. 6 na Na. 7 za mwaka 2004 na elimu juu ya UKIMWI mahali pa kazi kwa njia ya semina kwa viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri pamoja na baadhi ya Watumishi wa Wizara wanaohusika na usimamizi wa Sheria za Kazi. Walionufaika ni watendaji 130 kutoka Mikoa ya Morogoro, Pwani, Dar es Salaam, Tanga, Kilimanjaro, Manyara na Arusha na walielimishwa kuhusu mwelekeo mpya wa Sheria za Kazi Na. 6 na Na. 7 za mwaka 2004 na elimu juu ya UKIMWI mahali pa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo yatakayotekelezwa katika mwaka 2008/2009, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri itaendelea kutekeleza majukumu hayo ya kawaida kwa lengo la kuongeza kiwango uwezo wa vyama vya waajiri na wafanyakazi kuzingatia sheria mpya za kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maendeleo ya watumishi. Katika mwaka 2007/2008 Wizara ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Kushirikisha sekta binafsi katika utoaji wa huduma za ofisi, kama vile ulinzi, huduma za usafi na matengenezo madogo madogo ya vifaa vya ofisi.

(b) Kuajiri watumishi wapya na kuboresha mazingira ya kazi. Jumla ya watumishi wapya 111 wameajiriwa, watumishi 58 wamepandishwa vyeo na wengine 15 wamethibitishwa kazini.

(c) Kuanzisha Kamati ya Maadili, Nidhamu na Kudhibiti Rushwa katika Utumishi wa Umma, ambayo imetoa mafunzo kwa watumishi 279 wa Wizara katika Mikoa ya Tabora, Singida, Rukwa, Mbeya, Iringa, Shinyanga, Kagera, Mwanza na Dodoma.

(d) Kuendeleza watumishi kielimu, kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu watumishi 19 na watumishi 359 ya muda mfupi. *(Makofi)*

(e) Kutoa mafunzo ya vita dhidi ya UKIMWI kwa watumishi wa Wizara.

(f) Ofisi za Kazi za Mikoa sita ya Mwanza, Morogoro, Kigoma, Ruvuma (Songea), Shinyanga na Dar es Salaam zimefanyiwa ukarabati na Ofisi ya Same (Kilimanjaro) imejengwa upya. Aidha, ukarabati unaendelea katika ofisi ya Tanga na baadhi ya majengo katika Kituo cha Maendeleo ya Vijana cha Ilonga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo yatakayotekelezwa katika mwaka 2008/2009 Wizara itaendelea kutekeleza majukumu ya kawaida kuhusu maendeleo ya watumishi. Aidha, itaendelea kuboresha kwa kuzifanyia ukarabati na kuzipatia vitendea kazi ofisi za kazi na vituo vya Vijana.

Kazi ya ukarabati kwenye vituo vya Tanga, Mtwara, Lindi, Tabora, Bukoba, Lushoto, Korogwe na Muheza na katika vituo vya Vijana vya Ilonga, Sasanda na Marangu utakamilishwa. Aidha, ukarabati wa Ofisi za Kazi za Mbeya, Rukwa, Iringa, Kilombero, Kilosa, Mara, Singida, Kilimanjaro (Moshi) na Dodoma utaanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, usalama na afya mahali pa kazi. Utekelezaji wa malengo katika kipindi cha mwaka 2007/2008 wakala wa Afya na Usalama Sehemu za Kazi *(OSHA)* ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

(a) Kufanya kaguzi 2,846 za kawaida *(general workplace inspections)* na kaguzi maalum 7,489 zilifanyika na kutoa ushauri wa kitaalamu pale panapobainika upungufu.

(b) Kuandaa Sera ya Taifa ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi nchini.

(c) Kukarabati majengo ya ofisi za Kanda ya Kaskazini (Arusha), Kanda ya Ziwa (Mwanza) na Pwani (Dar es Salaam), kutoa vitendea kazi na kuongeza wakaguzi.

(d) Kutoa mafunzo ya usalama na afya mahali pa kazi kwa kupitia vipindi mbalimbali vya televisheni na redio hasa wakati wa Wiki ya Afya na Usalama Duniani 2008 na kusambaza vipeperushi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo yatakayotekelezwa katika mwaka 2008/2009 Wakala wa *OSHA* utaendelea kutekeleza majukumu yake ya kawaida ikiwa ni pamoja na:-

(a) Kufanya kaguzi 3,500 za kawaida na kaguzi 3,950 maalumu na za kisheria za usalama na afya mahali pa kazi;

(b) Kuimarisha ofisi za Kanda ya Kusini (Mtwara) na Kati (Dodoma);

(c) Kuboresha mfumo wa kuripoti na kutoa taarifa za magonjwa na ajali zitokanazo na kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala Wa Huduma za Ajira Nchini *(TaESA).* Wakala wa Huduma za Ajira ni Wakala mpya ulioanzishwa hivi karibuni baada ya kuhuishwa kwa kitengo kilichokuwa kinasimamia vituo vya ara nchini. Wakala huu ulizinduliwa rasmi wakati wa Wiki ya Utumishi wa Umma mwezi Juni, 2008.

Kwa sasa Wakala unatoa huduma zake kupitia vituo viwili *(Labour Exchange Centres),* vilivyopo Dar es Salaam na Mwanza, vilivyokuwa chini ya Idara ya Ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, *TaESA* itaendelea kujiimarisha na kuratibu shughuli za vituo vya ajira na kuanza mchakato wa kuanzisha vituo vingine katika Mikoa ya Mbeya, Kilimanjaro na Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Shirika La Taifa La Hifadhi Ya Jamii *(NSSF).* Shirika la Hifadhi ya Jamii liliendelea na majukumu yake ya kuandikisha wanachama, kukusanya michango, kuwekeza kwenye miradi mbalimbali na kulipa mafao ya aina saba kwa wanachama. Mafao yatolewayo na *NSSF* kwa sasa ni mengi kuliko yanayotolewa na shirika lingine lolote la hifadhi ya jamii hapa nchini. Matokeo muhimu ni pamoja na:-

(a) Kukusanya mapato ya shilingi 286,366.4 ikilinganishwa na lengo la shilingi 292,936.7 na hii ni sawa na asilimia 97.7 ya lengo. (Kiambatisho Na.VIII)

(b) Kukamilisha ujenzi wa majengo ya ofisi na vitega uchumi katika Jiji la Mwanza *(Mwanza Commercial Complex)* na ujenzi wa Jengo la *Benjamini William Mkapa Pension Tower* Jijini Dar es Salaam.

(c) Kukamilisha ujenzi wa mabweni matano katika Chuo Kikuu cha Dodoma yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 5,000.

(d) Kukamilisha ujenzi wa nyumba 248 za Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ); aidha, ujenzi wa nyumba za Polisi Kurasini Dar es Salaam unaendelea.

(e) Kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Biashara *(Business Park)* cha wafanyabiashara ndogo ndogo vijana (wamachinga) katika Manispaa ya Ilala, chenye uwezo wa kuchukua wafanyabiashara 10,000. *(Makofi)*

(f) Kwa kushirikiana na *ILO* kufanya tathmini ya hali ya kifedha ya mfuko *(Actuarial valuation – 2007/2008),* ambapo matokeo yameonyesha kuwa hali ya kifedha ya mfuko ni nzuri na unaweza kujiendesha bila matatizo yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo kwa mwaka wa fedha 2008/2009, *NSSF* inatarajia kuendelea kutekeleza majukumu yake ya kawaida pamoja na kuimarisha ofisi

zake za mikoani kwa kuziunganisha na mtandao wa komputa, kuboresha uwekaji wa kumbukumba, kutoa elimu kuhusu mfumo mpya wa Hifadhi ya jamii kwa wanachama wake, waajiri na umma kwa ujumla. *(Makofi)*

Kwa upande wa uwekezaji shirika litaendelea kukamilisha miradi niliyoitaja hapo awali pamoja na ujenzi wa majengo ya ofisi na vitega uchumi katika Mkoa wa Kagera , Kigoma, Shinyanga, Arusha na ujenzi wa ofisi za Wilaya ya Mbozi, Kahama, Kidatu na Njombe. Aidha shirika litaanza ujenzi wa jengo la kibiashara na ofisi katika kiwanja kilichokuwa cha AISCO zamani, jengo la ubalozi wa Tanzania jijini Nairobi nchini Kenya, jengo la ofisi za *PCCB,* hoteli ya kisasa Mwanza na Hospitali ya Apollo Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu daraja la Kigamboni, Shirika litashiriki na kuratibu mradi wa ujenzi wa daraja hilo. Kama ambavyo Waziri Mkuu alivyoeleza kwenye hotuba yake, Serikali imekwishafanya maamuzi ya msingi kuhusu ujenzi wa Daraja hili chini ya uratibu wa *NSSF*. Aidha, *NSSF* imeanza mchakato wa kumpata mbia (mwekezaji binafsi) atakayeshiriki katika ujenzi huu kwa kutoa tangazo tarehe 17 Julai, 2008 kwenye vyombo vya habari kuomba wenye nia wajitokeze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Shirika La Taifa la Tija *(NIP).* Utekelezaji wa malengo ya mwaka 2007/2008 Shirika la Taifa la Tija lilitekeleza kazi muhimu zifuatazo:-

(a) Kuendesha mafunzo 80 kwa Watanzania 1300 (kulinganisha na lengo la 1200) kutoka sekta mbalimbali yanayolenga kuwapa mbinu za kisasa za kuboresha utendaji kazi katika sehemu zao za kazi. Kati ya wanufaika ni Waheshimiwa wabunge wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii. *(Makofi)*

(b) Kutoa huduma ya uelekezi kwa wateja 32 kutoka taasisi za umma na binafsi. Hii ni sawa na asilimia 91.42 ya lengo lililopangwa.

(c) Kufanya tafiti nne kati ya nane zilizopangwa. Aidha, lilifanya utafiti wa mishahara kwa Wahandisi *(Tanzania Remuneration Survey for Engineers 2007)* na kuendelea na matayarisho ya mpango wa Taifa wa usimamizi wa tija *(National Productivity and Competitiveness Improvement Programme).*

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo yatakayotekelezwa mwaka 2008/2009. Kwa mwaka 2008/2009 Shirika litaendelea kutekeleza majukumu yake ya kawaida, pamoja na kuendesha mafunzo maalumu ya uchumi kwa kushirikiana na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya jinsi ya kujiandaa na maisha baada ya kustaafu kazi kwa wafanyakazi wa umma, taasisi mbali mbali na makampuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Usuluhishi Na Uamuzi *(CMA).* Jukumu kubwa la Tume hii ni ya Usuluhishi na Uamuzi *(Mediation and Arbitration)* wa migogoro sehemu za kazi. Tume hii iliyozinduliwa mwezi Mei, 2007 ilianza kazi zake kwa kutumia Fungu 65 la Wizara yangu na ilifanikiwa kufanya yafuatayo:-

(a) Kusuluhisha migogoro 5,214 kati ya 6,065 ilipokelewa sawa na 86%.

(b) Iliendesha mafunzo na mikutano ya kazi kuhusu uelewa wa sheria za kazi kuhusu namna ya kutumia sheria mpya za kazi.

(c) Kusimamia uundaji wa Mabaraza 10 ya Wafanyakazi sehemu za kazi *(Workers Councils)* na kuendesha semina 10 za kuyaimarisha.

(d) Kuajiri watumishi wapya 71 katika nyanja mbalimbali ili kuimarisha utendaji wa Tume.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo yatakayotekelezwa katika mwaka wa fedha wa 2008/2009, Tume itaendelea kujiimarisha kwa kuajiri watumishi wengi zaidi, kuwapatia mafunzo na vitendea kazi pamoja na kufanya kazi zake za msingi za usuluhishi na uamuzi wa migogoro wa kazi, na kutoa ushauri kwa walengwa kuhusu uzuiaji wa migogoro sehemu za kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *s*hukrani, majukumu yote niliyoyaeleza yametekelezwa kwa ushirikiano na mshikamano wa hali ya juu wa viongozi na wafanyakazi wote wa Wizara yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitumie nafasi hii kuwashukuru viongozi na wafanyakazi wote wa Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana pamoja na Mashirika na Taasisi zake kwa juhudi zao kubwa walizoonyesha katika kutekeleza majukumu tuliyopewa na Taifa. Shukrani zangu za kipekee nazielekeza kwa Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, Naibu Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa msaada na ushauri wake wa karibu. *(Makofi)*

Aidha, napenda pia nitoe shukrani zangu za dhati kwa Katibu Mkuu wa Wizara yangu Dr. Ladislaus Komba na Naibu Katibu Mkuu Bibi Edine Mangesho, pia kwa Wakuu wa Idara na Watumishi wote wa Wizara yangu, Watendaji Wakuu wa Mashirika na Taasisi zilizopo chini ya Wizara na Bodi zao ambao wameshirikiana na Wizara yangu katika kutekeleza majukumu tuliyopangiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nitumie fursa hii kuwashukuru washirika wetu wote ambao kwa namna mbalimbali wemetuunga mkono katika utekelezaji wa majukumu yetu. Kwa njia ya pekee naomba niwashukuru wajumbe wa Baraza la Ushauri wa Masuala ya Kazi Uchumi na Jamii *(Labour, Economic and Social Council (LESCO),* Chama cha Waajiri Tanzania *(ATE)* na Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi Tanzania *(TUCTA)* kwa michango na ushauri wao mzuri walionipatia katika kutekeleza majukumu na malengo ya Wizara yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inatambua na itaendelea kuthamini michango mbalimbali ya wahisani ambayo inasaidia kwa kiwango kikubwa kutekeleza majukumu yake. Kwa uchache naomba shukrani za dhati ziende kwa Serikali ya nchi na Mashirika ya Kimataifa ya Denmark, Marekani, *World Bank, ILO, UNDP, UNICEF, UNFPA, CYP* na *FHI.* Naishukuru pia *TACAIDS* kwa misaada mbalimbali kwa Wizara

yangu na Idara mbalimbali za Serikali na Taasisi zisizo za Kiserikali ambazo tumeshirikiana nazo vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nichukue fursa hii kuwashukuru sana wananchi wa jimbo langu la Urambo Mashariki kwa ushirikiano wao wanaoendelea kunipatia ambao umeniwezesha kutekeleza majukumu niliyokabidhiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, makadirio ya Bajeti ya Wizara. Ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu kwa mwaka 2008/2009, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 12,726,924,500/= kwa Fungu 65. Kati ya fedha hizo shilingi 6,512,606,000/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, ambapo shilingi 1,257,328,000/= ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 5,257,278,000/= ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kiasi cha shilingi 6,212,318,500/= ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo ambapo shilingi 2,178,845,000/= ni fedha za hapa nchini na shilingi 4,033,473,500/= ni fedha za nje. *(Makofi)*

Vile vile naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe kiasi cha shilingi 1,445,351,000/= chini ya Fungu 15 kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya Tume ya Usuluhishi na Uamuzi *(CMA),* ambapo shilingi 445,351,000/= ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 1,000,000,000/= ni kwa matumizi mengineyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru wewe binafsi, Naibu Spika, na Wenyeviti wa Bunge letu, kwa kuendesha shughuli za Bunge kwa viwango stahiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA – MWENYEKITI WA KAMATI YA YA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la mwaka 2007, nachukua nafasi hii kukushukuru wewe kwa kuniruhusu kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa mwaka wa fedha 2007/2008 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, majukumu ya Kamati hii pamoja na mambo mengine inafanyakazi ya kuchambua Bajeti ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. Tarehe 30 Mei, 2008, Mjini Dar es Salaam, Kamati ilifanya kikao na Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana.

Katika kikao hicho tulipata maelezo kuhusu Bajeti ya Wizara toka kwa Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, Katibu Mkuu na Wataalam wa Wizara. *(Makofi)*

Timu hiyo ilieleza kwa kina kuhusu dira, dhima, majukumu ya Wizara na utekelezaji wa maagizo ya Kamati kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2007/2008.

Aidha, tarehe 25 Juni, 2008, Mjini Dodoma Kamati ilifanya kikao mara ya pili na Wizara kupata maelezo zaidi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kuhusu utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo, Mapato na Matumizi kwa mwaka 2007/2008 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha na kazi zilizopangwa kufanywa kwa mwaka wa fedha 2008/2009. *(Makofi)*

Aidha, Wajumbe wa Kamati walijulishwa kwamba Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, yuko nchini India kwa ajili ya matibabu, Wajumbe wanamtakia kila la kheri na apone haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kutoa maoni na ushauri wa Kamati, napenda kwanza kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kumteua Mheshimiwa Al-shymaa Kwegyir, kuwa Mbunge wa Kuteuliwa na Mheshimiwa Mchungaji Dr. Getrude Rwakatare, kuwa Mbunge wa Viti Maalum, Wabunge wote hawa baada ya kuwa Wabunge, Mheshimiwa Spika aliwateuwa moja kwa moja kujiunga na Kamati ya Maendeleo ya Jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa kuwatambulisha Wajumbe wanaounda Kamati hii ya Maendeleo ya Jamii kama ifuatavyo, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti; Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Fatma Othman Ali, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Capt. John Komba, Mheshimiwa Florence Kyendesya, Mheshimiwa Dorah Mushi, Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji, Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfan, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika na Mheshimiwa Anna Lupembe. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Mchungaji Dr. Gertrude Rwakatare, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa Kiumbwa Makame Mbaraka, Mheshimiwa Elietta Switi, Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Mwajuma Hassan Khamis, Mheshimiwa Sameer Ismail Lotto, Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mheshimiwa Al-Shaymaa Kwegyir, Mheshimiwa Bujiku Sakila na Mheshimiwa Mohamed Ali Said. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha uliopita Kamati yangu ilitoa maoni na maagizo katika maeneo mbalimbali kama ifuatavyo, Kamati ilishauri Wizara kushughulikia mgogoro wa wafanyakazi katika kiwanda cha Sukari cha *TPC,* Mkoani Kilimanjaro; Serikali kupitia upya utaratibu uliotumika wa kumilikisha kiwanja 906/H cha Shirika la Tija ya Taifa *(NIP)* kwa Chuo cha *IMTU;* Serikali iharakishe kuandaa sera ya Shirika la Tija la Taifa *(NIP);* Serikali iangalie upya utaratibu wa kukata fedha za *other charges* (*OC*) za Halmashauri ambazo hazijarejesha mikopo ya Mfuko wa Vijana; Serikali iangalie upya uwezekano wa fedha za mikopo ya vijana kupitia katika *SACCOS*; Serikali iendeshe mafunzo kwa wamachinga kuhusiana na uendeshaji wa biashara kabla

ya Shirika la Hifadhi ya Jamii ya Taifa *(NSSF)* hawajakabidhi Jengo wanalojenga Mjini Dar es Salaam, Mtaa wa Karume; zoezi la kutambua vijiwe vya vijana liendelee na Serikali ianzishe ofisi katika kila wilaya ili iweze kuwaunganisha kimafunzo na mchakato wa kisheria wa kuanzisha Baraza la Vijana Tanzania (BAVITA) uharakishwe na mkakati wa kuanzisha baraza hilo uletwe katika Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Wizara iweke mikakati ya utoaji wa vibali vya ajira kwa wageni na kupunguza malalamiko kutoka kwa wananchi kuhusu utoaji wa vibali holela na ucheleweshwaji wa kutoa vibali hivyo; Serikali ione uwezekano wa fedha za Mfuko wa Uwezeshaji wa Wananchi (Mfuko wa JK) kwenda moja kwa moja katika *SACCOS* ili ziwafikie wananchi wengi zaidi na kurahisisha ufuatiliaji wa mkopo huo; Serikali itimize ahadi yake na iongeze kasi na ione umuhimu wa kujenga Daraja la Kigamboni na Msimamizi Mkuu wa Ujenzi huo awe Shirika la Hifadhi ya Taifa ya Jamii *(NSSF);* Shirika la Hifadhi ya Taifa ya Jamii *(NSSF)* iangalie uwezekano wa kujenga majengo mengine ya biashara kwa wamachinga, kama linalojengwa Dar es Salaam wajenge mahala pengine kama Mwanza na Arusha na kwa kuwa Wizara ilipata hati ya mashaka mwaka 2005/2006, Wizara iweke mikakati ili wasipate hati ya mashaka tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara kwa kiasi kikubwa imeyafanyia kazi baadhi ya maeneo husika na hatua za utekelezaji zimeonekana. Hata hivyo, katika maeneo ambayo Kamati imeona juhudi zaidi zinahitajika itaendelea kushauri ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2007/2008 Wizara iliidhinishiwa na Bunge matumizi ya shilingi bilioni 10.9. Waziri alielezea Kamati kwa undani kuhusu matumizi katika kutekeleza Bajeti ya mwaka 2007/2008.

Baadhi ya shughuli zilizotekelezwa na mafanikio yake ni kama ifuatavyo, ili kuondoa matatizo katika mishahara Bodi za Mishahara katika Sekta nane zilizinduliwa rasmi tarehe 18 Aprili, 2007 zimeanza kufanyakazi.

Bodi hizo ni Bodi ya Sekta ya Kilimo, Madini, Afya, Viwanda na Biashara, Ulinzi katika Makampuni Binafsi, Huduma za Usafiri na Mawasiliano, Huduma za Usafiri Majini na Huduma za Wafanyakazi wa Majumbani na Mahotelini, kukamilisha ukarabati wa Ofisi ya Kazi ya Dar es Salaam na Mwanza, Wizara imefanikiwa kuwashirikisha wadau na jamii kwa ujumla katika kupambana na Ajira mbaya ya Mtoto na baadhi ya watoto kuingizwa katika elimu za msingi na ufundi na Wizara imefanya kaguzi za kazi 893 katika sekta binafsi.

Pia kituo cha Ajira cha Dar es Salaam kinaendelea kuwaunganisha watafuta kazi na waajiri, rasimu ya Muswada wa Sheria ya Huduma na Kukuza Ajira imekamilika tayari kwa kupitishwa katika vyombo vya Maamuzi Serikalini, Wizara iliendelea kuratibu ukamilishaji wa marejeo ya Sheria ya Kazi Awamu ya Pili, Sheria ya Hifadhi ya Jamii na Sheria ya Ajira ambazo zimepitishwa na Baraza la Mawaziri, Sheria za *Occupational Health and Safety Act, Workman's Compesation and National Employment Service Act* zipo kwenye hatua za kukamilishwa, Serikali inaendelea kuandaa Mkakati wa

Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2007 na kwa kushirikiana na *UNFPA,* Wizara imeandaa mwongozo wa stadi za maisha ambao utatumika kuwafundishia vijana na wadau wote wanaojishughulisha na utoaji wa elimu hiyo na kazi zingine mbalimbali zimefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio, Waziri na watalaam walielezea changamoto zilizojitokeza katika kutekeleza Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2007/2008, changamoto hizo ni pamoja na namna ya kuhakikisha kuwa huduma za Hifadhi ya Jamii kwa kuzingatia Sera na Sheria ya Hifadhi ya Jamii na namna ya kuwafikia walengwa katika ngazi zote hadi vijijini, kukabiliana na tatizo la UKIMWI sehemu za kazi ili kupunguza au kuokoa kupotea kwa nguvu kazi za Taifa, uwezo mdogo uliopo wa kuweza kuwafikia vijana wote mijini na vijijini ili kuwahamasisha na kuwajengea uwezo wa kujiajiri, kuhakikisha kuwa mikopo ya wajasiriamali inawafikia walengwa kwa wakati hasa vijijini na upatikanaji wa takwimu sahihi za ajira mpya zinazozalishwa kote nchini hasa katika sekta binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake katika mwaka 2008/2009 imeomba kiasi cha shilingi 14,172,275,500/= kimeombwa, baada ya kupata taarifa na maelezo ya kina ya malengo na kazi zilizopangwa kufanywa kwa mwaka wa fedha 2008/2009, Kamati ilijadili kwa undani masuala mbalimbali na kuipitisha Bajeti ya Wizara. Kamati yangu inaunga mkono maombi ya Wizara hii hata hivyo Kamati ilitoa maoni na ushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kuhusu kuibuka kwa migogoro hapa nchini hasa baada ya Serikali kutangaza mishahara mipya katika viwanda. Kwa kuwa Serikali ilitangaza mishahara mipya katika viwanda vyetu baada ya kuundwa kwa Bodi za Kisekta na kwa kuwa Serikali imekuwa mara nyingi ikibadilisha katika kuweka kima cha chini katika viwanda kwa sababu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri kama ifuatavyo, wataalam wa Wizara na wa Bodi za Mishahara za Kisekta walifanyie utafiti wa kina suala la kima cha chini cha mshahara ili Serikali isiwe inabadilisha mara kwa mara na kutangaza kima kipya cha mshahara, kwa kuwa katika viwanda vingi hapa nchini hakuna mikataba ya ajira kwa wafanyakazi yenye kumnufaisha mfanyakazi wa kiwanda, Serikali iangalie upya na kuliwekea kipaumbele suala hili katika kuwaongoza waajiri na waajiriwa kutayarisha mikataba ya ajira yenye manufaa ili kupunguza migogoro sehemu za kazi.

Kwa kuwa vyama vya wafanyakazi ni watetezi wakubwa wa wafanyakazi, uongozi wa wafanyakazi uweke mikakati ya kuwaelimisha wafanyakazi sheria zinazozuia migomo au masuala yapi yakitokea wafanyakazi wanahitaji kugoma na yapi yanatakiwa kupelekwa mahakamani na maeneo gani yanahitajika kuwa na mazungumzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ni kuhusu migogoro na utendaji kazi wa Kampuni ya Reli Tanzania. Kwa kuwa kumekuwa na malalamiko mengi sana kuhusu utendaji kazi wa Kampuni ya Reli Tanzania hasa katika suala zima linalohusu wafanyakazi, hali

ambayo inaweza kuleta mgomo na kusababisha hasara kubwa kwa Taifa. Kamati inatoa ushauri kama ifuatavyo, Wizara itoe taarifa za mara kwa mara kuhusu malalamiko ya wafanyakazi na kuyafanyia kazi ili kuepusha migogoro, Serikali isisite kutoa maamuzi ya haki iwapo mwekezaji atabainika wazi kwamba ni dhaifu katika kuboresha maslahi na haki za wafanyakazi kwa mujibu wa taratibu na sheria na Kamati inaiomba Serikali izingatie na kutekeleza makubaliano yaliyopo katika mkataba ambao mwekezaji ameuweka na Shirika la Reli ili kuepusha migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu ni kuhusu mgogoro katika kumilikisha Kiwanja cha Shirika la Taifa la Tija *(NIP)* kwa Chuo cha *IMTU*. Kwa kuwa tatizo la umiliki wa kiwanja cha *NIP* limekuwa ni la muda mrefu na kwa kuwa Kamati iliiomba Serikali kupitia upya utaratibu uliotumika wa kumilikisha kiwanja Na. 906/H cha *NIP* kwa Chuo cha *IMTU*, kwani inaonekana wazi katika mchakato mzima wa kumiliki kiwanja hiki kuwa haki haikutendeka, kwa hiyo, Kamati inashauri yafuatayo, kwa kuwa Kamati haikuridhika kabisa na mawasiliano yanaendelea kufanywa na Serikali ya kuwalipa *NIP* shilingi milioni 11 kama salio lililobaki, ukilinganisha na tathimini iliyofanywa siku za nyuma ilionyesha kwamba fidia ingekuwa ni zaidi ya shilingi milioni 200, Kamati inashauri kwamba Serikali ifanye tathmini upya kujua ni kiasi gani Shirika la Taifa la Tija *(NIP)* inapaswa kulipwa? Kama hiyo haiwezekani basi miliki ya kiwanja irudishwe kwa *NIP*. *(Makofi)*

Kwa kuwa inasemekana kwamba *NIP* ilinyang'anywa miliki ya kiwanja hicho baada ya kutoendeleza kwa takriban miaka mitatu, Chuo cha *IMTU* nacho itabidi miliki yake iondolewe kwa sababu hakijaendeleza zaidi ya miaka mitatu, lakini Kamati inashangaa bado *IMTU* wameendelea kumiliki kiwanja hicho na hawajamaliza kulipa fidia kwa *NIP*. Kamati inashangazwa na mambo haya yote na inaomba Wizara ichukue hatua ili kutenda haki na kukuza shirika la *NIP* kwa sababu ni Shirika la Tija kubwa katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali iangalie upya utaratibu wa kutatua tatizo hili na itoe taarifa kwenye Kamati haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu fedha za Mfuko wa Vijana kupelekwa katika *SACCOS*. Kwa kuwa fedha za Mfuko wa Vijana ni muhimu sana katika kuwaendeleza vijana. Kamati bado inaamini kwamba utaratibu uliopo wa Wizara kupeleka fedha katika Halmashauri zetu ili kutoa fedha za vijana kwenye vikundi bado hauna ufanisi mkubwa, Kamati inashauri kama ifuatavyo, Serikali ione umuhimu wa kuongeza fedha hizo na kuzipeleka moja kwa moja katika *SACCOS* za vijana zinazotambulika. Hii itarahisisha ufuatiliaji wa fedha hizo na kuleta manufaa kwa vijana kwa sababu Mfuko huo utaendelea kujizungusha na kujizalisha zaidi. Pia Kamati haioni umuhimu wa kuwakata Halmashauri zetu fedha za *OC* kama hazijarejesha fedha za kukopesha vijana kwani kufanya hivyo ni kuwaumiza wananchi, hatua kali zichukuliwe kwa watendaji waliohusika na sio kukata fedha za *OC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, karibu miaka miwili sasa imepita toka fedha za uwezeshaji wa wananchi (Mfuko wa JK) zianze kutolewa hapa nchini. Kamati inawaza

siku zote kwamba, benki haijawa rafiki wa maskini hasa katika kutoa mikopo ni vyema kutumia *SACCOS*. Tunampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake Ukurasa wa 16 - 17, anaunga mkono kwamba fedha za uwezeshaji wa wananchi sasa zipelekwe moja kwa moja kwenye *SACCOS* na Asasi za Kifedha zingine na suala la kupitishia benki fedha hizo liangaliwe upya na Kamati inashauri kama ifuatavyo, Serikali iandae Waraka ili fedha za uwezeshaji wa wananchi kiuchumi zipelekwe kwenye *SACCOS* na asasi za fedha zinazotambulika, Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana waandae utaratibu wa kufuatilia utekelezaji wa fedha hizo ili fedha ziweze kukopeshwa na kurejeshwa na kuendelea kukopesha zaidi na Serikali iweke mikakati ili fedha hizo ziweze kuwafikia walengwa. Wizara ipewe uwezo wa kufuatilia katika mabenki kujua kama fedha hizo zimekopeshwa kwa walengwa na ikiwezekana hata Waheshimiwa Wabunge wawezeshwe kupata taarifa hizo kila mara wanapozihitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wananchi wengi sana walijitokeza kuomba mikopo ikilinganishwa na kiasi kidogo cha fedha kilichotengwa, Serikali iangalie namna ya kupata fedha za kutosha kwa lengo la kuwafikia wananchi wengi iwezekanavyo na kwa kuwa wananchi wengi hawana elimu ya ujasiriamali inayowawezesha kubuni na kuandaa miradi mizuri na kupanga matumizi bora ya mikopo waliyokopeshwa na urejeshaji wake, Serikali iweke mikakati ya kuwaelimisha wananchi kuhusu ujasiriamali na kwa kuwa marejesho ni muhimu sana katika kuendeleza Mfuko wa JK, Serikali iweke mikakati ya kutoa taarifa ya marejesho ya mikopo ya mfuko wa uwezeshaji wa wananchi kiuchumi, mafanikio na changamoto ili kama kuna kasoro mbalimbali ziweze kurekebishwa mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa suala la ujenzi wa daraja la Kigamboni limekuwa ni suala la muda mrefu bila kutekelezwa na kumekuwa na majibu mbalimbali likiwemo la ujenzi wa Daraja hili lipo kwenye mchakato wa kuidhinishwa na Serikali ambapo Waraka wa Baraza la Mawaziri umeandaliwa. Waraka ambao unataka *NSSF* ishirikiane na mbia wa sekta binafsi kujenga daraja hilo.

Aidha, tumepewa taarifa kwamba Waraka huu umepitishwa na Kamati ya Makatibu Wakuu *(IMTC)* na sasa upo tayari kuwasilishwa kwenye Baraza la Mawaziri na kibali kimeshatolewa ili *NSSF* itangazwe na kumpata mbia, Kamati inashauri kwamba Serikali iharakishe mchakato huu ili kazi ya ujenzi wa daraja hili uweze kuanza mapema iwezekanavyo kabla ya mwaka 2010 kwa kuwa utaleta tija kwa wananchi wa Dar es Salaam hususan wakazi wa Kigamboni na kuleta maendeleo katika nchi yetu ya Tanzania kwa ujumla, Serikali iweke muda wa kuanza kazi ya ujenzi wa daraja hili *(timeframe)* badala ya kuendelea kusema kwamba Serikali ipo kwenye mchakato. Utafutaji wa mbia uharakishwe ili kazi ya ujenzi ianze mara moja, mara kazi ya ujenzi wa daraja utakapoanza Serikali iweke mikakati ya kukabiliana na changamoto ili kazi ya ujenzi iweze kuwa na manufaa kwa Taifa, ili mradi uweze kuwa na manufaa kwa taifa Serikali iweke mikakati ya kujenga barabara za kuunganisha daraja la Kigamboni na mji wa Dar-es Salaam na Serikali itenge fedha kwa ajili ya kulipia fidia kwa wananchi katika maeneo ambapo mradi utapita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mafunzo ya ujasiriamali kwa wamachinga kabla ya kukabidhiwa jengo la kufanyia kazi. Kwa kuwa tatizo kubwa la wajasiriamali wetu hapa nchini hasa wamachinga ni kutokuwa na elimu ya ujasiriamali inayowawezesha kubuni na kuandaa miradi mizuri inayokopesheka, kuiendesha miradi kwa ufanisi pamoja na kupanga matumizi bora ya mikopo waliyokopeshwa na urejeshaji wake, Kamati inashauri kama ifuatavyo, Wizara iandae mitaala maalum katika zoezi la kuwafundisha wamachinga na kupata orodha yao wanaohitaji mafunzo ili waweze kufundishwa kabla ya kukabidhiwa mahali pa kufanyia kazi, Serikali kwa kushirikiana na taasisi zingine ziandae mpango mzima wa mafunzo kwa wamachinga, nataarifa ya mpango huo uwasilishwe katika Kamati na Shirika la Hifadhi ya Taifa ya Jamii *(NSSF)* iendelee na mikakati ya kujenga majengo ya wamachinga katika miji ya Mwanza na Arusha na miji mingine hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa Serikali wa kuibua ajira mpya milioni moja ifikapo mwaka 2010. Kwa kuwa Rais wetu alitamka katika Ilani ya Uchaguzi kwamba ataongeza ajira milioni moja ifikapo mwaka 2010. Kwa takwimu tulizonazo hadi sasa ajira mpya ni 475,000 hii haijafikia hata nusu ya ajira mpya zilizoahidiwa. Kamati inashauri kama ifuatavyo, Serikali iweke wazi changamoto zote zinazosababisha kutofikia lengo hilo na namna ya kukabiliana na changamoto hizo. Kwa kuwa sekta binafsi inaweza kutoa mchango mkubwa sana katika kupata ajira mpya. Kamati inaishauri Serikali kuliangalia eneo hili kwa makini. Kwa kuwa zoezi la kutambua vijiwe vya vijana na kuwawezesha kiuchumi kwa kuwasaidia fursa mbalimbali ni muhimu sana katika kupunguza watu wasio na kazi. Kamati inaishauri Wizara kuendelea na zoezi hili kwa ufanisi mkubwa na kuwatengenezea mikakati ya ajira ili kufikia lengo la Mheshimiwa Rais la kuongeza ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kuna nchi mbalimbali ambazo zimepiga hatua kubwa katika kuongeza ajira mfano nchi ya Ghana, Serikali lazima iweke mikakati ya kwenda kujifunza katika nchi hizo ili uzoefu huo uweze kutumika katika nchi yetu. Kwa kuwa suala la kuongeza ajira milioni moja sio tu suala la Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, hivyo Serikali lazima iweke mikakati kwa Wizara zote na hasa Serikali za Mitaa kuibua ajira mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wanakamati wenzangu naomba kukushukuru wewe binafsi, kwanza kwa kunipatia nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati yangu na pia niwashukuru Wenyeviti wa Bunge kwa shughuli wanazozifanya za kumsaidia Mheshimiwa Spika na wewe katika kufanya kazi ya kusimamia shughuli za Bunge za kuchambua Bajeti mbalimbali. Lakini nakushukuru wewe binafsi kwa kuwa umeanza kuisimamia hotuba hii ya Bajeti ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa ufanisi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee naomba nimshukuru Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mbunge wa Koani ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii, kwani mara zote amekuwa akinisaidia sana kusimamia na kusaidiana na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati kuendesha shughuli za Kamati ya Maendeleo ya Jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati hii kwa michango yao katika kuboresha mijadala mbalimbali na maoni na mapendekezo ya Kamati. Napenda kumshukuru Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, Mheshimiwa Dr. Makongoro Mahanga, Naibu Waziri na Katibu Mkuu Dr. Komba na watumishi wote wa Wizara na Mashirika yaliyo chini ya Wizara hii kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia katika kipindi chote tunachofanya kazi za Kamati na hasa katika kuchambua Bajeti ya Wizara yetu. Kamati inawashukuru sana na kuwatakia mafanikio makubwa zaidi katika kazi za ujenzi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Ndugu Lawrence Robert Makigi na Ndugu Brown Mwangoka ambao ni Makatibu wa Kamati yetu, wamekuwa vijana watiifu, wameisaidia Kamati yangu na hasa mimi kuhakikisha shughuli za Kamati zinafanyika vizuri na kuweza kufikia ufanisi unaotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu, naomba nimshukuru sana mume wangu mpenzi Leonard Mhagama kwa kuwa amekuwa akinipa moyo sana wa kufanya kazi hizi za kisiasa na mara nyingi ninapokuwa katika majukumu yangu ya kisiasa yeye amekuwa akishughulika na mambo mengine mengi, kwa kweli ananisaidia sana. Namwombea afya njema na Mungu aendelee kumpa baraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru watoto wangu wapenzi. Vile vile naomba kwa namna ya pekee niwashukuru sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Peramiho. Wapiga kura wangu pia wamekuwa pamoja nami katika shughuli mbalimbali na wamekuwa wakinipa moyo na kunisaidia sana katika majukumu yangu ya kisiasa ambayo nimekuwa nikiyatumikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima naomba niwashukuru sana Waheshimiwa wabunge wote kwa kunisikiliza**.** *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusoma hotuba hii naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. SALIM ABDALLAH KHALFAN – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa majaliwa yake ya uzima wetu sote. Naomba kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, kuwasilisha maoni juu ya hotuba ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 99(7) toleo la 2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru wananchi wa Jimbo langu la Tumbe kwa kuendelea kuniunga mkono na kunipa hoja nyingi za kuleta mbele ya Bunge hili Tukufu. Aidha, naomba kutoa shukurani zangu za dhati kwa Kiongozi wetu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Naibu wake Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa na Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani kwa ushirikiano wao mkubwa

walionipa hadi kuniwezesha kusimama mbele yenu kuwasilisha hotuba ya Kambi ya Upinzani, kutokana na hoja iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wa Upinzani na Wabunge wote kwa ujumla wao, wana wajibu wa kushirikiana katika kuwatumikia Watanzania kwa lengo kuu la kuwaondolea Umaskini uliokithiri, maradhi na ujinga pamoja na kujenga Utaifa wetu wa dhati. Mwenyezi Mungu aziweke pamoja nia zetu na kuzibariki katika kutekeleza azma hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru wewe na Mheshimiwa Spika kwa kuliongoza Bunge letu kwa umahiri na hekima kubwa inayofanya shughuli za Bunge kwenda kwa utulivu na maelewano. Aidha, niwapongeze Wenyeviti wetu kwa kufuata vyema nyayo zenu katika kuliongoza Bunge letu kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuwa na mfumo wa sheria ya kazi na usuluhishi wa migogoro ya kazi ni sehemu muhimu sana ya soko la ajira, ulinzi wa haki za wafanyakazi na kuongeza tija. Baada ya kuona kuwa sheria za kazi za zamani hazikidhi mahitaji ya soko la ajira kwa sasa, Bunge lako Tukufu lilipitisha sheria mpya za kazi, namba 6 na 7 za mwaka 2004. Kutungwa kwa sheria mpya kulitarajiwa kuboreshe maslahi ya wafanyakazi na kuweka uwiano mzuri baina ya wafanyakazi na waajiri. Mojawapo ya sababu zilizocheleweshа utekelezaji wa sheria hizi ni kusubiri kanuni na miongozo yake. Hatua za kutengeneza miongozo *(Regulations)* zitakazopelekea kuanza kutumika kwa sheria hiyo zimefikia pazuri na sasa tunazo Kanuni za Mahakama ya Kazi ambazo zimechapishwa tarehe 18 Mei, 2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa kwa sasa ni kuwa na wataalam wa kutosha kuendesha shughuli za mahakama hii kwa ufanisi na kwa haraka. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuweka utaratibu wa kuwapa mafunzo watendaji kuhusu utatuzi wa migogoro inayohusiana na ajira kwa ujumla wake. Kwa maana kuwa pale wasuluhishi wanapomaliza kazi yao lakini upande wa mwajiri ukakataa kukubalina na maamuzi ya usuluhishi, hivyo basi tunapendekeza hatua kali za ziada zitumiwe dhidi ya wale wanaokataa kutekeleza maamuzi yaliyofikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mahusiano mema baina ya wadau wakuu wa ajira yaani Serikali, waajiri na waajiriwa (kupitia vyama vya wafanyakazi) ni hitaji muhimu katika kuchochea maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Uzalishaji makini na wa tija hutegemea sana uhusiano huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uhuru halisi wa Vyama vya Wafanyakazi ni nguzo muhimu siyo tu ya utawala bora, ila pia ni mhimili wa demokrasia iliyo ya kweli. Kauli na sauti ya wafanyakazi huwa ni kauli ya wazalishaji, ambayo pia ni kauli na sauti ya walipa kodi. Vyama vya wafanyakazi vilivyo huru na makini ni sehemu ya jamii huru ya kiraia au *civil society.* Watendaji Serikalini na katika sekta binafsi ni lazima waijue kwa kina dhana nzima ya vyama vya wafanyakazi *(trade unionism),* ndani ya ukweli na mazingira ya soko huria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, demokrasia ya kweli katika nchi yoyote ile duniani inaanzia kwa wafanyakazi kuwa na vyama vyao vilivyokuwa huru na vinavyoweza kudai maslahi yao ya msingi. Hivyo muendelezo huo wa uhuru wa vyama vya wafanyakazi huleta demokrasia ya kweli kwa nchi. Ili kufikia muafaka wa kiasi gani mwajiri anatakiwa kumpa mwajiriwa, majadiliano baina ya chama cha wafanyakazi na mwajiri wa sehemu husika ni muhimu sana. Kambi ya Upinzani inaipongeza Serikali kwa kuliona hilo na kuanza kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tofauti na hilo ni kumlazimisha mwajiri kufanya *down sizing* ambapo mtu mmoja hulazimika kufanya kazi iliyokuwa ikifanywa na watu watano kwa msaada wa mashine. Hii inachangia kuzidisha tatizo la ajira.

Mheshimiwa Spika, wakala wa usalama na afya mahala pa kazi *(OSHA).* Hiki ni kitengo muhimu sana, hasa linapokuja suala la mustakabali wa afya za wafanyakazi sehemu za kazi. Pamoja na kuanzishwa kwa Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (*OSHA*), bado haijawa na meno na nguvu ya kusimamia kwa ukamilifu sheria ya Bunge iliyoanzisha *OSHA.*

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya umuhimu wa kitengo hiki kimekuwa kinafanyakazi kwa kasi isiyoridhisha. Kambi ya Upinzani kwa mara nyingine tena inaitaka Serikali kutoa taarifa kuhusiana na utendaji kazi wa Kitengo husika na mipango yake katika kuhakikisha kwamba usalama na afya sehemu za kazi unazingatiwa na mikakati ya Wizara kuhakikisha kwamba fidia kwa wafanyakazi wanaopata ajali wakiwa sehemu za kazi zinaongezwa ikizingatiwa kwamba zilizokuwepo sasa ni ndogo mno na zimepitwa na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunaitaka Serikali kutoa taarifa hizo kwa msingi kuwa sehemu nyingi za kazi kama vile za ujenzi, migodini, mashambani na kwenye viwanda bado wafanyakazi wanapata ajali mbalimbali na waajiri wao wanakataa kuwalipa haki zao za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inazidi kusisitiza kwamba Wakala hawa wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi (*OSHA*) wawezeshwe zaidi ili waweze kufanya kazi zao vizuri na kwa ufanisi mkubwa na pia waweze kuyafikia maeneo tofauti ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Tija la Taifa *(NIP)* ni muhimu kwa Taifa letu kutokana na shughuli zake zinazolenga kuongeza tija katika utendaji na ufanisi wa mashirika na makampuni mengi nchini japokuwa lina rasilimali watu ndogo sana. Taarifa zilizopo zinaonyesha kuwa shirika hilo linaidai Serikali shilingi milioni 213. Katika fedha hizo shilingi milioni 49 walizitumia kuendeleza kiwanja chao namba 906/H *Mbezi Beach* ambacho baadaye walinyang'anywa na Serikali katika mazingira ya kutatanisha kwa madai kuwa shirika limeshindwa kutimiza masharti ya kukamilisha ujenzi kwa kipindi cha miaka mitatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba Serikali ilitoa fedha za kujenga nyumba moja katika mwaka wa fedha wa 1994/1995 na Serikali ilikuwa iendelee kutoa fedha nyingine lakini miradi ya maendeleo ilisimama kutokana na hali ngumu ya fedha katika mwaka huo. Hata hivyo, wakati ujenzi unaendelea, hatua ya kutaka kufuta milki ya kiwanja hiki ilianzishwa na Wizara ya Ardhi mwaka 1995, wakati ambao Serikali ilikuwa inatoa fedha za kukamilisha ujenzi wa nyumba moja. Kufuatia uamuzi wa Wizara ya Ardhi, Serikali iliamua shirika lipewe shilingi milioni 26 tu, tofauti na madai halisi ya shirika na cha kusikitisha zaidi hadi sasa shirika limelipwa shilingi milioni 15 tu kati ya shilingi milioni 26 zilizoamuliwa na Serikali. Kambi ya Upinzani inaomba ufafanuzi katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iweke wazi nini kimetokea mpaka Wizara ya Ardhi ikakigawa kwa watu wengine kiwanja hicho ambacho tayari Shirika lilishatumia kiasi cha shilingi milioni 49 katika kukiendeleza. Ni lini Serikali italirejeshea Shirika fedha zake hizo kama linavyodai, sawa sawa na gharama walizotumia kukiendeleza kiwanja hicho? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu kubwa ya Serikali kuwanyang'anya *NIP* kiwanja hicho na kuwapa *IMTU* ilikuwa ni Shirika kushindwa kukiendeleza, lakini hadi sasa hakuna hatua zozote za kukiendeleza ambazo zimechukuliwa na *IMTU. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inataka kujua kama kweli kushindwa kukiendeleza kiwanja hicho ndani ya miaka mitatu ndio iliyokuwa sababu ya kuinyang'anya *NIP* kiwanja chake au kulikuwa na ajenda nyingine ya siri? Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kulirudishia Shirika kiwanja chake baada ya *IMTU* nayo kushindwa kukiendeleza kiwanja hicho kwa miaka yote iliyokabidhiwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ni muhimu sana sio tu kwa kuwahudumia wanachama wake bali hata kwa maendeleo ya nchi kwa ujumla. Mifuko hiyo imekuwa mstari wa mbele katika uwekezaji kwenye sekta mbalimbali za uchumi. Kwa Tanzania japokuwa sekta hii ya hifadhi za jamii bado iko katika hatua za mwanzo ukilinganisha na Mataifa yaliyoendelea lakini inatoa ishara ya matumaini endapo udhibiti wa matumizi ya fedha zao utawekewa miongozo madhubuti na matunda yake ni dhahiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria iliyopitishwa na Bunge lako ya kuundwa kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Hifadhi za Jamii *(Social Security Regulatory Authority Act, 2008)* itaongeza ufanisi wa mifuko hiyo na kuwa mlinzi wa fedha za wanachama. Hii itakomesha matumizi yasiyo na tija kwa baadhi ya mifuko hiyo, matumizi ambayo yamekuwa hayamnufaishi mwanachama wa mfuko husika moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii imeainisha bayana kwamba hifadhi za jamii ziwasaidie wanachama wake kwa kuwapa mikopo ya kujengea nyumba za bei nafuu kwa wale ambao tayari wana viwanja vyao binafsi, tunategemea hilo litatekelezwa. Kwa njia hii hifadhi zitapata mtazamo mpya toka kwa wanachama ambao wanadhani zinatumiwa kuwanufaisha matajiri tu na si kwa wanachama wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Taifa la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii *(NSSF).* Majukumu makubwa ya *NSSF* ni kukusanya michango, uwekezaji wa michango na kulipa mafao kwa wanachama. Kambi ya Upinzani inapenda kuipongeza *NSSF* kwa juhudi hizo za kutimiza wajibu wao. Kwa mujibu wa taarifa zilizopo ni kuwa michango imekua kwa zaidi ya asilimia 30. Mapato kutokana na vitega uchumi vyake yameongezeka kwa takriban asilimia 25. Aidha, kwa utaratibu uliotajwa katika sheria namba 28 ya mwaka 1997 *NSSF* inajitahidi kukamilisha utoaji wa mafao yote kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na *NSSF*, bado yapo maeneo ambayo yanahitaji kushughulikiwa haraka. Moja ya maeneo hayo ni ujenzi wa daraja la Kigamboni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwa muwazi na muungwana kuhusiana na kilichojiri katika kadhia nzima ya ujenzi wa daraja la Kigamboni. Kambi ya Upinzani imeuona uungwana huo wa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kutangazwa zabuni ya daraja hilo kama alivyoahidi hapa Bungeni wakati akifanya majumuisho kwa hotuba ya Bajeti yake mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya waajiri wa sekta binafsi ambao hawafuati sheria za nchi hii na hasa katika kuhakikisha kuwa wanawaingiza wafanyakazi wao kwenye mifuko ya hifadhi za jamii kama *NSSF* na mingineyo na hii huwaathiri sana wafanyakazi hao pindi wanapostaafu ama kupata ajali wakiwa kazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inataka maelezo ya kina kuwa ni kwa nini waajiri hawa wanakiuka sheria za nchi na hawachukuliwi hatua zinazostahiki. Ukiukwaji huu umekithiri sana kwenye Sekta ya Utalii kama vile hoteli ya kitalii, viwanda vya samaki, viwanda vya nguo na kadhalika. Hapa utawakuta wafanyakazi wana miaka 10 kazini lakini bado ni vibarua. Hizi ni hila na ghilba za waajiri hawa kusudi wasipeleke michango ya wafanyakazi hao *NSSF*. Hili limekuwa ni tatizo sugu hapa nchini kwa baadhi ya waajiri. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe kauli kuhusu ujanja ujanja wa aina hii wa makampuni hayo kwa wafanyakazi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka *NSSF* iongeze kasi kwa kujenga majengo kwa ajili ya Vyuo Vikuu kwa kushirikiana na mifuko mingine nchini na hata kutoa udhamini wa makampuni ya nje kwa ubia. Aidha, ujenzi wa ofisi ya Ubalozi wetu kule Nairobi uharakishwe na hilo linaweza kwenda sambamba na kujenga ofisi zetu za Balozi kwenye nchi mbalimbali duniani kwa ajili ya kupunguza gharama na adha za upangaji na ulipaji kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu wa Kenya wanakaribia kumaliza ujenzi wa ofisi yao kwenye kiwanja chao cha Dar es Salaam wakati sisi bado hatujaanza. Hii ni aibu kwa nchi yetu. Tunayapongeza Mashirika yetu kwa ujenzi wa Hosteli za Chuo Kikuu hapa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ajira. Ajira ni suala la msingi sana kwa maendeleo ya Taifa lolote. Duniani kote Serikali zinahangaika kuwapatia watu wake ajira ili kukuza uchumi, kuimarisha huduma na kuboresha kiwango cha maisha. Kila kukicha mikakati inaundwa ya namna ya kutengeneza fursa za ajira. Kwa mujibu wa takwimu za utafiti wa Bajeti ya kaya (*Household Budget Survey*) ya mwaka 2000/2001. Tathmini hii ya mapato na matumizi ya kaya inaonyesha kuwa asilimia 84.2 ya nguvu kazi ya Tanzania inaajiriwa katika Sekta ya Kilimo. Kwa takwimu za zamani, nguvu kazi hii ilichangia asilimia 44.7 ya Pato la Taifa. Kwa takwimu mpya kilimo na uvuvi vimechangia asilimia 30.7 tu mwaka 2001. Ikiwa mchango wa Sekta ya Kilimo ni mdogo kiasi hicho wakati asilimia 84.2 ya nguvu kazi ya Tanzania iliajiriwa katika kilimo mwaka 2001, hii sio dalili njema kwa ukuaji wa uchumi na sekta ya ajira hapa nchini. Kwa kasi hii kamwe hatuwezi kufikia zile ndoto za maisha bora kwa kila Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti wa nguvukazi wa mwaka 2001 ulionyesha kuwa kila mwaka ajira mpya 400,000 zinaanzishwa wakati nguvu kazi laki saba inaingia katika soko la ajira. Serikali ya awamu ya nne iliahidi itaanzisha ajira mpya milioni moja katika kipindi cha miaka mitano wastani wa ajira laki mbili kwa kila mwaka. Waziri ameeleza kwamba katika kipindi cha miezi 18 kuanzia mwezi Julai 2005 hadi Desemba 2007, ajira mpya 412,608 zilikuwa zimepatikana. Ajira 194,325 zimetokana na sekta rasmi na ajira 218,283 zimetokana na sekta isiyo rasmi. Hata hivyo, Kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa katika mwaka 2007 hakina jedwali linaloonyesha ajira hizo na sekta zake. Kitabu hicho kinaonyesha ajira viwandani imeongezeka toka watu 89,316 mwaka 2005 na kufikia watu 91,112, ongezeko la wafanyakazi 1,796 tu. Kwa kadri muundo wa uchumi unavyobadilika ndivyo sekta ya viwanda inavyotegemewa kutoa mchango mkubwa kwa ajira mpya. *(Makofi)*

Aidha, Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge lako Tukufu, hizo ajira zaidi ya laki nne ziko sekta gani au ajira hizo ni ajira hewa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sekta kiongozi kwa kuajiri ni kilimo na kilimo hicho Serikali haikithamini kabisa hivyo basi ni bora ikiri kuwa umaskini vijijini ni wa kutisha zaidi kuliko ilivyokadiriwa mwaka 2001.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna matatizo makubwa sana ya vijana wa Kitanzania kupata ajira kwenye Makampuni mbalimbali ya simu za mkononi hapa nchini na hata wanapopata ajira hizo huwa hawalipwi kiwango sawa na wenzao kutoka nchi jirani za Kenya na Uganda hata kama viwango vyao vya elimu viko sawa sawa. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kufanya utafiti wa kina na kujua ni vigezo gani hasa vinatumiwa katika kuwaajiri na hata kuwalipa vijana wa Kitanzania kwenye Makampuni husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa inafanya tathimini ya kina na kuyajua makampuni haya ya simu za mikononi na kuangalia kama waajiriwa ambao wanatoka nje ya nchi wanasifa za kupata ajira hapa nchini ama laa na je, wana vibali vya kufanya kazi hapa nchini au hawana? Kwani kuna

malalamiko kutoka kwa Watanzania kuwa waajiriwa wengi wao hawana hata vibali vya kufanya kazi nchini ukiachilia sifa ambazo Watanzania hawana *(rare professional)* ila wameajiriwa kinyemela.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ninukuu sehemu ya hotuba ya Waziri wa Fedha aliyoitoa hapa Bungeni mwaka 2004, alisema nanukuu; "Maeneo ya uzalishaji *(production)* ndiyo yatatuondoa kwenye ujinga na umaskini kwa haraka zaidi kuliko mengineyo ambayo ni ya ulaji *(consumption).* Kupanga ni kuchagua pale panapoweza kulivusha Taifa letu haraka haraka. Tutaweza kulima kwa wingi, kusindika mazao hayo kwa wingi na kusafirisha mazao ya kilimo na viwanda hadi nchi jirani." Mwisho wa kunukuu. Wizara ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa sekta ya uzalishaji inakua na kuongeza ajira ili tuweze kukuza uchumi wa Taifa letu hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wa Kitanzania ambao wanajishughulisha na ajira ambazo sio rasmi na hasa biashara ndogo ndogo ambao tumewapa jina la wamachinga wanafanya shughuli zao kwenye mazingira magumu sana kutokana na Serikali kutokuweka mkakati thabiti wa kuwasaidia vijana hawa ambao kutwa nzima wanakuwa wakitembea na bidhaa zao maeneo ya Mijini. Itakumbukwa kuwa kwa kipindi cha mwaka jana Serikali iliahidi kuwa itajenga kituo kikuu cha wamachinga Jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kuwasaidia vijana hawa kufanya shughuli zao eneo moja. Pamoja na hilo Kambi ya Upinzani ina wasiwasi na ujenzi wa vituo vya wamachinga nchi nzima. Hii ni kuhalalisha kuwa sasa Tanzania linakuwa Taifa la wamachinga badala ya Taifa la wazalishaji. Hili ni jambo la hatari sana kwa mustakabali wa nchi yetu. Hivyo basi, tunamtaka Mheshimiwa Waziri kuliangalia upya suala hili ambalo linatekelezwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa malengo ya MKUKUTA ukosefu wa ajira lengo ni kushuka hadi kufikia 6.9% ifikapo mwaka 2010, mwaka 2005 ilikuwa 12.9% mwaka 2007 ni 11%. Kambi ya Upinzani inauliza, je, ni kweli Serikali inafuata miongozo na dira ya MKUKUTA au ni wimbo tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshuhudia Serikali kwa hatua mbalimbali ilizozichukua katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi mwaka 2000 na baadhi mwaka 2005 ambazo naomba baadhi yake kuzinukuu:-

(i) Mashirika ambayo ni ya msingi na nyeti (bandari, reli, posta, simu, mabenki ya umma na nishati) kwa maendeleo ya Taifa yanaendelea kumilikiwa na dola.

(ii) Sera za kurekebisha mashirika ya umma itakwenda sambamba na hatua za kuwalinda wafanyakazi wa mashirika yatakayohusika, CCM itaona kuwa na ajira ya wafanyakazi inalindwa kwa kadri itakavyowezekana, fidia za haki kwa wafanyakazi watakaoachishwa kazi zinatolewa na wafanyakazi wanaoachishwa kazi wanasaidiwa nao waingie katika sekta ya wananchi wanaojiajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inasikitishwa sana kwa jinsi Serikali inavyosimamia na kutekeleza Ilani ya CCM kwa kutokuitekeleza kama

ilivyoahidiwa na kuwaacha patupu wafanyakazi wasijue la kufanya. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inauliza kuwa, je, ni kweli ajira za wafanyakazi zimelindwa baada ya kuuzwa viwanda? Je, wafanyakazi walioachishwa wamesaidiwa kuingia katika sekta binafsi kuwa wajasiriamali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutimiza ahadi ya lengo dogo la ajira milioni moja kwa Watanzania, na kuacha kuwafanyia wafanyakazi hadaa wakati inapohitaji msaada wa wafanyakazi hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inasisitiza kuwa ni lazima kuwe na mkakati maalum, sera na sheria itakayoharakisha kukua kwa uchumi na upatikanaji wa ajira nchini kinyume na hali halisi ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo ya shilingi bilioni moja kwa kila Mkoa. Kwa kuwa lengo kuu la utoaji wa fedha hizo lilikuwa ni kuwawezesha wananchi kiuchumi ikiwa ni pamoja na kuongeza ajira. Huu ni uamuzi ambao kwa ujumla unastahili kupongezwa. Ni ukweli ulio wazi kuwa hadi sasa robo tatu ya fedha hizo zimekwishatolewa katika Mikoa husika, lakini hadi sasa imedhihirika kuwa nusu ya fedha hizo hazijarejeshwa. Urejeshwaji wa fedha hizo unaweza kuwa mgumu kutokana na sababu kadhaa zilizo nje ya uwezo wa wakopaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri atoe tathmini ya kina juu ya mpango huu. Je, mpaka sasa ni ajira ngapi zimeweza kupatikana kutokana na mkopo huu? Je, waliokopeshwa ndio walengwa? Hii ni kwa sababu wananchi wa kawaida ambao ndio walikuwa walengwa wa mkopo huu wanalalamika kuwa hawajauona mkopo huu ila uliwanufaisha zaidi wakubwa na matajiri kuliko kuwanufaisha wao. *(Makofi)*

.

Mheshimiwa Naibu Spika, tujiulize, hivi kinachokuja kwanza ni nini wazo la biashara ama mkopo? Mtizamo wa Serikali hii ni kutanguliza mbele mikopo tena midogo midogo. Kwa misingi hii, hoja ni kwamba vijana wanao utamaduni na nidhamu ya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inasema hili ni kosa kubwa kwani Watanzania hatukulelewa kwa misingi ya biashara vivyo hivyo na kwa vijana wetu. Mikopo midogo midogo isiyotanguliwa na elimu inaweza kuwa chanzo cha umaskini kutokana na kushindwa kwa biashara kutaka kuzalisha madeni makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaweka mkazo katika kujiajiri hususani kwa kukuza sekta isiyo rasmi. Sekta hii bado inakabaliwa na changamoto mbalimbali. Tafiti zinaonyesha kuwa zaidi ya theluthi mbili ya biashara ndogo ndogo zilizoanzishwa na watu waliotazamia kujiajiri wenyewe zinakufa kabla ya kufikisha umri wa miaka mitano kutokana na upungufu wa mafunzo ya stadi za biashara miongoni mwa vijana, elimu ndogo miongoni mwa wajasiriamali vijana na isiyojitosheleza, utamaduni wa watu wengi kupenda ajira rasmi zaidi ya kujiajiri na kutovutia au kutelekezwa kwa kilimo ambayo ni sekta kuu ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutofanikiwa wakati mwingine kwa biashara hizi pia kunatokana na mali/mitaji ya akinamama na vijana hawa kuharibiwa au kupotea na wao wenyewe kuishia mikononi mwa Polisi na au askari wa Jiji na mgambo kama wahalifu. Wakati mwingine tunawahamisha waende katika maeneo ambayo hayafikiki kirahisi na hivyo kuwakosesha wateja. Kwa misingi hii hatujengi Taifa bali tunabomoa Taifa hili ambalo ni changa bado kiuchumi na linalokua kwa taabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hili ambalo linasababisha kupotea kwa mitaji ya wajasiriamali kwa kiasi kikubwa lilitokana na kutokufanyika kwa upembuzi yakinifu juu ya fursa na vikwazo vya maendeleo kwa kila Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuliona hilo, tarehe 5 Julai, 2007, Mheshimiwa Kabwe Zitto, alimwandikia Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana wakati huo Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe akimshauri njia muafaka ya jinsi fedha hizo shilingi bilioni moja zitakavyofikia lengo lake kuu. *(Makofi)*

Moja ya mapendekezo hayo ni kuwa kwa kuwa kila Mkoa una viashiria tofauti vya kukuza uchumi, hivyo basi, upembuzi yakinifu ufanyike kuhusiana na hilo kabla ya kutoa hizo fedha na alishauri msimamizi mkuu wa washauri *(supervisory consultant)* awe ni yule anayefanya kazi na MKUKUTA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inasikitika kuwa viongozi wetu kwa sababu zao binafsi wanashindwa kuwa na maono, alichoshauri Mheshimiwa Kabwe Zitto, sasa hivi kingefanyika kingeinufaisha Mikoa kwa kuongeza ajira. Kambi ya Upinzani inaamini kabisa kuwa kama ushauri huo ungetolewa na wahisani basi usingeachwa kama ulivyoachwa huo wa Mheshimiwa Kabwe Zitto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baya zaidi hadi sasa tunapowasilisha hotuba hii majibu ya barua yake kutoka kwa Mheshimiwa Waziri hajayapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inadhani sasa ni wakati muafaka kwa Serikali kuangalia upya taratibu na mipango yake ili fedha hizi zitumike vizuri na ziwasaidie walengwa. Ipo haja ya kuwapa vijana wajasiriamali mafunzo ya jinsi ya kuendesha biashara zao vizuri. Hilo likishafanyika ndipo dhana ya kujiajiri itakuwa na maana kwa vijana wa nchi hii. *(Makofi)*

Kambi ya Upinzani inasema hii inaweza kufikiwa kwa kufanyika kwa tafiti za upembuzi yakinifu kwa kila Mkoa kuangalia viashiria vya ukuaji uchumi kwa Mikoa hiyo na ndio sababu nchi zilizo makini na maendeleo Bajeti ya *Research and Development* inakuwa ni kubwa na inakuwepo miaka yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati akitoa hotuba ya kuliahirisha Bunge mwezi Agosti, 2006, Mheshimiwa Waziri Mkuu wa wakati huo aliunda Kamati ambayo ingeshughulikia utaratibu wa kutoa mikopo hiyo. Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge lako Tukufu ni kazi gani imefanywa na Kamati hiyo

kwani hadi sasa walengwa wamekosa mikopo hiyo japokuwa vigezo vyote vilivyohotajiwa walivitimiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uhitaji wa kigezo cha uzoefu katika ajira. Kambi ya Upinzani inalileta tena suala la uhitaji wa uzoefu katika ajira kwa ajili ya mjadala. Tujiulize na kujadili tukikumbuka matangazo mbalimbali ya ajira. Ni asilimia ngapi ya matangazo hayo hayana kigezo cha uzoefu?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inatambua na kuthamini mchango wa uzoefu katika utumishi na kazi. Hivyo, kambi haina tatizo uzoefu kuendelea kuwa kigezo cha muhimu katika kuajiri. Lakini, Kambi ya Upinzani haioni umaana wa uzoefu kutumika kama kigezo cha lazima. Utaratibu wa sasa wa asasi nyingi za Serikali na sekta binafsi kutumia uzoefu kama kigezo cha lazima unawazuia vijana wahitimu ambao hawajafanya kazi bado, hata kupata nafasi ya kusailiwa na kupimwa uelewa na vipaji vyao kuhusiana na kazi husika ni kuwanyima haki yao ya msingi. Watapata lini uzoefu bila kupata fursa ya kupata uzoefu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iweke utaratibu wa kuishawishi sekta ya umma na binafsi kupenyeza mabadiliko katika utaratibu wao kuhusiana na suala hili la uzoefu kwa kutoa motisha ya vyeti vya punguzo kidogo la kodi kwa makampuni yatakayochukua wanafunzi toka vyuoni moja kwa moja *(graduate tax relief certificate).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara yetu ya kazi haifanyi kazi yake ipasavyo ya kuwaunganisha waajiri na wanaotafuta kazi ili kurahisisha kazi ya kupata ajira na kuwa na mikakati ya kuwasaidia wazalendo ni muhimu mambo yafuatayo yafanyike, kwanza tuwe na upendeleo wa makusudi kwa wazawa katika kutoa fursa za biashara na uwekezaji nchini kila mwekezaji lazima awe na mshirika Mtanzania katika uwekezaji huo. Hii iambatane na kuwapunguzia ugumu wowote unaoweza kujitokeza wakati wa utoaji wa fursa hizo za biashara na uwekezaji na pili, tuwe na vigezo tofauti vya kutoa mikopo na vivutio vya biashara ili tuwasaidie wazawa kutengeneza fursa nyingi za kazi na kuajiri watu wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, tuwe makini katika kutoa vibali vya kazi kwa wageni ili kuhakikisha wawekezaji wanafuata sheria na masharti ya ajira katika kuwekeza nchini kwetu kwani sheria ziko wazi kuhusu mgawanyo wa ajira kati ya wageni na wazawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Idara ya Vijana, vijana ni sehemu muhimu sana ya nchi yetu. Ni muhimu kwa sababu ya nafasi yao katika uchumi wa Taifa na uhai wa Taifa kwa siku za usoni. Kiuchumi, hii ndiyo nguvu kazi ya Taifa ambayo inatarajiwa kuzalisha na kuleta tija. Ili waweze kushiriki vizuri lazima wawekewe fursa katika uchumi ili waweze kujiajiri na wengine kuajiriwa na kuajiri wengine. Taarifa za tafiti na takwimu mathalani, MKUKUTA zinatuonyesha kuwa suala la vijana kutokushirikishwa katika uchumi wa nchi ni suala mtambuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sera ya maendeleo ya vijana. Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2002 vijana wa kati ya miaka 15 mpaka 35 ni takribani 11,775,259.

Hivyo hili ni kundi ambalo halipaswi kupuuziwa. Na zaidi ukitazama hali ya vijana nchini; wengi wao hawana ajira, wengi wao wamekata tamaa, wao ndio waathirika zaidi wa UKIMWI na mambo mengine. Kwa vyovyote vile, tusipoweka kipaumbele kwa kundi hili Taifa lipo katika bomu la wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapaswa kubadili mtizamo wetu kuhusu vijana na kuwatazama kama suluhisho badala ya tatizo. Kwa asili vijana ni kundi muhimu kiuchumi kama wazalishaji wakuu, ndio wenye uwezo wa kulisukuma Taifa mbele kutokana na nguvu na ubunifu wao. Ndio maana maendeleo ya vijana inapaswa kuwa ajenda mtambuka *(cross cutting agenda)* kwa sekta zote. Kwa kuwawezesha wazee tunajenga Taifa lipitalo, kwa kuwalea watoto tutajenga Taifa la kesho, kwa kuwezesha vijana tunawekeza katika Tanzania ya leo na kesho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tufike huko tunahitaji sera muafaka ya maendeleo ya vijana. Kwa muda mrefu tumekuwa tukitumia sera ya maendeleo ya vijana ya mwaka 1996. Kwa vyovyote vile sera hii imepitwa na wakati. Kwa miaka kadhaa sasa imekuwa ikitoa matamko kwamba iko katika mchakato wa kuibadili sera hii. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge ni lini sera ya maendeleo ya vijana itakuwa tayari?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote na Watanzania kwa ujumla kwa kunisikiliza na ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, ahsante sana kwa kwa hotuba nzuri uliyoandika. Sasa tunao wachangiaji wafuatao, Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu moja au nyingine kuna wengine wameleta vi-*note* wanaomba kuchangia siku ya Jumatatu, sisi tunawatoa wote walioandikishwa hapa kama hawapo hatuwezi kuahirisha Kikao kwa sababu watu watachangia siku ya Jumatatu. Tunaendelea tu.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, ambaye atakuwa hayupo basi tena, maana hatuwezi kukatisha Bunge mchana tukasema hawa waliobaki watachangia Jumatatu, kwa hiyo, tunaahirisha Kikao hiyo haiwezekani. Kwa hiyo, wale walioniandikia vi-*note* kuwa watachangia siku ya Jumatatu, nawashauri wabakie humu ndani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa ambao hawajachangia hata mara moja ni Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Monica Mbega. Waliochangia mara moja ni Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa Maulidah Komu, Mheshimiwa *Eng.* Stella Manyanya, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, ndiyo hawa. Wengine sasa humu ndani hawamo wamekwenda kwenye msiba, lakini watakuwepo baadaye jioni. Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya mwanzo katika kuchangia katika Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, umefanya jambo zuri sana leo kwa sababu mimi ni Naibu Katibu wa Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi. Lakini hapa nitatetea vijana wa Chama cha Mapinduzi na vijana wote wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuanza kuchangia kwa huzuni kubwa napenda kumpa pole mwenzetu Mheshimiwa Savelina Mwijage kwa kumpoteza mtoto wake na dereva kwa ajali ambayo imetokea leo, kwa kweli tunampa pole sana tuko pamoja na yeye na Mwenyezi Mungu ampe subira.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sana kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi yake nzuri ambayo anaifanya pamoja na ushirikiano mzuri na Naibu wake Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga na Katibu wake Mkuu na vile vile viongozi wa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia kabla sijasahau. Napenda kuitaja kwanza dhana ya ujana. Dhana ya ujana kwanza tutambue kwamba vijana ndiyo Taifa la leo na vile vile ni viongozi wa leo na Taifa la baadaye. Lakini tukitazama hawa vijana kwamba ni Taifa la leo na vile vile ni Taifa la baadaye. Lakini ukichunguza kwa undani hawa vijana wanaonekana kama ni watu ambao wanadharauliwa sana na ni kwa kweli vijana ni kama jamii ambayo inaleta msukumo mkubwa katika Taifa hili katika kuletea maendeleo Taifa hili. Kwa sababu vijana mbali na yote, lakini pia tunawatumia katika harakati za chaguzi mbalimbali wao ndiyo *campaigner* wakubwa na ndiyo wapigaji kura wakubwa wa vyama vyetu. Kwa hiyo, napenda sana kwanza kuwapongeza vijana wote wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna mkanganyiko kidogo wa umri wa vijana, sisi kwenye chama chetu tunao vijana wenye umri na Serikali tunajua pia wana umri lakini watu wengi hawaelewi dhana hii ya vijana mwanzo wake ni miaka mingapi na ukomo wake ni miaka mingapi. Huwa kuna mkanganyiko kidogo kwa wananchi. Kwa hiyo, naomba hapa akija kujibu Mheshimiwa Waziri atujibu inakuwaje hii miaka inakwendaje maana yake wengine wamefikisha miaka 50 lakini wanajiita vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira kwa vijana. Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 mpaka 2010 imedhihirisha wazi kwamba kuwe na ajira ama kutakuwa na ajira milioni moja ifikapo mwaka 2010 kwa ajili ya vijana. Vijana hawa napenda kusema kwamba tunaweza tukafikia lengo kwa sababu Serikali yetu ina mkakati madhubuti wa kufikia huko. Tunahakikisha Serikali tunapenda kwamba ikifika mwaka 2010 vijana milioni moja wawe wameshaajiriwa na hiyo tunaihakikisha kwa sababu hii ni Serikali ya Chama cha Mapinduzi inafanya kazi kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia napenda kuwasemea hawa vijana wa Vyuo Vikuu, tunafahamu kwamba katika Wizara hii kuna ile *labour bank*, vijana ambao wanamaliza masomo yao ya Vyuo Vikuu huwa wanajiandikisha Wizarani. Napenda kuelewa kwamba vijana hao wanaojiandikisha kule Wizarani katika Tanzania nzima ama

sehemu za Mikoani kwao ni wangapi wote, na vile vile wapi ambao wameajiriwa kupitia hiyo *labour bank?*

Mheshimiwa Naibu Spika, hasa tukitilia maanani katika ile *labour bank* sana wanaoajiriwa ama wanaopata ajira wengi wao tunaweza tukasema ni vijana ambao wanamaliza Chuo Kikuu. Lakini vile vile mimi naamini sijui lakini nasema kwamba mimi natetea vijana maskini sifikirii kama vijana wa kimaskani wengi wanapata ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naamini kwamba vijana hawa wengi walio na wazazi wao *well-off* sijui wakubwa, matajiri, mimi naamini hawa ndiyo wengi wanaopata ajira na elimu kama ni Chuo Kikuu wamemaliza wote. Mtoto wa kimaskani kasoma kapata elimu na vile vile mtoto wa tajiri kapata elimu tusiwe na ubaguzi. Naomba sana Mheshimiwa Waziri hili ulione. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napenda kuuliza kwamba wale vijana wa Zanzibar wanaomaliza Vyuo Vikuu kwa Vyuo Vikuu vya Muungano, je, na wao wale wanapokelewa vipi katika *labour bank* na wangapi wameajiriwa? Na wangapi wanawake wa Vyuo Vikuu kutoka Zanzibar wamepata ajira kupitia huo mpango? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo kwa vijana, kwanza napenda kumshukuru Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuanzisha Mfuko huu wa JK. Haijapata kutokea naamini dunia nzima. Lazima tumpongeze Rais wetu katika kuwasaidia vijana wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ila napenda kuuliza je, ni kweli ile azma ya Mheshimiwa Rais Kikwete kweli inatekelezwa ilivyo na ni kweli hao vijana ambao waliolengwa ni kweli wanaopata mikopo? Au wanaopata mikopo ni watu wanaofanya kazi matajiri wakubwa wakubwa wanaongezewa? Mimi naomba hizi bilioni moja kwa kila Mkoa na milioni 100 kule Tanzania Visiwani naomba ziwafikie walengwa, vijana waliojiuna na *SACCOS* mbalimbali, zipo *SACCOS* nyingi. Tunaomba zifike mpake vijijini. Inasemekana kwamba zinatumiwa vibaya. Kwa hiyo, naomba ufuatiliaji wa karibu uwepo katika fedha hizi za JK hapo ndiyo tutaweza kuwakwamua vijana katika kujileteama endeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kwenye unyanyaswaji wa vijana wanaofanya kazi kwenye makampuni ama sekta binafsi. Nasikitishwa sana kampuni binafsi ama mashirika binafsi wanatumia nguvu zao katika kuwadhalilisha vijana katika kuwafanyisha kazi. Ni wengi tunaweza tukasema mfano viwandani, migodini, hotelini, shambani kwenye mashamba ya chai huko mashamba tofauti, vijana wanatumiwa vibaya. Kwa sababu hawana uwezo wa kwenda popote lazima waende pale, vijana wanatumiwa vibaya, ajira hizo ambazo hawawekewi mikataba ambayo ni mizuri, wanaajiriwa tu kesho wanafukuzwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajionea wenyewe kwenye televisheni hata sisi viongozi tukitembelea tunawaona watu wa viwandani jinsi wanavyofanya maandamano, waajiri wanawadhalilisha sana. Naiomba Serikali ifuatilie sana waajiri hawa binafsi wengine sio wazuri wanawanyanyasa sana hasa wanawake. Mfano kama mtu anafanya

kazi katika hoteli hasa pale Dar es Salaam mimi ninao ushahidi. Nilipata *aunt* mmoja akawa ananiambia, bwana mimi nafanya kazi hapa hotelini lakini sisi hapa toka asubuhi tutakapokuja saa 12.00 tunaondoka saa 5.00 usiku, hatupewi hata kikombe cha chai, mtoto wa kike. Halafu mfano akipiga deki mle kwenye sehemu za hoteli zile wanaambiwa mpaka wainame migongo, hakuna dekio la kusimama lile, hiyo haisafishi hiyo lazima uiname mgongo kila siku, hivyo kijana mwanamke kila siku atainama mgongo katika kusafisha au atakuja toka asubuhi saa 24 mtoto anafanya kazi hakuna likizo, hakuna siku za mapumziko mpaka Jumamosi vijana wanafanya kazi kwenye hoteli. Naomba mtembelee hoteli za Dar es Salaam na kwingineko mtaona hiyo ili ifuatiliwe iondoke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia Mwenge wa Uhuru. Mwenge wetu wa Uhuru kwanza napenda kuishukuru Serikali kwa kuanzisha hili kwamba kila mwaka kuna mzunguko wa matembezi wa Mwenge wa Uhuru. Mwenge wetu wa Uhuru ni mwenge ambao unaleta maendeleo katika nchi yetu. Kwa sababu mwenge huu unapotembea katika sehemu ya Tanzania unahamasisha wananchi katika kujiletea maendeleo katika kuendesha miradi mbalimbali katika kufungua miradi mbalimbali ya maendeleo na kadhalika. Lakini nashangazwa kuna watu wengine wanaunyanyasa huu mwenge wa Uhuru eti mwenge wa Uhuru unaleta UKIMWI. Hivyo nani atakayesema kama Mwenge unaleta UKIMWI. Eti mkesha wa Mwenge unaleta UKIMWI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata juzi yuko Mbunge mmoja hapa alisema namshangaa sana UKIMWI unaletwa na wewe mwenyewe. UKIMWI hauletwi na mkesha wa mwenge. Tabia yako ndio inayokufanya wewe upate UKIMWI, lakini sio mwenge, tusiudhalilishe mwenge wa Taifa. Leo tunasema mwenge wa Tanzania kuna mwenge wa *Olympic* na unatembea dunia nzima, je, huu mwenge wa hapa hapa kwetu mwenge wa Uhuru ni mwenge unaoleta vichocheo vya maendeleo katika nchi yetu? Naipongeza sana Serikali na isisite kila mwaka. Napenda pia kuwapongeza watembeza mwenge na napenda sana kuwapongeza vijana imara sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wajasiriamali wamachinga. Zamani nilikuwa nachukia sana kuona wale vijana wamachinga wanavyonyanyaswa wanafukuzwa mara huku mara huku yaani mimi siku nyingine huwa natokwa na machozi. Lakini sasa naona Serikali imeona kwa sababu Wabunge tunapiga sana kelele na Serikali yetu ni sikivu, tunaishukuru sana Serikali kuwawekea nafasi ile wamachinga ili kuja kufanya kazi zao kwa burudani kabisa, tunaipongeza sana Serikali. Lakini kama walivyosema wenzangu mmoja akasema isiendelee mikoani lakini na mimi napenda hata kule mikoani majengo kama yale yawe yanajengwa kwa sababu wamachinga hawako Dar es Salaam tu, wamachinga wako kila sehemu. Lakini naomba kabla ya kufanya hivyo kazi katika maeneo wapewe elimu nzuri ya mambo ya biashara zao na vile vile kulitunza hilo jengo ambalo limejengwa kwa ajili yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, UKIMWI na vijana. Hapana asiyejua kwamba waathirika wakubwa wa janga hili ni vijana, *teenagers* hao ambao wanaingia kwenye rika ya kuhangaika hangaika. Hili rika ni baya sana lakini tunatakiwa Serikali iendeleze elimu ya UKIMWI ya mijini na vijijini isitoe elimu na semina mijini tu lakini iende mpaka vijijini na sisi viongozi wote tushirikiane na tunafanya hiyo kazi ila napenda kuwashauri

wazazi wa majumbani wazazi wenzangu tusiwaonee aibu watoto wetu kuwaweka kitako kuwaelimisha, mwanangu UKIMWI ni hivi hivi, usione aibu muelimishe mtoto aelewe pengine mtoto anafanya au kijana anafanya kwa sababu haelewi, si wote ambao wanakwenda kwenye semina. Si wote ambao wanapata elimu kutoka kwenye *TV* na redio wengine hakuna. Tukae na watoto wetu tuwaelimishe janga hili ni baya, janga hili ni sakili, kwa hiyo, wajiepushe na sisi wenyewe tujiepushe na ngono zembe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sana kuchangia mambo ya dawa za kulevya dhidi ya vijana. Vile vile kama UKIMWI, dawa za kulevya sana sana zinakwenda kwa vijana. Vijana wanapokaa pamoja au wanapokaa hawana kazi, hawana ajira wanakuwa wana unyonge sana hawajui la kufanya, wanakaa kwenye vigenge katika mazungumzo yao wanapeana pale aah, bangi safi, *cocaine* hebu onja kidogo, kitu kama hiki.

Naomba sana vijana waepukane na magenge hayo. Ukimwona kijana mwenzako anakushauri kuhusu bangi mambo ya dawa za kulevya huyo sio rafiki. Tunaomba sana vijana waelimike, Serikali inaelimisha kila siku lakini naomba sana vijana wajielimishe pia wenyewe kwa kuona kwamba kijana ambaye atakuja kunishauri mimi kuhusiana na dawa za kulevya au bangi na mambo mengine mabaya yoyote na ngono na kila kitu huyo si rafiki mzuri, muepuke. Nashukuru sana Serikali yetu inajitahidi kwa hilo katika kuelimisha na iendelee kuelimisha vijana wetu dhidi ya dawa za kulevya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia naomba kuchangia ama kupongeza Mashirika haya kama *NSSF,* napenda kulipongeza sana hili Shirika jamani uongozi wake ni mzuri sana. Uongozi wa Shirika hili ni mzuri sana na vile vile mashirika yale mengine ambayo yamejenga majengo ya Chuo Kikuu cha Dodoma jamani aliyekuwa hajapata kwenda kuona yale majengo aende, huwezi kujua au huwezi kuamini ukifika kule. Majengo ni mazuri, hosteli ni nzuri yaani Serikali pale imefanya kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishukuru Serikali yetu pale iendelee kujenga hosteli kama hizo katika Vyuo Vikuu sehemu nyingine na nyingine. Natamani waje Zanzibar pia wajenge majengo kama yale. Mheshimiwa Waziri nakuomba sana tunahitaji na majengo ya Vyuo Vikuu kule Zanzibar na sisi yawe majengo kama yale ili *NSSF* ikija Zanzibar kwa kweli itakuwa imetukomboa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana naomba kuunga mkono hoja tena mia kwa mia, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante walipokuja Wabunge wa Kenya walipelekwa kule, walipofika kule walishangaa kweli kweli wakasema ninyi Watanzania sasa mnatufanyia mchezo mnataka sisi tuwe tunawafuata nyuma nyuma. Walisema watawatumia wale Wabunge kupeleka Muswada Binafsi mle ndani kusudi watumie Mifuko ya Jamii hii kufanya maendeleo kuliko kuweka fedha Benki ziwe zinakaa ndio zilikuwa *comment* zao na mimi nilikuwa na wale wageni. Nakubali kweli yale majengo na ni *NSSF* nafikiri na *PPF* na wale wengine *Local Government Provident Fund* wamefanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Sasa nitamwita Mheshimiwa Shally Raymond na Mheshimiwa Monica Mbega, ajiandae, tunaweza na Mheshimiwa Anna Lupembe pia ajiandae.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai. Pia nawashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Kilimanjaro walionituma hapa kwa ridhaa yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pole kwa Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Savelina Mwijage kwa janga kubwa lililowapata asubuhi ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, Katibu Mkuu na Naibu wake na watendaji wote kwa kutuandalia hotuba nzuri ambayo tunaijadili asubuhi hii ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia maeneo mawili tu. Eneo la ajira na pia lile eneo la fedha zilizotolewa na Mheshimiwa Rais ili kuwawezesha vijana na akinamama. Ajenda ya ajira ni jambo kubwa duniani na linasumbua sana hata mataifa yaliyoendelea. Hapa kwetu ni zaidi na inapotokea kwamba ajira hakuna basi vijana wetu wanakuwa katika makundi ambayo yanasababisha uhalifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tungependa sana vijana wote waajiriwe wakati wa umri ukifika kwamba wanaweza kufanya kazi na ukizingatia kwamba vijana wetu Tanzania wana nguvu na wanalelewa katika mazingira ya kufanya kazi. Bahati mbaya sana jambo hili haliwezekani. Tumepokea hotuba nzuri ya Waziri iliyoeleza na kuonyesha majedwali mbalimbali zikiwemo takwimu za fedha zilizotolewa na pia zikionyesha mikoa na sehemu zote ambazo zimefanikiwa. Tatizo nililopata katika takwimu hizo au katika majedwali hayo sikuona idadi kamili ya vijana ambao hawakufanikiwa ukilinganisha na vijana waliopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba na kushauri ikiwezekana basi tuwe na idadi kamili ya vijana wetu ambao wako katika umri wa ajira, vijana hao tujue wana ujuzi kiasi gani au wana elimu ya darasa la ngapi au wamemaliza vyuo gani? Nasema hivyo kwa sababu tunapochukua wote kwa mkumbo tukasema kwamba ajira zimekosekana wakati ambapo wengine wangeweza wakasaidiwa kuwafungulia aina ya ufundi inakuwa kwamba hapa tunajichanganya. Sisi tuko tayari kabisa katika maeneo yetu kutumia watendaji wa Kata, kutumia viongozi wetu wa Wilaya na hata mikoa ili waweze kuandaa takwimu hizo lakini je, si ingekuwa vizuri kama hiyo ingekuwa ni jambo la Serikali la kufa na kupona? Hivi majuzi vijana wetu walikuwa wakimaliza shule wanakaa wanazubaa tu tukaanza na tukafanikiwa ujenzi wa shule za sekondari. Jambo ambalo lilifanyika usiku na mchana kwa kujitolea na kwa usimamizi mzuri na sasa vijana wetu wakimaliza darasa la saba wengi wao wanaweza kwenda kidato cha kwanza mpaka cha nne. Ni kutokana na hilo basi nasema yawezekana pia kupata takwimu za vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vyama vya dini, kuna vyama binafsi ambavyo vinaweza vikatumika kutafuta takwimu hizo tukajua nchi hii tuna vijana wangapi ambao wamekaa tu na pia wangeweza wakapatiwa ajira. Ongezeko la uhalifu katika nchi yetu linachangiwa sana na ukosekanaji wa ajira. Hapa utaona kwamba vijana hawa kwa nia nzuri kabisa wangependa wakakaa mahali wakaajiriwa na wenyewe wakapata riziki. Lakini hakuna na wanakatishwa tamaa sana pale ambapo wanaomba kazi na kuambiwa kwamba hawana ujuzi au hawana *experience*. *(Makofi)*

Sasa nauliza hivi kijana aliyemaliza Chuo Kikuu ana *experience* gani? Huko tulikotoka sisi ilikuwa ukikaribia kumaliza Chuo wanakuja watu kutoka Utumishi na wanaonyesha ni ajira zipi ziko wazi mtu unachagua ajira ambayo unataka. Hilo lilifanyika labda kwa vile tulikuwa wachache. Lakini haina maana kwamba sasa hivi watu hawaajiriwi, wanaajiriwa na bado wataendelea kuajiriwa. Kwa nini basi, kwa wale ambao ajira zao ziko wazi wasitumie mpango huo? Mbaya zaidi vijana wetu wanaomaliza chuo hawajui ni namna gani wapate ajira, wanadhani labda bado kuna ile kitu ya kutafutiwa kazi jambo ambalo halipo. Sasa wanaosumbuliwa zaidi ni Wabunge au ndugu zao ambao wanafanya kazi kwingineko. Jambo hili ningeomba ikiwezekana kwenye vyuo waelimishwe namna ambavyo wanaweza wakatafuta kazi na sio tu kwa kutumia hiyo *data bank*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi juzi na sio juzi ni jana tu Mheshimiwa Waziri Mkuu ametueleza jinsi gani zile hela alizotoa Mheshimiwa Rais hazikuweza kufanikisha azma yote kwa sababu pia kuna matatizo yaliyojitokeza. Mimi hapa nataka nichangie baadhi ya matatizo ambayo nayaona kule nilikotoka au kwa wengine ni kikwazo kikubwa. Mikopo inayotoka kiwango chake ni kidogo na wale wanaofanikiwa kuchukua hata kwenye *SACCOS* wanapewa muda mfupi sana wa kurejesha. Kama vile haitoshi riba yake ni kubwa na hapa nitaanzia na lile la riba. Mikopo hiyo imetolewa na Mheshimiwa Rais ipatiwe wananchi kwa riba ya asilimia 10 na hilo ndilo linalofanyika wakati *SACCOS* zinakwenda kukopa. Lakini *SACCOS* zinapofika sasa kwenye Ofisi hawawezi tena kutoa mikopo hiyo kwa ile asilimia 10 tu kwa sababu *SACCOS* zenyewe zinatakiwa kujiendesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo wana-*SACCOS* wenyewe wanakaa na kuongeza asilimia kati ya tatu mpaka tano ili waweze kuendesha ofisi zao. Inakuwa sasa mkopo ule utatoka kwa asilimia 15. Anapouchukua mwana-*SACCOS* au anapouchukua mwananchi sasa anakwenda kufanyia kazi mkopo asilimia 15 atafanya biashara yake na hapo anatakiwa akishafanya kazi faida anayopata aende akaweke kwenye akiba. Anarudi kwenye *SACCOS* au kwenye Benki kuweka akiba. Akiba hiyo anapoweka yeye analipwa asilimia mbili au tatu tu na hiyo ndio *rate* ambao wanatoa sasa hivi kwenye mabenki.

Sasa vijana wetu wanajiuliza na hao wamekuwa wakiniuliza kwa sababu mimi nilikuwa nafanyia kazi Benki. Hivi wewe mama inakuingia akilini tukuchukue mkopo wa asilimia 15 halafu tunapokwenda kuweka hela yetu tupate asilimia mbili. Nasema hivyo nikiwa na maana kwamba wanapoweka kwa 2% shilingi laki moja wanapata shilingi 2,000/= kwa mwaka sasa wanauliza tutawekaje hela ambayo inazalisha kidogo hivyo. Hapa nilikuwa naiomba Serikali iangalie endapo itashusha riba hiyo labda ifike

mpaka asilimia tano na wao wanapokwenda sasa kukopa *SACCOS* walipe asilimia saba mpaka 10. Nikiwa na maana kwamba hiyo itakuwa na motisha kidogo kwa sababu wao sasa hawatalipia tena ile asilimia ya kuendesha hizo *SACCOS. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini siishii hapo nilikuwa naomba pia hizo *rates* za Benki za kuwekeza ziwe na mvuto, ziwe na motisha angalau ziangaliwe basi zipande kidogo hata tunaposema *Savings and Credit* hiyo *Savings* iwe na maana. Mtu hawezi kupeleka hela Benki shilingi laki moja kwa ajili ya kuwekeza akizingatia kwamba anakatwa pia *service fee* kwa hiyo, hela yake inakwenda ikipungua badala ya hela kuongezeka. Hili jambo linawanyanyasa vijana wetu na pia linawanyanyasa wale akinamama waliofanikiwa kuchukua mikopo hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwango wanachopewa ni kidogo. Ninapokuja kwenye kiwango nasema kwamba baadhi wanapewa kati ya shilingi 50,000/= mpaka 200,000/= ni hela kidogo kwa kweli. Hata kama tunasema ni ile ya kununua vitu na kuuza, lakini je, unaponunua na kuuza kwa kiwango cha shilingi 200,000 halafu unaambiwa urejeshe kwa miezi sita kweli utakuwa umeizungusha hiyo hela na kupata mtaji? Hapa naona muda ni kidogo sana na ningependekeza kwamba wapewe sasa kati ya mwaka au miaka miwili ili waweze kufanya *projects* ambazo zitawawezesha kuzalisha mtaji wa kuendeleza shughuli zao. Hiki ni kilio na nimetumwa na wananchi wa Kilimanjaro nikilete hapa Bungeni na Serikali yetu isaidie kuliangalia jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba sasa nirudi kwenye hotuba rasmi ya Mheshimiwa Waziri na hapa nakwenda kwenye ukurasa wa 14 kifungu G. Hapa kuna hela tulizoelezwa kwamba ni za Mfuko wa Dhamana. Naomba kusoma Kifungu G kinaelezea; "Wizara iliendelea kuratibu fedha za Mfuko wa Dhamana *(Revolving Fund)* wa Mradi wa Usawa wa Jinsia na Ajira Bora kwa Wanawake, jumla ya mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 888 ilitolewa kwa wajasiriamali 3,800 nchini."

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanzoni niliposoma nilidhani ni hizi hela za Mheshimiwa Rais lakini nilivyoendelea kifungu H kilielezea hela za Mheshimiwa Rais. Sasa nauliza wakati ambapo kuna fungu lililotolewa na Rais wote tukaelimishwa nchini na tukaelewa na tukahamasisha hizi hela zilizo kwenye kifungu G ni hela zipi, mbona hatujaelimishwa hela hizi tukaweza kuwapigia debe au tukaweza kuwaelewesha akinamama wetu waweze kunufaika kwa hela hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba wakati Waziri anatoa majumuisho aweze pia kunielezea kuhusu hela hizi ili sisi tuweze kuwafahamisha akinamama ambao wanazihitaji na tujue zitapatikana vipi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naona pia nichukue fursa hii niipongeze mifuko ya fedha ambayo pia imepitisha Muswada hivi juzi, bado havijarudi, lakini Muswada ulileta Bungeni itakayofanya mifuko yote iweze kutoa riba ambayo itafanana fanana. Kwa hiyo, hapo labda itasawazisha *NSSF, PPF* na hiyo mingine iwe inatoa huduma bora zaidi kwa wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nitakuwa sijatenda haki na pia nitakuwa kwa kweli mtovu wa nidhamu kama sitachukua fursa hii kuwashukuru sana viongozi wa zile Benki ambazo wameweza kufanikisha hela ambazo zimetolewa na Mheshimiwa Rais zikakopesheka.

Lakini hapo hapo nilikuwa nawaomba pia kwa zile Benki ambazo zipo kwenye miji ya mikoa tu wafanye juhudi zozote zile ili ifike pia kwenye miji ya Wilaya kwa sababu wananchi, vijana wanapochukua nauli kwenda mijini hii nayo inakuwa ni hasara au inakuwa ni matumizi yasiyohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano tu, mtu kama yuko Same akachukua mkopo huu ili arejeshe lazima aende Moshi Mjini. Mtu aliye Mwanga na kwingineko popote Rombo ambako ni mbali na mji mpaka Siha, mpaka kule Hai, bahati nzuri Hai kuna Benki ya *CRDB* ambao ndio wengi wamekopa, lakini sasa wengine inabidi mpaka waje mjini. Nilikuwa naomba watumie utaratibu wa kufungua matawi huko ili pia iwapunguzie gharama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru tena sana na pia naomba niwashukuru Wabunge wenzangu kwa kunisikiliza, ahsanteni sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MONICA N. MBEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika hotuba hii ya Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea naomba nichukue nafasi hii kumpa pole nyingi sana Mheshimiwa Savelina Mwijage, kwa msiba mkubwa huu alioupata tunamwombea Mwenyezi Mungu amweke kijana wake mahali pema peponi, *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba nichukue nafasi hii kutoa pongezi nyingi kwa vijana wetu wa Timu ya chini ya miaka 17 waliokwenda Brazil na kweli natoa pongezi kwa sababu pia nikiwa Mkuu wa Mkoa Ruvuma kuna vijana watatu wanatoka Mkoa wa Ruvuma na wamefanya kazi nzuri sana. Kwa maana hiyo basi nitoe tu ombi kwa Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii ashirikiane na Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo pia wafadhili wetu hawa wa *Kopa Cocacola* ili waweze kuifanya timu hii ya vijana wawe katika eneo moja ambalo itakuwa rahisi Serikali kuwafuatilia kwa maendeleo haya ya mpira ili kwa siku zijazo ikawa ni timu nzuri ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wangu wa Manispaa ya Iringa ambao wamenisababisha niwe hapa leo lakini kwa dua zao njema zilizosababisha nikawa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma na kwa dua ambazo zinaendelea katika kunifanya niweze kufanya kazi zote mbili za Ubunge pale Manispaa lakini pia za Ukuu wa Mkoa, nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba niende kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, naomba niseme tu kwanza naiunga mkono kwa asilimia mia moja na naomba

nijikite katika ukurasa 18 wa malengo ya mwaka 2008/2009 naomba ninukuu kidogo katika sehemu (a) na (b) ambapo Mheshimiwa Waziri anasema kwamba katika kipindi kinachokuja Wizara itaendelea kusimamia Sera ya Taifa ya Ajira na Mkakati wa Taifa wa Kukuza Ajira lakini pia kuweka Mfumo wa Kitaasisi wa Kutekeleza Sera ya Kitaifa, Ajira ikiwemo kuanzisha dawati la ajira katika ngazi ya Mkoa na Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kutoa pongezi nyingi sana kwa sababu dawati hili la ajira katika Wilaya na Mkoa litasaidia sana kuweza kutambua ajira ngapi zinapatikana. Tukichukua Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi naomba ninukuu katika ukurasa wake 68 inapotoa aina za ajira inatoa katika eneo la kwanza inasema ni ajira zile rasmi lakini pili ni ajira kwa maana ya kujiajiri binafsi.

Naomba nijikite katika ajira binafsi ambazo wananchi wetu wengi ndio wako huko kwamba ukiwa katika kilimo hiyo ni ajira, ukiwa katika ufugaji, uvuvi, viwanda, biashara, kuchimba madini, udereva, ufundi, ualimu, uhasibu, kuendesha migahawa, ushonaji, uhandisi, uanasheria, uhandisi ukandarasi na kadhalika mtu akiwa katika shughuli hizi ambazo ni shughuli binafsi basi ajione kwamba yuko katika ajira. Lakini sasa hivi wananchi wetu wengine ni wakulima ukiwaambia anafanya shughuli gani anakwambia mimi sina ajira yoyote kwa sababu hajui maana ya ajira kwamba ni kitu halali anachokifanya ambacho kinachompa mtu riziki. Kwa hivi kupitia deski hili ambalo litakuwa katika Mkoa na Wilaya ninajua litatoa sasa elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara hii ituwekee wataalamu wa kutosha. Kwa sababu mpaka sasa hivi deski ambalo linashughulikia vijana limekuwa ndani ya Maendeleo ya Jamii kule kwenye Halmalshauri. Kwa hivi hata hii mikopo ya JK ilipokuja ilisimamiwa na vijana hawa ambao wanatoka katika Maendeleo ya Jamii. Kwa hivi kwa maana ya ile kukuza ajira unakuta wale wako ndani ya kitu kingine.

Sasa kama wako ndani ya kitu kingine kwa kweli inakuwa si rahisi sana. Kwa hivi naomba sana kwamba Wizara hii basi ipate wataalamu ambao watakuwepo kule ambao kazi yao itakuwa ni kujikita kuhakikisha kwamba wanatambua kwamba ni ajira kiasi gani zinapatikana ili waweze kuweka kumbukumbu lakini wanatoa elimu kwa wananchi ili waweze wengi zaidi kuingia katika ajira hii binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukichukua kwamba lengo la fedha za Mheshimiwa Rais zinajulikana rasmi kwamba za JK lilikuwa kwa kweli ni kumsaidia mwananchi wetu aweze kuondokana na umaskini, ndio lengo kubwa. Lakini unakuta kwamba waliopata fedha hizi ni wachache na kwa maana hiyo lengo lile ambalo lilikuwepo toka mwanzo naona kidogo lina walakini kwa maana ule utaratibu uliofanyika mara ya kwanza wa kupitisha fedha Benki ambao sioni kama ni ubaya ni sawa kabisa fedha zile zimepita Benki. Lakini kupitisha katika *SACCOS* kwa maana vijana wanatakiwa wawe katika *SACCOS* sasa utaratibu wa *SACCOS* ndio huu ambao kwa kweli naona kidogo una matatizo. Kwa sababu utaratibu wa *SACCOS* nakubaliana kabisa kwamba ni mzuri na pengine fedha hizo zinazokuja tena zipitie huko kwenye *SACCOS* lakini ni wangapi ambao wako katika *SACCOS* ni watu wachache. Kwa sababu utaratibu wa *SACCOS* unampata mtu wa katikati, haumpati yule mtu wa chini ambaye kwa kweli ndio lengo la

Serikali la kumkwamua mwananchi wa chini ili na yeye aweze kuwa na hali nzuri kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, anapokuwa na hali nzuri kiuchumi mwenyewe maana yake anabadilisha maisha yake, anakuwa na maisha mazuri lakini pia anachangia katika kuongeza Pato la Taifa. Lakini utaratibu wa mwanzo umemwacha kabisa mwananchi huyu wa chini. Kwa sababu *SACCOS* inatakiwa uwe na kiingilio, uwe na hisa, uwe na amana na uwe na akiba, mwananchi wa chini si rahisi kuwa na hivi vitu. Sasa mimi nasema ili hizi ajira ziweze kupatikana na ajira binafsi hizi mtu aseme mimi ni mkulima niko katika kikundi naweza kupata mkopo wa pembejeo, kupitia katika kikundi changu. Maana yake yupo katika kikundi anapata mkopo. *(Makofi)*

Lakini kwa sababu hana uwezo wa kuingia kwenye *SACCOS* maana yake mkulima hakuweza kufanikiwa katika kipindi kilichopita kuweza kupata mkopo wa Rais. Sasa sidhani kama lilikuwa lengo ni Serikali. Lengo la Serikali ni kumkwamua mwananchi aweze kupata maisha bora kama ambavyo Ilani ya Chama cha Mapinduzi ilisema kwa ajili ya uchaguzi wa mwaka 2005. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwamba ili shughuli hizi binafsi zikaweza kukua na ajira nyingi zikapatikane pale, mpango huu wa fedha za Mheshimiwa Rais katika awamu iliyofuatia naomba zikapitie Benki kule kule sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sasa ziende kwenye *SACCOS* lakini zipitilize pia ziende katika vikundi vya kiuchumi vilivyoundwa na wananchi wetu katika majimbo yetu ambavyo tunavijua viko vingi kabisa lakini vinashindwa kupata mikopo hii kwa sababu Hazina havina sifa ile ya *SACCOS* zile zinazotambulika. Wengine wanajiita ni *SACCOS* lakini kumbe hawana sifa kwa sababu sifa ya *SACCOS* kwa kupitia sheria ile ya Ushirika kweli utaratibu wake ni mgumu sana na mimi kupitia Manispaa ya Iringa vijana wengi sana walijiingiza katika mpango huu wa *SACCOS* lakini mpaka sasa hivi hawajaweza kujiita *SACCOS* bali ni vikundi. Sasa kama tutafika kupitia Benki na zikaweza kutambua vikundi hivi ambavyo kwa kweli wanafanya kazi nzuri tu ya kuweza kukopeshana na kuweza kubadisha maisha yao na wakaweza kufanya shughuli zisizo rasmi na baadae zikawa rasmi. Maana kama ni kikundi mle ndani wakakopeshana na mmoja akakua na akafikia mahali ambapo anaweza akatoa ajira basi tena na yeye anaweza akaingia katika ajira iliyo rasmi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba sana tena sana kwamba lengo la Mheshimiwa Rais lilikuwa zuri la kuwakwamua wananchi wake wote lakini utaratibu wa kwanza haukuwapata watu wote. Bahati mbaya utaratibu wa sasa hivi fedha zilizokuja katika awamu ya pili, lakini zinapitia katika *SACCOS,* lakini Benki ambazo zimeteuliwa kwa mfano mimi katika Jimbo langu la Iringa ni *Postal Bank* hawakupata kwa hiyo, fedha hizi zimekwenda vijijini. Sasa sisi wananchi wangu wa Mjini Iringa hawapati fedha hizi katika awamu ya pili ambapo tumepiga kelele la mgambo kubwa kabisa tukisema tusubiri maana ile ya kwanza tuliwapa lugha nzuri kwamba utaratibu huu kidogo haukuwa mzuri kwenu basi subirini awamu ya pili.

Sasa awamu hii kila nikiulizwa pale Manispaa ya Iringa nikiangalia *Postal Bank* kwa Manispaa hawana. Kwa hiyo, wanapeleka *Postal Bank* katika vijiji. Sasa wananchi

wa Manispaa mara nyingi wananchi wa mijini wale ambao hawana uwezo ni wengi sana. Kuna namna fulani tunaweza kusema ni *miss conception.* Wanadhani kwamba kila mtu aliopo mjini ana uwezo. Mimi naomba niseme kwa Manispaa ya Iringa si kila mtu ana uwezo. Wengi hawana uwezo na ningependa kweli wapate uwezo sasa na wanapenda, wanaingia katika vikundi sasa wanaghairi namna ya kupata mikopo hii. Lakini kama ingekuwa utaratibu huu unaruhusu basi wangeweza kupata mikopo hii. Sasa mimi naomba kwamba kwa utaratibu unaokuja basi vikundi hivi viwezeshwe kupitia huko Benki ili wafanye kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba nishauri kwamba inawezekana namna ya kuviunda vikundi hivi haueleweki. Naomba Wizara hii ambayo ni Wizara ya Vijana, ikishirikiana na Wizara nyingine yoyote ambayo ikiona inafaa lakini pia kwa kupitia Benki Kuu, naomba waende Mkoa wa Ruvuma ambako wameanzisha Vikoba katika Manispaa ya Songea na muasisi wake ni Mheshimiwa Devota Likokola ambapo utaratibu wa Vikoba ni mzuri sana na unawachukua watu wa chini na kuwaweka watu wa chini mahali ambapo wanachanga kutokana na uwezo wao mdogo na mwisho wanakopesha.

Mimi mwaka 2005 nilimchukua mtaalam kutoka Songea na nikamleta katika Manispaa ya Iringa na aliweze kufundisha katika Kata moja ambapo mwezi uliopita nilipita pale Iringa katika Kata ya Kitwiru, vikundi saba vya Vikoba vina jumla ya shilingi milioni 69. *(Makofi)*

Sasa kitu kama hiki ni kikubwa, lakini kwa kikundi kimoja kimoja hakijaitwa *SACCOS* kwa sababu utaratibu wa *SACCOS* upo tofauti na ukitaka kukaa nao uweze kutengeneza *SACCOS* unapata kitu ambacho hakiwezekani. Lakini kwa kuitwa tu Vikoba wanamtaji mkubwa, waajabu na ambao unawasaidia na sasa hivi tunasema tupate utaalamu zaidi wa kujiunga zaidi waanzishe Benki ya Wananchi na inawezekana kabisa. Kwa hiyo, mimi naomba utaratibu huu ambao ni mdogo ambao umeanzishwa tu na mtu lakini unaleta manufaa makubwa na pale Songea mimi nimeona unakwenda vizuri kabisa na nadhani mnakumbuka wiki mbili uliopita umeingia katika Jimbo la Mheshimiwa Aloyce Kimaro. Tumeona wananchi wengi wameingia katika mpango wa Vikoba na wameukubali na fedha nyingi wameweza kuchanga na wameweza kuchanga na wanaendelea kukopeshana bila matatizo yoyote. *(Makofi)*

Kwa hiyo, wale wanapata ajira kwa jinsi watakavyokuwa wanafanya kazi maana yake watajikwamua kiuchumi. Sasa ni mpango mdogo ulioanzia Songea lakini mimi sioni sababu kwa nini tusiuchukue na Serikali ikatuma wataalamu wake wakaenda kujifunza, waone wanavyoweza kuuboresha na wakaueneza Tanzania nzima kwa sababu una lengo la kumkwamua mwananchi wa chini. *SACCOS* mimi nakubaliana nazo lakini zinampata mtu wa kati, hazimpati mtu wa chini mwenye kuchanga shilingi mia tano au shilingi elfu moja. Lakini kwa Vikoba utaratibu wake ni mzuri sana, mwenye shilingi mia tano au elfu moja unampata anachanga na anayekuwa mwanachama na halafu mpango wa vikoba unakitu kinaitwa akiba ya maafa, kwamba mwenzako anapokuwa anaumwa basi wanampa mchango ili aweze kujitibia. Kwa sababu tunaona kwamba wengi wanashindwa kuendesha shughuli zao na wengi wanashindwa kurejesha mikopo kwa

sababu anapokuwa anauma au amefiwa au ana sherehe anachukua mtaji na hivyo anafilisika na mwisho anashindwa kurejesha mkopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kupitia Vikoba wana akiba zinazoitwa za maafa. Kwa hiyo, mwenzao akiugua wanampa, mwenzao akifiwa wanampa pesa. Kwa hiyo, ni tofauti na ule ule mpango wa *SACCOS*. Kwa hiyo, naomba Wizara hii ikaone utaratibu huu mzuri watafute wataalam waende Songea wakajifunze ili uenee Tanzania nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba niseme naunga mkono na ahsante sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MHE. ANNA R. LUPEMBE**: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuweza kunipa nafasi kwa siku hii ya leo kuweza na mimi kuchangia hotuba ya Wizara hii. Kwanza kabisa naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametupa uhai kuwa wazima mpaka sasa hivi. Pili, naomba kutoa rambirambi zangu kwa Mheshimiwa Savelina Mwijage, kwa msiba mkubwa aliyoupata na vile vile yule alikuwa ni mtoto wetu, Mungu amlaze mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa kazi nzuri ambazo wanazifanya siku hadi siku. Waziri naomba nikupongeze sana. Naomba nimpongeze Mkurugenzi Mkuu wa *NSSF* kwa kazi nzuri ambazo anazifanya siku hadi siku. Kwa kusema kweli Mkurugenzi huyu anatakiwa apate pongezi kubwa sana kwa ajili hali tunayoiona siku hadi siku ni kubwa sana lakini mimi nashangaa kitu kimoja, sijui Serikali ina kigugumizi gani kuwapa nafasi waweze kujenga lile daraja la Kigamboni kwa sababu kazi yao ni nzuri na kwa muda mfupi tumeona sisi wenyewe kazi walioyoifanya kwa muda mfupi ya Chuo Kikuu cha Dodoma, ni kazi nzuri sana na ni kubwa. Sasa sijui Serikali inaona kigugumizi gani kuwaachia *NSSF* waweze kujenga lile daraja kwa mara moja. Naomba vile vile nitoe pongezi kwa Mkurugenzi wa *PPF* naye kwa kazi nzuri anazozifanya. Kusema kweli wanafanya kazi nzuri sana ambazo zinazidi kuongeza Taifa letu kwa mambo kukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kabisa nianze na mambo ya *SACCOS* vijijini. Kweli tunampongeza Rais kwa mpango wake mzuri ambao ameuanzisha kwa kusema kuwa wananchi wa vijijini waweze kuboresheka. Lakini naona mipangilio hatukuipanga vizuri. Sisi watu wa mijini tuna uelewa kidogo lakini watu wa vijijini hawana uelewa. Kwanza kabisa ilitakiwa kazi ya kufanya ni uhamasishaji na elimu ili huyu mtu wa kijijini ajue maana ya mkopo ni nini, anakwenda kukopa wapi na kwa sababu gani na nia gani. Ili akikopa ajue afanyeje ile hela aitumie kwa kuifanyia nini. Huyu mwananchi wa kijiji haelewi kitu chochote kinachondelea, anasikia tu pesa za JK nendeni benki mkakope akienda mara moja au mara mbili, akirudishwa anaanza kusema mbona mikopo yenyewe wanatubabaisha tu.

Lakini kama wangekuwa na elimu ya kuwapa wale wana vijiji hamasa kubwa nafikiri tungepa mafanikio makubwa sana. Maana una mwambia nenda ukajiunge kwenye *SACCOS* mtu wa kijijini anasubiri kulima tu akipata mazao yake alime ile pesa

anajua ile fedha anaifunga vifungu vingapi achukue apeleke shuleni afanye hivi. Hawezi kusema ajue, aende akapeleke hela na kuweka amana, sijui nini kwanza anaona unamwongezea mzigo mkubwa badala ya kumpa manufaa ya kwake yeye mwenyewe kujitegemea. Yeye anaona ni mzigo kwa ajili anaona amana ni shilingi 10,000/=, akiba shilingi 10,000/= jumla inaweza ikafika shilingi 50,000/=.

Sasa anauliza hii shilingi 50,000/= kwa nini niipeleke kwenye *SACCOS*. Lakini kungekuwa na elimu na hamasa kubwa ya kuwaelimisha hawa watu na tuweze kujua nafikiri tungepata manufaa makubwa sana wala tusingepata matatizo sasa hivi. Ukiangalia na benki zetu kama nilivyosema mara ya kwanza kabisa benki kumjua mkulima ni nani maana akijua akimpa mkulima hela pesa zake haziwezi kurudi. Kwa sababu anajua huyu ni mtu wa msimu mtu, atalima, wakati wa mvua wakati mwingine mvua ikikataa hapati mazao au mvua ikizidi hapati mazao ndiyo maana haoni sababu ya kumpa mkopo. Ndiyo maana tunasema mabenki yote si rafiki wa mkulima au maskini. Mtu yeyote wa benki anajua yeye mfanyabiashara maana anajua atafanya biashara atapeleka pesa kurudisha katika mkopo aliokopa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunaiomba Serikali iangalie upya kutoa hamasa kwa wanavijiji hawa waweze kujua maana ya *SACCOS* ni nini ili waweze kukopesheka. Ukiangalia maafisa ushirika katika nchi hii ni wachache mno. Kama ukiangalia mkoa wa Rukwa maafisa ushirika sijui wako watatu, Wilaya ya Mpanda yupo mmoja, Sumbawanga Vijijini yupo mmoja na Wilaya ya Nkasi hakuna kabisa. Sasa unajua kabisa huyu Afisa Ushirika ambaye tuna mtegemea ambaye ndiyo Mtendaji Mkuu kabisa wa kuunganisha vikundi vya *SACCOS* na mtoa hamasa mkubwa sana katika shughuli za *SACCOS,* lakini hawapo au wachache.

Sasa kama Wilaya ya Mpanda ni kubwa jiografia yake mbaya yupo Afisa Ushirika mmoja na sisi pale tuna Halmashauri mbili ya Mjini na Wilayani. Sasa huyo huyo afanye mjini na wilayani. Ahamasishe vijana, ahamasishe akinamama atafanya kazi ngapi. Hamasa ni ndogo. Tunaiomba Serikali iwaongeze Maafisa Ushirika ili waende Mikoani kufanya hamasa upya ili hawa wananchi waweze kujikwamua kujua kukopa ni nini. Tatizo kujua kukopa ni nini ndiyo tatizo. Lakini ingekuwa hamasa ipo wala tusingepata taabu, sasa unakuta watu wachache ambao ni waelewa ambao wanaweza kukopa pesa hizo ambao wameingia *SACCOS* hizo ambazo tunazoziona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba niipongeze *SCULT*. *SCULT* imejitahidi sana kwenda mpaka vijijini kwenda kutoa mikopo kwenye *SACCOS* ambazo ziko hai. Lakini *NMB*, *CRDB* wamewapa wale *SACCOS* kubwa kubwa. *NMB* ndiyo wameshindwa na mkataba safari hii wamekataa kabisa kuingia kukopesha wananchi wadogo wadogo ambao ni maskini. *SCULT* ndiyo wamejikongoja wameingia vijijini kutoa mikopo kwa wale *SACCOS* ambazo ziko kidogo hai. Naomba tuwapongeze sana watu wa *SCULT* kwa kazi yao nzuri ambayo wanaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasema ajira kwa vijana lakini tunaona vijana wengi wanazurura mitaani, vijana wengi wapo vijiweni hawana shughuli ya kufanya. Unakuta kuna vijana mafundi baiskeli unakuta marundo kumi, mafundi pikipiki wamekaa kumi

ishirini. Lakini hata siku moja sijaona hamasa ya Serikali labda kuwafuata wale vijana kuwauliza mko wangapi, mnafanya shughuli gani, mnafanyaje fanyaje ili tujue jinsi gani ya kuweza kuwasaidia, hakuna. Wale vijana wanahangaika wenyewe, wanaajiri wenzao wanawavuta wanawaweka pale. Sasa unategemea huyu kijana atakuaje na wale tungezidi kuwaboresha wale vijana mafundi pikipiki na mafundi baiskeli wangezidi kuwavuta wenzao ili ajira kwa vijana ikawa kubwa. Lakini tunawaacha wajishughulikie wenyewe.

Tunaiomba Serikali wawatambue hawa mafundi ili kuwapa hamasa zaidi. Kuna mafundi seremala ambapo kuna vyuo vya *VETA* ambavyo vipo kwa ajili ya kuwafundisha useremala na fani nyingine. Lakini Serikali hata haiwafatilii wale wenye magereji kujua je, umeajiri watu wangapi unaweza kuajiri watu wangapi kutoka *VETA* ili hawa vijana wasiweze kuzurura ovyo wala kuvuta bangi. Lakini tunawaacha wala gereji hizi hatuzifuatilii na wala vikundi hivi vya mafundi vijana watuvifuatilii. Zile ni ajira tosha kwa vijana wala wasingeweza kuzurura mitaani ovyo na kuiba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ivijue na ivitambue hivi vikundi ili viweze kuinuka. Mimi naiomba niipongeze *SIDO*. *SIDO* wanajaribu siku hadi siku kuhamasisha vijana kubuni mbinu tofauti tofauti ili wapate ajira zao binafsi. Sasa tulikuwa tunaiomba Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana iangalie *SIDO* je, imehamasisha vijana wangapi na imewapa vifaa vijana wangapi ili kwa zike takwimu waweze kuelewa vijana wangapi wamepata ajira. Unajua uelewa bado hatujapata kwa sababu kila siku mtu kupata ajira labda ofisini ndiyo anajua ameajiriwa. Lakini hata hizi za kwenye baiskeli na vikundi mbalimbali nazo ni ajira watu hawata zurura ovyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwa leo sina mengi ya kuzungumza naomba niunge mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya muda uliopo hauwezi kumtosha. Sasa asubuhi Mheshimiwa Kabwe Zitto, aliniandika akiwa na mashaka kwamba nafasi aliyopewa Mheshimiwa John Malecela, asubuhi kutoa maelezo yale binafsi pengine ilikuwa si sawa kwamba ingepaswa labda kuwa baada ya *adjoining motion*. Sasa nilitoa maelezo kwamba hizi Kanuni ziko mbili tofauti. Kanuni aliyoitumia Mheshimiwa John Malecela ni Kanuni ya 50(1) ambayo inasema; "Maelezo binafsi ya Wabunge. Kifungu cha kwanza kinasema; "Mbunge yeyote anaweza kwa idhini ya Spika kutoa maelezo binafsi Bungeni yanayolenga kufafanua kuhusu jambo lolote linalomhusu na lililoifikia jamii." Sasa kama alivyosema tuchangie ile taarifa ya Kamati ya Madini magazeti fulani fulani yakaandika kwamba Mzee huyu alikuwa anataka kuiumbua Serikali ya Kikwete, kwa hiyo, alikuwa na nafasi hiyo.

Kwa hiyo, hilo linatokea mara baada ya maswali kama kauli za Mawaziri hazipo. Sasa Kanuni aliyokuwa anai-*refer* Mheshimiwa Kabwe Zitto ni Kanuni ya 28(1)(11) yenyewe inasema. "Bila ya kuathiri masharti ya Kanuni hii wakati Spika anapotaka kuahirisha Bunge wakati huo unaweza kutumiwa kama fursa kwa Mbunge yeyote kutaka ufafanuzi utolewe juu ya jambo lolote lililo chini ya madaraka ya Waziri huyo au kuanzisha mjadala juu ya jambo lolote la dharura kwa idhini ya Spika isipokuwa kwa

jambo ambalo haliwezi kujadiliwa bila hoja maalum kutolewa kwanza kwa ajili hiyo.” *(Makofi)*

Kwa hiyo, mnaona kwamba hapa ile ya kuuliza kabla ya kuahirisha kikao cha Bunge inailenga Serikali inawezekan kwa jambo lililotokea humu ndani au tamshi lililotolewa na Serikali mahali fulani. Kwa hiyo, Mbunge yeyote anaweza kusimama wakati huo na wakati huo kama nimekaa hapa na kama nimepewa taarifa hiyo nitamwita Waziri Nchi anayehusika na masuala ya Nchi atoe hoja ya kuahirisha kikao. Akishatoa hoja ya kuahirisha kikao, mimi namwita yule Mbunge anayehusika na yeye atatumia sio chini ya dakika thelathini. Kwa hiyo, ndiyo tofauti ya kifungu hiki na kile. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nimeagizwa pia ingawa itatangazwa jioni kwa sababu Wabunge wapo wachache kwamba Kocha Msaidizi wa *Bunge Sports Club* anasema ile mechi kati ya Bunge na *NSSF* haitakuwepo kesho kwa hiyo, anawaomba radhi waliodhurika na mambo haya. Kwa hiyo, baada ya hapo nasitisha shughuli za Bunge mpaka jioni saa kumi na moja. *(Makofi)*

*(Saa 06.52 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

## HOJA ZA SERIKALI

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati wa mchana tuliwapa nafasi wenzetu ambao hawajachangia hata mara moja. Sasa tunaingia orodha ya waliochangia mara moja. Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya ataanza, Mheshimiwa Mhonga atafuatia, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, atafuatia, Mheshimiwa Maulida Komu, naye ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa mawazo yangu kuhusu hoja iliyo mbele yetu. La kwanza kabisa, ningependa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wake na wataalam wote kwa kazi nzuri na hotuba hii waliyotuandalia. Vile vile nataka niungane na wenzangu wengine waliotangulia kueleza namna wanavyoridhika na mambo mazuri yanayofanywa na Wizara yenyewe pamoja na Wizara zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wengi waliotembelea miradi ambayo imesimamiwa na kuendelezwa na *NSSF* wanaridhika sana. Uongozi na utaalamu wa hili shirika ni imara sana na wanajali sana wajibu wao. Hata wananchi wanaochangia katika shirika hili hawawezi kusikitika kwa sababu linaongozwa vizuri na matunda yanaonekana, kwa hiyo, tunawapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, mimi nataka kusema na hili siyo tu kwa Serikali ya CCM ambayo iko madarakani, lakini nataka hili niseme kwa faida ya Wabunge wote. Tanzania katika idadi ya watu zaidi ya milioni 36, asilimia kubwa ya idadi hiyo ni vijana wenye umri kati ya miaka 18 na 35, ndio walio wengi na wakati wa uchaguzi mtakumbuka jinsi makundi ya vijana katika uchaguzi wa mwaka 2000 yalivyoamka na kuonyesha msimamo na mwamko wa kiasiasa.

Kwa hiyo, ukitata kusema kweli unaweza ukasema sisi kama hatuhangaiki na kufanikisha shughuli za hawa vijana, wote tutakuwa tumekalia kuti la moto kwa sababu hawa ndio wengi na ndio wapiga kura na siku hizi vijana ni hodari sana katika kampeni, wanaweza hata wakavuruga mkutano wa uchaguzi, mimi nimeshuhudia, nimeona, na kilio chao ni kazi, ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nataka kutoa ushauri kwamba jambo hili tusiliseme kwa jumla, tunahitaji kuwa na mpango endelevu utakaotafsiri makundi haya kwa uwezo wao na mahala walipo. Kwa mfano, mimi natoka Rukwa, Rukwa na hata viongozi wote mmeshuhudia, hakuna hata kijana mmoja wa kutoka Mkoa wa Rukwa ambaye yuko Dar es Salaam anafanya biashara ya machinga, wale wamefundishwa uzalishaji, wako mashambani. Lakini hawawezi kulima na jembe la mkono sasa, kilimo endelevu ni *plau* na maksai. Hawa vijana wakipewa mikopo hii ya kilimo, watafanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ushauri wangu hapa ni kusema tupange makundi haya kwa namna yalivyo. Kwa mfano, vijijini tungetengeneza mipango itakayosaidia kukuza uzalishaji mali katika kilimo na nguvu kazi ni vijana. Nitatoa mfano mzuri, wakati wa uhai wa Mheshimiwa Baba Yetu wa Taifa, Marehemu Julius Kambarage Nyerere, dhamira na nia ya kuanzisha vijiji wakati ule, ilikuwa ni kuwa na mahala ambapo watu wamekaa wanaweza wakapata huduma za kijamii, lakini vile vile wakawa na mipango ya kiuchumi inayoeleweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tuna vijiji ambavyo vingine vina familia 2000 mpaka 3000. Unaweza ukakuta kijiji kina watu wenye uwezo wa kufanya kazi 3000/4000. Lakini hawa wako wenyewe tu, hawana wataalam wa kuwaongoza. Lakini kiwanda kikijengwa na kimeajiri watu 200 au 300 tu, kitakuwa na mameneja na watalaam msululu. Lakini kijiji chenye watu 4000 wenye uwezo wa kufanya kazi, hakina hata mtu wa kuandika *minutes*, hata ma-*VEO* wenyewe tumewaweka hawajakwenda shule wengine. Tunawezaje kukabidhi nguvu kazi 4000 kwa *VEO* ambaye hawezi kuandika hata muhtasari? *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi ninachoshauri hapa, nataka sasa tuanze kufikiria namna ya kupeleka madaraka vijijini lakini kwa maendeleo ya kupeleka watu angalau hata ngazi ya Kata, kwamba kila Kata iwe na Afisa Mchumi, iwe na Bwana Shamba mzuri, kuwe na timu, sekretarieti ya wataalam katika ngazi ya Kata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii habari ya kuzungumza mambo ya vikundi, sijui vitakopa ni ndoto tu, watakopaje hawawezi kuandika mradi na Benki wanataka miradi iliyoandikwa! Sasa hawa wanavijiji ambao wanaongozwa na *VEO,* wanaandikaje mradi

wa kuweza kukopa mamilioni ya fedha? Kwa hiyo, nashauri Serikali turudi kwenye vijiji ndio tukaanzie na kwa sababu nchi ni kubwa, tuchukue Kata kama ndio msingi wa maendeleo ya vijiji katika maeneo yetu, na itawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, mijini. Wakati wa nguvu kazi, Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu wa sasa alikuwa Katibu Msaidizi wa Rais, Mwalimu Julius Nyerere wakati ule. Mimi nilikuwa Mkuu wa Mkoa, tukaambiwa tuanzishe nguvu kazi, baadhi ya Mikoa ikiwemo Dar es Salaam walianza kukamata vijana na kuwarudisha kwao kwa kusema hawana kazi Dar es Salaam. Mimi nikaenda Ikulu nikamwambia mwambieni Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam wakati ule Marehemu Mhaville, aniletee watu wote wanaotoka Morogoro awarudishe kwangu mimi nitawapokea na kazi nitawapa, kwa sababu mtawala mwenye akili ni watu! Utaendeshaje nchi wakati huna watu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati ule tulikuwa na ugomvi wa kutafsiri kazi halali, mimi pale Morogoro nikasema, akinamama mnaopika vitumbua ni halali, mke wa ndani aliyeolewa ni halali na ni kazi. Kuolewa kwenyewe na kuchunga watoto ni kazi, kwa sababu zilianza kampeni za kuvuruga watu, kamata watu peleka kwao! Sasa unawapeleka wakafanye nini kule! Mtu amezaliwa Dar es Salaam, amekulia Dar es Salaam, unampeleka Sumbawanga akafanye nini! Pili, watu wanaopiga brashi, mimi niliwasajili, nikamwambia Afisa Mipango wa Morogoro, wapiga viatu wote muwasajili, ni kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninachotaka kusema hapa, kazi halali ni kazi inayompa mtu riziki yake japo hata ni ndogo. Kwa hiyo, hata mijini lazima tuwajue hawa vijana, wafanyabiashara tuwatambue, katika uzalishaji mali tuwatambue ili mipango yetu endelevu ilenge makundi ambayo tunayajua. Kwa mfano; tukiuliza swali Wizara hii ya wenzetu walioleta hoja hapa, tukiwauliza swali, mna idadi ya vijana kwa maana ya mpango huu? Watasema hawana! Kwa hiyo, mimi nazungumzia idadi ya mpango wa maendeleo, mpango endelevu wa ajira kwa hawa vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, twende kwa wasomi. Zamani mtu akimaliza Chuo Kikuu alikuwa ana uhakika ameajiriwa. Leo hapana! Kwa hiyo, vile vile *atitude, mind set* yetu ibadilike kwamba anasoma mtu ajiajiri, lakini lazima kuwe na mpango. *(Makofi)*

Kwa mfano, tuna vijana pale *Sokoine University*, lazima tuwajue wangapi wataingia Serikalini na wangapi watakwenda kujitegemea ili siku anapotoka pale Sokoine ana zana za kwenda kuanzisha utaalam wake. Atakuwa *Consultant*, Bwana ng'ombe, wafugaji wa Sumbawanga, watakwenda pale atatibu mifugo yao, atafanya *extension*, watampa hela, atapata posho, anaweza akafungua kaduka kake ka dawa ka kuuzia wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikwenda zamani Egypt, kule walikuwa na mpango, wale mabwana shamba, wale vijana wanaosoma, anajua kabisa akimaliza atapewa mtaji wa kwenda kuanza kilimo katika eneo lenye *irrigation*. Anapewa heka nne tu. Heka nne atavuna mara mbili. Kwa mfano, nilikuwa nazungumza na wataalam wangu juzi, tulikuwa tumepeleka vijana wetu waende wakajifunze kilimo kule Malaysia. Malaysia

sasa, kwa hekta moja wanavuna mara mbili, kila vuno la kwanza ni tani 11 kwa hekta. Kwa hiyo, kwa mwaka kwa sababu wanalima mara mbili, wanavuna tani 22 kwa hekta moja, sisi Mbarali kwenye *irrigation* tunavuna tani tatu kwa hekta. Sasa huu ni utani!

Kwa hiyo, mimi nataka tuzungumzie ajira ambayo ina rasilimali inayojulikana. Mimi mtu angeniuliza, ningesema tufanye mipango ya kuongeza kuwa na miradi ya uzalishaji mali, lakini kila watu kwa fani yao waliyosomea. Huo ndio ungekuwa ushauri wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, natoa wito hapa kwamba tuandae mipango kwa ajili ya hawa vijana kwa sababu tusipojiandaa sasa watatusumbua. Hata hivyo, ningependa vile vile, Mheshimiwa Rais wetu na chama chetu wakati wa uchaguzi wa mwaka 2005 alitoa ahadi na hii iko katika Ilani ya CCM kwamba kwa miaka 10 ijayo Serikali yetu itaweka ajira milioni moja. Sasa hivi tumekwishafikisha ajira ya watu 437,000 kwa awamu ya kwanza ya miaka mitano. Mimi nataka kuipongeza Serikali kwa mafanikio hayo, ni mafanikio makubwa sana tena ya kujivunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, mikopo hii inayotolewa mimi napongeza mafanikio ni makubwa sana, lakini inavyoonekana tafsiri ya wataalam wetu imekuwa finyu. Wao wakizungumzia wajasiriamali, maana yake ni wafanya biashara ndogo ndogo! Kule kwetu katika Mkoa wa Rukwa, wakulima wamejiona kama ni wanyonge maana hawapewi mikopo ya kilimo kwa sababu wanasema hizi pesa tumeleta ni za wajasiriamali. Wajasiriamali ni wachuuzi wanaonunua mahindi ambayo hawakulima. Sasa hiyo, mimi naona ni jambo ambalo lingefaa tulirekebishe ili lengo liwe ni kuongeza uzalishaji zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ambalo ningependa kumalizia, mimi niliingia Bungeni, nilikuwa na umri wa miaka 25 na sasa mimi ni mzee. Wakati ule tulipoingia sisi Bunge, hatukuwa hata na Daktari, hatukuwa na Daktari kwa maana ya usomi. Tulikuwa na watu wa *University* na watu wenye elimu ya sekondari wachache pia na wakati ule ni *degree* moja moja! Leo hiki chumba kimejaa Maprofesa, Madaktari na wasomi, taja fani yoyote, wako humu. Kwa hiyo, jamii inategemea pia kiwango cha uwakilishi katika Bunge hili kiwe cha juu pia na mambo tunayoleta humu Bungeni yafanane na Bunge lenye watu wenye uwezo hivyo hivyo. Mimi mngeniuliza, naweza nikasema naona kama kidogo viwango vinaanza kushuka na inaweza kushuka kwa sababu gani, mara nyingine tunang'ang'ania sana mambo yanayohusu watu binafsi kuliko mambo ya msingi ya kuleta maendeleo kwa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kanuni hizi tulizonazo, zinalinda pia raia kwamba tunapokuja Bungeni tusiwatuhumu watu ambao hawana uwezo na haki ya kuja kujitetea humu! Watakuja kujiteteaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka nitoe tahadhari kwamba heshima ya Bunge hili ni kuwatetea Watanzania na kulinda heshima ya Watanzania waliotuchagua. Lakini ikiwa Bunge litageuka kuwa la watu ambao kila wakisimama wanawatuhumu wananchi, wapiga kura ambao hawana nguvu ya kuja katika Bunge hili, tunaharibu

heshima ya Bunge na mifano tunaiona, leo katika magazeti yanavyoandika juu ya mambo yetu, watu wa Tanzania wakisoma hawaelewi Bunge limekuja kufanya nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mambo mengi ya maendeleo ya kufanya, nitatoa mfano mmoja, kama mtu kwa mfano, ameingia mkataba na Mzindakaya, Watanzania wengi wanakwenda kwenye taasisi mbalimbali kukopa, hivi kila aliyekwenda kukopa akipatana na riba itakuwa ajenda ndani ya Bunge? Lazima tupime jamani! Watu wote waliokopa, sasa tutakuja kubishana humu, huyu alikopa, riba kubwa, huyu ndogo. Hivi walikokuwa wanakopana kule na kusainiana riba tulikuwepo sisi Wabunge! Wewe umechukua mkopo kwa hiari yako, utageuzaje kusema huyu ni mnyonyaji aliyekukopesha, si uliandika mwenyewe mkataba! Kwa nini tunataka kubadilisha kazi ya Bunge kuwa kazi ambayo hatukutumwa sisi hapa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka kutoa angalizo hilo na nataka niseme, Kifungu cha 71 cha Kanuni zetu na hii Mheshimiwa Spika, aliing'ang'ania sana iwepo na sisi tukakubali, inasema hivi, naomba kunukuu: "Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 na 101 ya Katiba, mtu yeyote asiye Mbunge ambaye atajisikia kuwa amepata athari hasa kutokana na kauli au maneno au shutuma zilizotolewa Bungeni, atakuwa na haki ya kuweza kulalamika na kupeleka kwa maandishi kwa Spika."

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Bunge lisiwe mgomvi na raia wapiga kura. Bunge linatakiwa kuwa rafiki na mpenzi wa wapiga kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nataka vile vile niseme, mimi nakuunga mkono, unafanya kazi yako vizuri ya Unaibu Spika. Spika wetu anaongoza Bunge vizuri, lakini duniani, mimi ni Mkristo, Yesu alisulubiwa pia msalabani, Spika anajitahidi kuongoza vizuri Bunge, lakini ukiona inavyoandikwa, utafikiri kama sisi Wabunge tulichagua mtu hivi hivi tu. Lakini Spika, anajitahidi, tulimpigia kura sisi, lazima tulinde heshima ya Spika wetu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, naunga mkono hoja! *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Kifungu alichosema Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, ni sahihi. Lakini ni sahihi pia kwa Waheshimiwa Wabunge, tunapoongea hapa tunalitangazia siyo Bunge tu, ulimwengu. Kwa hiyo, mtu anapotoa maneno yake, ni lazima awe na uhakika ndio maana kuna kanuni nyingi hapa zinatutaka kabisa tuwe na uhakika na jambo tunalolisema, kwa sababu hata kama tuna *immunity*, lakini pia tunatakiwa kuwajibika. Kwa hiyo, ninadhani ni kauli. *(Makofi)*

Kuna Waheshimiwa Wabunge wengine wanasema siku moja wewe Spika, utakuwa peke yako. Bahati nzuri hawakuandika hata majina. Kwamba siku moja Mheshimiwa Spika, utakuwa peke yako. Anasema siku moja ukija hapa unakuta wewe mwenyewe unahutubia tu peke yako tu. *(Kicheko)*

Jamani, Kanuni ya 77 inasema uhalali wa shughuli. Akidi kwa kila kikao cha Bunge wakati wa kufanya maamuzi, naomba nirudie, wakati wa kufanya maamuzi

itakuwa ni nusu ya Wabunge wote. Kwa hiyo, hivi sasa hivi, haisumbui. Kwa mfano, leo tungekuwa tumefika, tunaingia Kamati ya Matumizi, tusingekubali, ingebidi tupige kengere, kama haitoshi, basi tunaahirisha. Lakini kuwasikiliza Waheshimiwa wanasema, hii bado haizuru kufanya maamuzi na mwingine anasema anaona Serikalini. Serikali ipo! Tukifanya maamuzi, tutapiga kengere. Kama hawatatokea watu idadi inayotakiwa basi inabidi tungoje tena siku nyingine. Lakini kwa hivi sasa tunatosha! *(Makofi)*

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi na mimi kuchangia jioni hii ya leo katika hoja iliyoko mbele yetu, hoja ya Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nitoe pole kwa Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Savelina Mwijage kwa msiba alioupata kwa kufiwa na mwanae pamoja na dereva wake walipokuwa wanaelekea Dar es Salaam asubuhi ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Waziri kwa taarifa yake nzuri. Pia nitoe pongezi kwa Naibu Waziri ambaye yuko katika matibabu sasa, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na wataalam wake pamoja na watendaji wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine katika kukamilisha taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ni nzuri na yenye matumaini makubwa kwa maendeleo ya Watanzania wote. Tegemeo letu ni utekelezaji kwa yale yote yaliyoainishwa ili kuleta maendeleo kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa juhudi zake za kusimamia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii *(NSSF), PPF* pamoja na mingine katika kusimamia masuala ya ujenzi wa majengo mbalimbali ndani ya nchi yetu yakiwemo yale mabweni matano ya Chuo Kikuu hapa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana kwa kuisimamia mifuko hiyo, pia naipongeza mifuko hiyo kwa kazi zake nzuri inazozifanya katika kuimarisha majengo ya Taifa hili. Bila shaka juhudi hizo zitaweza kukumbukwa kwa vile wanatuletea maendeleo ndani ya nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niongezee kwa kuchangia suala la kiwanja walchiomilikishwa Shirika la Tija la Taifa *(NIP)* ambacho walikabidhiwa tokea miaka ya 1980 na kupewa hatimiliki mwaka 1995. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ardhi iliwamilikisha kiwanja hiki Shirika la Tija la Taifa na kiwanja hicho baada ya kumilikishwa waliweza kujenga nyumba ndani ya kiwanja hicho ambayo iligharimu shilingi milioni 46 na wakati huo huo wakakiimarisha kwa kujenga uzio ambao pia uligharimu pesa nyingi na vile vile wakawa wanakiimarisha kiwanja hicho kwa sababu kilikuwa tayari ni cha kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la kusikitisha ni kuwa baada ya Chuo cha *IMTU* kupeleka maombi ya kutaka kiwanja Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya

Makazi, walikatisha haraka umilikishwaji huo na kuwaandikia barua Shirika la Tija la Taifa kuwa umebadilishwa umiliki huo. Lakini la kusikitisha ni kuwa Chuo cha *IMTU* baada ya kumilikishwa kiwanja hicho mwaka 2002 walitoa fedha za fidia shilingi milioni 15 tu wakati hata zile za nyumba hazikufika walizogharamia Shirika la Tija kujenga nyumba ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naliomba Bunge hili Tukufu likae pamoja na Waziri husika kulitatua suala hili. Suala hili ni mgogoro mkubwa ambao wamedhalilishwa kwa kiasi fulani Shirika hili la Tija la Taifa ambalo Shirika hili ni muhimu katika kuleta maendeleo ya Taifa hili. Ni vema mgogoro huu ukawekwa sawa ili kupatikana haki kama inavyostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nichangie suala la Fedha za Mifuko ya Vijana ambazo walipatiwa vijana kwa kipindi cha miaka kadhaa iliyopita, nafikiri kipindi cha mwaka 2002/2003, kitu kama hicho. Fedha hizo ni nyingi ambazo zilitolewa kwa mifuko hiyo kwa madhumuni ya kuwaendeleza vijana wa Taifa hili. Lakini hadi leo hii fedha zilizotolewa ni nyingi na zilizorudishwa ni chache mno! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iangalie vizuri namna ya kuzipata fedha hizi. Wadhamini ambao waliwadhamini *SACCOS* hizo katika kupata fedha hizo ni vizuri wakasimamiwa vizuri, fedha hizi zikarejeshwa kwa sababu wako vijana wengi ambao wanazisubiri fedha hizo na ambao hawakubahatika kipindi hicho kupata fedha hizo katika kujiendeleza kiuchumi. Namuomba Mheshimiwa Waziri kwa kushirikiana na timu yake aweze kusimamia vizuri fedha hizi ili ziweze kurudishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, tunakumbuka kuwa Bajeti ya mwaka 2006 ilitamka rasmi, Serikali kama Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwezesha shilingi bilioni moja kila Mkoa. Naiomba Serikali kuifuatilia vizuri mifuko hii ili kwenda moja kwa moja katika *SACCOS* husika kwa sababu vikundi mbalimbali ambavyo vimo ndani ya *SACCOS* hizi yaani mtu mmoja mmoja wanakuwa na utaratibu mgumu katika ujazaji wa fomu hadi kupata fedha zile. Ufuatiliaji hadi kuzipata fedha zile unakuwa ni mrefu. Ni vizuri fedha zile zikaenda moja kwa moja kama alivyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu katika Bajeti yake, ni vizuri fedha hizi zikaenda moja kwa moja katika *SACCOS* husika ili utaratibu ule uwe unafanywa na *SACCOS* husika na wao watawasimamia vikundi vyao kuwapa mikopo hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia ifuatilie Benki, fedha hizi zilizotolewa na Serikali, kweli zinawafikia walengwa? Kwa sababu, tumeangalia katika vikundi vingi, *SACCOS* nyingi hazijafaidika na mifuko hiyo. Wengi wanalalamika, tunasubiri, tunasubiri, lakini bado hawajafaidika. Ipo awamu ya kwanza, imepita, sasa hivi awamu ya pili na ya tatu, lakini, naiomba Serikali kulifuatilia kwa kina suala hili ili mifuko hii iweze kuwafikia walengwa vijana wetu waweze kufaidika kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niongelee suala la fedha zinazotolewa za mikopo kwa kiwango cha chini cha shilingi 50,000. Kiwango hiki bado ni kidogo kwa

sababu tukiangalia sasa hivi shilingi 50,000/= hujui ufanyie nini. Ukizichukua zile kama unakwenda kufanya mradi wowote, kwa kweli utaratibu wake haufiki pahali. Kwa hiyo, naiomba Serikali angalau kuongeza kima hiki cha chini ili vijana hawa waweze kufaidika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali pia kuweka mikakati ya taarifa ya urejeshwaji wa mifuko hii ili vijana au vikundi ambavyo havijafaidika na mifuko hii, waweze kufaidika mapema iwezekanavyo kabla ya mwaka 2010. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, naiomba Serikali iandae mafunzo ya ujasiriamali kwa *SACCOS* mbalimbali ambazo hazijapata mafunzo ya ujasiriamali. Ipo sera ya mafunzo ya ujasiriamali ambayo inawataka wajasiriamali wawe vipi, waanzishe vipi miradi yao. Ni vema Serikali ikawa inaliimarisha suala hili katika *SACCOS* zote kwa sababu mara nyingi fedha hizi wanazopewa vikundi hivi wanakuwa hawana utaalamu wa kuziendeleza.

Kwa maana hiyo, wanakuwa hawafiki pahali, yaani wanachukua muda mrefu kuingiza, pia wanachukua muda mrefu kurejesha fedha hizi na matokeo yake wanaweza wakawa wanasahau, matokeo yake fedha hizi zinakuwa hazirudishwi na kufaidika wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema Serikali ikaandaa mafunzo haya kwa wajasiriamali wote ili kuweza kufaidika na mafunzo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wangu wa Kaskazini Pemba wapo wana *SACCOS* mbalimbali ambao tuliwasaidia kwa njia moja au nyingine katika kuwapatia mafunzo haya ya ujasiriamali na sasa hivi zipo orodha nyingi tu ambazo wanasubiri mikopo hii, namwomba Mheshimiwa Waziri kwa kushirikiana na Waziri wa kule Zanzibar na Mkuu wa Mkoa pamoja na Halmashauri za kule kuweza kuviwezesha vikundi vile kwanza vilivyopata mafunzo ya ujasiriamali ili kuweza kufaidika kwanza, badala yake tutaendelea na mafunzo kwa wale wengine ambao hawajapata mafunzo haya kwa kusubiri wenzao baada ya kukamilika na wao kuweza kufaidika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema fedha hizi zikaenda moja kwa moja kwa wale ambao tayari wameshaanza mafunzo kuliko ambao hawajaanza mafunzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo kwa wamachinga ambao tumewaandalia jengo Mjini Dar es Salaam ambalo linajengwa na *NSSF*, ni vizuri tukaangalia kwanza kuwapatia mafunzo wamachinga hawa kabla hawajakabidhiwa jengo hilo wakapewa elimu kwanza ili kuweza kuwapa utaalamu wa kufanya biashara mbalimbali, ni vema Serikali ikalizingatia hili katika kuwaimarisha wajasiriamali hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naomba Serikali kuhamasisha *NSSF* kujenga majengo kama haya katika Mikoa mingine kwa sababu ipo mikoa mingi ambayo ipo tayari kujiendeleza kiuchumi lakini hawana misingi ya kuanzia wala hawana majengo ya kufanyia biashara kama hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu orodha ya waajiri ambao wameomba vibali kwa madhumuni ya kutoa ajira nchini, wapo waajiri ambao ni wazalendo na wapo waajiri ambao ni wageni, naomba kuishauri Serikali kwanza kuwapa vipaumbele waajiri ambao ni wazalendo katika kuwaangalia vijana wetu. Vile vile hawa wageni ambao wameomba vibali hivi ni vema kuwaangalia wageni hao ajira zao ni za namna gani ili wasije wakawadhalilisha vijana wetu, naiomba Serikali kwanza iwape vipaumbele wale walioomba vibali ambao ni wazalendo wan chi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la watumishi, maendeleo ya watumishi wetu bado ni duni, wengi hawajathibitishwa kazi, hawajapandishwa daraja, ajira bado hazijaendelea, lakini naishukuru Wizara au Serikali kwa kupanga ajira milioni moja bila shaka Mheshimiwa Waziri ataweza kulifuatilia kwa makini suala hili ili vijana wetu wa nchi hii ambao hawana ajira waweze kufaidika na ajira hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri pia watumishi uwekwe muda maalumu wa kuwapa elimu kuhusu UKIMWI, wafanyakazi wengi wanaathirika na wanaosababisha tatizo hilo ni wafanyakazi wenyewe kwa wenyewe badala yake unyanyapaa unakuwepo sehemu za kazi, naiomba Serikali kama kutakuwa na waathirika ndani ya Wizara basi waweze kuwapa elimu na kuwasaidia waathirika hao bila kufanyiwa unyanyapaa wa aina yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie pia vijiwe vya vijana, vijiwe vya vijana vipo vya aina mbili ninavyofahamu mimi, vipo vijiwe vya vijana ambavyo Wizara inaviendeleza na wamewapa kazi, mfano askari jamii na mambo mengineyo, lakini vipo vijiwe vya vijana ambao hawana mwelekeo yaani vijiwe tu vipo wanajikusanya kazi yao ni kuvuta bangi, dawa za kulevya, kuendeleza UKIMWI na mambo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vijiwe hivi tuvitambue, tuvitafute na kuviorodhesha kwa kuwapa mafunzo mbalimbali ambavyo wamejikusanya tu hawana kazi yoyote na ambao wengi ni vijana na wameshaathirika kisaikolojia, lazima Wizara iweze kuweka mkakati wa kuwasaidia kama vijana wa nchi hii ili kuondoa maambukizo zaidi ya UKIMWI na kuwaepusha na mambo mengine ambayo ni mabaya ndani ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika baada ya maelezo haya naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na namshukuru Mwenyezi Mungu kwa ajili ya siku hii ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake katika kushughulikia masuala mbalimbali ya Wizara yao hususani ya kusaidia kusuluhisha migogoro hasa ya ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba kwa kuwa Wizara hii ni Wizara mtambuka na nyeti sana, ni nyeti kwa sababu inagusa maisha ya watu, lakini Wizara hii

pia imekuwa na nguzo kupitia Wizara nyingine haiwezi kusimama yenyewe kama ilivyo, kwa hiyo, hata mchango wangu hautakuwa moja kwa moja kwenye Wizara peke yake kwa sababu hata sera ya ajira na vijana na maendeleo ya kazi inazungumzia wazi kwamba kuna Wizara ambazo zitasaidia katika kuhakikisha kwamba ajira zinapatikana na ndiyo maana nitajipa uhuru katika maeneo yale ambayo naona yanachangia kutokuwepo kwa ajira endelevu na ajira bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nianzie kumuuliza Mheshimiwa Waziri ametueleza kuna zaidi ya ajira laki nne ambazo tayari tumeshaziorodhesha, mimi nafurahi kwa sababu tunasogea, lakini swali langu la msingi ni kwamba ajira hizo ziko katika mafungu yapi kufuatana na ubora wake, kwa sababu ukiangalia hata katika kitabu ambacho tumepewa hapa, kinaonesha wazi kuhusu ujasiriamali mdogo mdogo, kuna kuku hapa nimewaona, kuna vijimkaa na vitu vingine, kwa hiyo, kimsingi katika kutafuta kipato cha kumwezesha mwananchi kuweza kukimu maisha yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu spika, lengo langu la kuzungumza hapa ni jinsi gani Wizara imejipanga katika ajira zile ambazo ni nyeti, ajira ambazo zinazalisha ajira nyingine kwa wingi na vile vile zinatumia teknolojia, nauliza hivyo kwa sababu kwanza nimefuatilia wakati ambapo pesa zinatolewa kwa ajili ya kuwasomesha wanafunzi ambao tunawalenga baadaye wawe katika soko la ajira na wale ambao watakuwa ni wafanyakazi bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiangalia kwa mfano katika upande wa marubani wa ndege, naomba nifahamu Tanzania hii tuna marubani wa ndege wangapi ambao wapo chini ya umri wa miaka 50, nauliza hivyo kwa sababu kuna vijana ambao wanachukua mafunzo ya urubani wanajilipia, lakini walipoenda kutafuta mikopo hawakuweza kusaidiwa na hiyo ni kuonesha kwamba kuna sekta ambazo zinakuwa hazijawezeshwa kuweza kupata wajuzi na nadhani hiyo ndiyo kikwazo kikubwa sana kinachofanya kwamba hata ukienda kwenye vyuo sasa hivi kati ya wale wahitimu wanaohitimu katika mafunzo ya sayansi na uhandisi ni wachahe sana tofauti ni kubwa sana. Kwa mfano, mwaka jana wakati wa *graduation* katika *Masters* ya Nishati, nakumbuka alikuwa ana-*graduate* mtu mmoja aliyefundishwa na profesa kwa muda mrefu kwa sababu hana wenzake. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu ni kwamba wale wanaohitimu wakisharudi kwenye maeneo yao au wanapotafuta kujiendeleza kunakuwa hakuna uwanja mpana, lakini ukiangalia kwa upande wa *MBA* kulikuwa na wanafunzi wengi sana matokeo yake sasa kunakuwa na mtu mmoja wa *profession* fulani kuwa katika nafasi ya kuweza kufanya kazi za kila *profession,* naomba sana Mheshimiwa Waziri unifahamishe kuna utaratibu gani wa kuendeleza marubani hasa ukizingatia kwamba nchi yetu ina shirika la ndege ambalo linahitaji kuendelea kukua kwa kutumia teknolojia ya kisasa na hivi itahitaji marubani ambao wana ujuzi kufuatana na ndege hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niende katika suala la sera ya wajasiriamali au *SME Policy.* Sera hii ndiyo sasa hivi tumeishikia bango na kwa sababu sera yenyewe ni nzuri imefafanua vizuri ni jinsi gani itawawezesha watu kujizalishia

kipato, imeweza kufunika hata sera nyingine na wakati anachangia Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, aliuliza mbona hawa wakulima hawakopeshwi, ni kweli hawawezi kukopeshwa kwa sababu sera ya wajasiriamali inasema wazi kwamba kilimo hakimo katika sera hiyo, kwa hiyo, kwa sababu mabilioni hayo yalitolewa kwa ajili ya wajasiriamali na kwa sura iliyopo sasa hivi ni kwamba mjasiriamali ni yule anayefanya biashara ndogo ndogo basi inamtenga huyu mkulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nashauri kwanza kabisa kwa sababu pengine sitapata nafasi ya kuchangia kwenye kilimo basi sera ya kilimo itakapokuwa inafanyiwa mapitio iangalie ni jinsi gani huyu mkulima anaangaliwa sasa kama yeye na ni jinsi gani ana-*fit* katika sera ya wajasiriamali.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile sera hii haiwatenganishi hawa wakulima kujulisha kwamba huyu ni mkulima wa aina gani ili aweze kupewa msaada kufuatana na lile daraja lake, kama ni mdogo sana ama mkubwa sana, kwa sababu tunapozungumzia kwa mfano matrekta hatutegemei kwamba kila mkulima ana uwezo wa kuchukua trekta kwa wakati ule, kwa hiyo, nilikuwa naona kwa kweli iko haja ya kuziangalia hizo sera zingine na vile vile kuweka mikakati madhubuti katika kuhahakikisha kwamba sera hizo zinatekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sera nyingi nilizopitia ambazo zingeweza kuongeza ajira kwa haraka zinaonyesha wazi kwamba zimejaribu kuchukua maeneo mengi na ni sera nyingi lakini tatizo liko kwenye utekelezaji mipango yetu inakuwa haiongei moja kwa moja kwa hiyo nilikuwa nashauri sera kwa mfano ya kilimo katika utekelezaji wake, naomba kuwe na mawasiliano yaani *coordination* ili kuweza kuhakikisha kwamba yale ambayo yamekusudiwa na hasa kwa ajili ya hawa ambao wamejiajiri katika kilimo na ndiyo wengi wanaoishi vijijini basi waweze kuwezeshwa na isiwe kwamba sasa wao watachukua *option* ya kukimbilia mjini badala ya kuishi vijijini ambako kuna hali ya nzuri na vile vile kuna rasilimali ambazo zinaweza zikabadilishwa kuwa ni kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu nyingine niliyoiona inaleta tatizo ni katika eneo la Wizara ya Miundombinu ambayo inatakiwa kuchangia ongezeko la ajira, katika eneo hili naangalia bandari yetu ya Dar es Salaam, nimefuatilia baada ya kupata malalamiko kwamba kuna kazi zetu zingine zinaongezeka thamani kwa sababu tu mizigo inakuwa imechelewa pale kwenye bandari na kucheleshwa kwa mizigo hiyo kunatokana na mrundikano wa makontena kutokana na hali halisi ya bandari ile pia ukiacha kwamba kuna huduma zinazohusika pale lakini pia hata uwezo wake umeanza kuwa ni mdogo kufuatana na watumiaji wengi, matokeo yake sasa zile meli ambazo zinaleta mizigo ambazo zilikuwa zinatakiwa zifike na kuendelea na safari yake zinabidi pengine zikae hata siku tatu na zikishakaa siku tatu ina maana kila siku zinachajiwa si chini ya dola 30,000 matokeo yake zinaamua kubadilisha *route* na kushusha mizigo maeneo mengine.

Kwa hiyo, kutoka kule inabidi zije meli ndogo ndogo na kushusha mizigo katika bandari sasa ya Dar es Salaam, lakini wakati huo huo unakuta kwamba katika vile viwango tunavyochaji sisi unapoleta meli ndogo ina maana unapata mapato kidogo

kuliko ungeleta ile meli kubwa, sasa kwa sababu tayari utafiti ulishafanyika na kulishaonekana kwamba bandari ya Mtwara ingeweza kusaidia kupunguza hilo tatizo kwa sasa hivi inatoa kontena chini ya elfu kumi lakini kama wangeruhusu utaratibu ukaanza kutumika kule, bandari ya Mtwara nimeambiwa kwamba ina uwezo mkubwa na ina uwezo wa kuchukua mpaka makontena 150 na hawa wadau wako tayari wao wafikishe kule na warudishe sehemu yoyote inayohitajika kwa bei ile ile, sasa tatizo letu lipo wapi, kwa nini tusiwe tunafanya maamuzi kama wajasiriamali kwa kuona kwamba hapo tunapoteza na tuweze kusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hilo ndipo ninaporudi kwenye suala la utawala bora kwa sababu masuala ambayo ni ya msingi yanachukua muda mrefu sana kufanyiwa maamuzi, lakini masuala mengine yanapata maamuzi ya haraka sana kwa hiyo, mimi naomba kwa kweli Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa sababu kama hayo makontena yataweza kupita kama inavyostahili naamini ajira nyingi sana zitaongezeka na pia hata miji ile ya Kusini sasa nayo itaanza kuchangamka, tukianzia na Mtwara ambako hata mimi sitoki huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudi kwenye suala la motisha kwa wale ambao wanakuwa wamezalisha ajira, nilizungumza asubuhi na sasa hivi narudia, hali hii ya kutenga wale wawekezaji wakapewa unafuu wa ulipaji wa kodi kwa sababu tunawavutia, mimi nakubali wapewe lakini hata huyu mwekezaji wa ndani na yeye aangaliwe ili aweze kuwekeza katika maeneo hayo ambayo yako mbali vijijini au maeneo mengine, kwa sababu tunapokuwa tunamfunga kabisa kwa sababu tu kwamba yupo nyumbani lakini naye anakabiliwa na mazingira mengine ambayo yapo nje ya uwezo wake pengine yule anayekuja anakuwa tayari yale mazingira kwake ameshayatatua, kwa hiyo, mimi nilikuwa nashauri kwa kweli *TRA* waliangalie vizuri hili suala, kutolewe *incentives* za kuwawezesha hawa *private sectors* kuweza kuzalisha ajira nyingi ili kuweza kutoa ajira kwa wingi pia kwa watu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho kabisa ni kwamba hili naona ni zito lakini kwa sababu lina msingi naomba nilizungumze yawezekana likawa linagusa kidogo Katiba lakini kwa sababu nataka kuchangia jambo ambalo pengine linaweza likaboresha naomba liangaliwe kama mchango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naangalia hasa jinsi ambavyo sera zetu zinawezaje kuwa endelevu, nilikuwa nafikiria kama kuna uwezekano basi pengine tungefanya *research* ya kuona kabisa Wizara zetu kama ambavyo zimekuwa zinakaa ziwe zinazingatia mambo yapi ili ikiwezekana hizi sera ziweze kusimama kwa muda mrefu kwa sababu sera ya kilimo na ufugaji, sasa hivi tayari kuna mabadiliko kwa hiyo, unakuta zinapobadilika mara kwa mara yawezekana zikawa zinachangia kutokuwa na uendelevu wa yale ambayo tunakuwa tumekusudia, kwa hiyo nilikuwa naomba liangaliwe kwa mapana na hili sizungumzii kama ni suala la haraka lakini liangaliwe kwa mapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hotuba hii iliyopo mbele yetu, kwanza napenda kutoa pole kwa Mheshimiwa Savelina Mwijage kwa kufiwa na mtoto wake pamoja na dereva wake, naomba Mwenyezi Mungu ampe moyo wa subira, hapa duniani tu wasafiri, Bwana alitoa Bwana ametwaa jina lake lihimidiwe, *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nichukue fursa hii nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu ambaye ni rafiki yangu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa wanayoifanya ingawa kwa kweli wanaifanya katika mazingira magumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni nyeti sana, ndiyo imechukua asilimia 50 ya Watanzania na hasa walio maskini, inategemewa na walalahoi wote wa nchi hii kwa hiyo, Serikali iangalie kwa upana zaidi Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kuongelea yafuatayo; nitaongelea *SACCOS*, vikundi vya uzalishaji mali vya vijana, *NSSF*, vitendea kazi kwa maafisa usharika na maafisa vijana, mafunzo kwa vijana na takwimu za vijana hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa masikitiko naomba nielezee kwamba pale Dar es Salaam kuna *SACCOS* nyingi sana lakini mojawapo ya *SACCOS* hizo nimetembelea *SACCOS* tatu ambazo kimtazamo zina uwezo mkubwa sana wa kiutendaji, ambazo ni *Kitunda SACCOS* ambayo iko katika Kata ya Kitunda, Wilaya ya Ilala, *Ukonga SACCOS* ambayo iko kata ya Ukonga, Wilaya ya Ilala na *Temeke Women SACCOS*, hizi zote zina idadi ya wananchama wanaozidi 3,000 na zimekwishatoa mikopo inayokadiriwa kuwa karibu shilingi bilioni 1.3, swali najiuliza je, *SACCOS* hizi hazina sifa za kupewa fedha za JK, lakini mpaka leo hii hazijapewa ukifuatailia utakuta *SACCOS* ambazo hazizidi hata watu 300 zimepata pesa.

Kwa kweli hapa najuiliza kuna nini, hii ni haki kweli? Mmetutuma tupige debe na tumepiga debe kweli miaka miwili na nusu sisi kazi yetu ilikuwa ni kupiga debe kuhamahasisha watu wajiunge na *SACCOS* na zimefanya vizuri lakini ambazo zimefanya vizuri zimetupwa pembeni, hii mnatuambia nini, tuache kupiga debe maana yake mimi naanza kukata tamaa, hatuwezi kuhangaika kila siku tunafikia hatua nzuri lakini inafika wakati wa kugawa fedha zinaenda kupewa *SACCOS* ambazo hazieleweki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba *SACCOS* hizi zinawajua wananchi walio chini na zinawatambua wenye mahitaji halisi, hawa akinamama wauza mboga, wauza samaki na wauza maandazi, mafundi seremala, hawa wote wanategemea *SACCOS* hizi kwani hawana sifa za kupata mkopo katika benki zetu kwa kuwa riba ni kubwa lakini *SACCOS* hizi zinatusaidia na hasa katika huu mkopo wa JK ni ndogo lakini kusema kweli riba ni ndogo na muda wa kulipa ni mwaka mmoja tofauti na hizi zingine baada ya mwezi au wiki unatakiwa kulipa, kwa kweli mimi nimesikitika sana naanza kukata

tamaa katika kazi hii mliyotutuma ya kuhamasisha wananchi kujiunga kwenye *SACCOS*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa wanachama wenyewe ombi lao ni punguzo la riba na mafunzo ya ushirika ni mafunzo ambayo ndiyo mara kwa mara wanayaomba, wale ni wachapakazi sana na hasa akinamama wana ari ya kazi lakini kwa kweli tunakosa ushirikiano na viongozi wetu walipo Serikalini wanatoa mikopo hii kwa upendeleo, wanaangalia suala za watu kwa kweli mimi sijui tunaenda wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiangalia katika *SACCOS* ya Kata ya Kitunda, mayai yote ambayo yanauzwa Mkoa wa Dar es Salaam yanatoka katika *SACCOS* ya Kitunda na *SACCOS* hiyo ndiyo inayotoa mikopo kwa hawa wajasiriamali, eneo lile pia wanajihusisha na ukulima wa mboga mboga na Mheshimiwa Naibu Katibu Mkuu ni shahidi, aliend kufungua jengo lao, jengo ni kubwa lenye ghorofa moja, ni jengo la kisasa lina sifa, bodi yao iko makini lakini nashangaa sijui tunafanya nini kwa kweli, mimi nasikitika sana si kawaida yangu kusikitika sikitika ovyo na si mtindo wangu kwa kweli mimi sikuumbwa kusikitika, lakini kwa hili nasikitika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikirudi *Ukonga SACCOS*, nimetembelea *SACCOS* ile, ina uwezo mkubwa ina *branch* Temeke, imefungua pale Magomeni ina uwezo mkubwa na ina wanachama mpaka Mkoa wa Pwani, hizi *SACCOS* ambazo naona kama Serikali haitaki kuzipatia fedha, haiziamini lakini zina uwezo mkubwa, Serikali ina kigugumizi kwao, mimi kwa kweli naendelea kuamini *SACCOS* ndiyo mkombozi wa wanyonge hapa nchini.

Naiomba Serikali iziangalie hizi *SACCOS* kwa jicho la huruma na Mheshimiwa Rais alikuwa na azma ya dhati kabisa katika kusaidia lakini watu wanamuangusha, Mheshimiwa Waziri Mkuu nakuomba ukazitembelee *SACCOS* wakati ukiwa Waziri wa *TAMISEMI* una wafahamu sana wale akinamama wa *SACCOS*, tunakuomba kwa kofia yako hiyo uzitembelee hizi *SACCOS. (Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Umeona Waziri hatoshi mpaka uende kwa Waziri Mkuu. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Naibu Spika, uchungu tu. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu ukazitembelee uweze kujua kwamba hizi *SACCOS* zina sifa au hazina maana yake hawa watu mnaowatuma naona hawaelewi, tunaomba kwa kweli mtusaidie, sisi bila *SACCOS* Dar es Salaam hatuwezi kufika popote, wale vijana wanaokaa vijiweni wataokoka vipi bila *SACCOS* na hamtaki kuzitambua, mnatupa wakati mgumu Dar es Salaam ina watu zaidi ya milioni 4, kwa kweli mimi toka rohoni nasikitika sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nisiendelee tena nisije nikalia bure. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwa upande wa vijana, vikundi vya uzalishaji mali, pale Dar es Salaam eneo la Vingunguti kuna kikundi kimoja cha vijana kinaitwa

Sahara, kinajihusisha na utengenezaji wa majiko sanifu, vijana wale wamejiunga ni kikundi ambacho kinazalisha majiko mengi sana na hata yale yanayouzwa mikononi huko Dar es Salaam, lakini wamekuwa wakipata taabu sana kwa kutafuta eneo, wameandika barua zaidi ya kumi katika mamlaka husika, hamna mtu anayewasikiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa vijana wamekuwa kama watoto yatima au kuku wa kienyeji, wamejikusanya, sasa wameingia kwenye nyumba za watu wamepanga wanatengeneza vitu vyao mara mwenye nyumba anasema sitaki nimepandisha kodi, wanahama na kuanza kutangatanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa vijana baba yao ni nani, ni nani anayewaangalia wameshajikusanya, ni nani mwenye majukumu ya kuwaangalia, tutaishia sisi wanasiasa sawa tunaenda, lakini watendaji kwa nini wanakosa dhamira ya dhati, hawana uzalendo, kwa nini tunawanyanyapaa hawa vijana, halafu baadaye tunasema vijana hawana adabu, wavuta bangi, sisi wenyewe hatutaki kuwasikiliza wala kuwasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iwaangalie vijana kwa jicho la huruma na utekelezaji, kama ilivyo azma ya mpendwa wetu Rais. Rais wetu ana nia njema sana, lakini watendaji baadhi yao wanatuangusha, moyo wa uzalendo umepotea, yule baba anahangaika mwenyewe tu na wasaidizi wake wachache lakini tumebaki kusikia tu tunapiga makofi tunamwachia au tunawaachia baadhi, nchi yetu itajengwa na wenye moyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Marehemu Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere alisema tunahitaji vitu vine, watu, ardhi, saisa safi na uongozi bora. Watu naona wanapotea, hawapo kila mtu anajiwazia nafsi yake, lile bomu unaloliacha bila kulihudumia litakuja kukugeukia mwenyewe, bomu la vijana si bomu la kuchezea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa hawa vijana na hasa katika Mkoa wa Dar es Salaam tunaomba watengewe maeneo ya uzalishaji mali. Katika maeneo ya pale Pugu Wilaya ya Ilala wajengewe viwanda vidogo vidogo ili wale vijana waweze kuzalisha katika fani mbalimbali, kuna kutengeneza majiko, kama kuna vile vikundi ambavyo vimezagaa zagaa pale mtaa wa Gerezani mara unakuta mabati yako kwenye mifereji waweke eneo moja kule Pugu eneo lingine peleka Mbagala, lingine peleka Machimbo ya Kunduchi, viwanda vidogo vidogo wazalishe tuachane na kazi hii ya vijana kuzurura na soksi mbili mikononi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii nchi haiwezi kwenda kwa kushika soksi mbili mikononi na kutafuta hela za *operation,* mgambo wale kamata machinga. Zile fedha za machinga kajenge kule viwanda siyo hela ya *population* kulipa watu ambao hamna faida. Maana unapofanya *operation* unatumia gharama. Hela za gharama kajenge viwanda, kwa njia nyingine tutafute taasisi ambazo zinaweza kutusaidia. Mimi naiomba Wizara ishirikiane na Halmashauri kuainisha maeneo ya hawa vijana waweze kuzalisha mali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba pia niipongeze hii taasisi ya *NSSF* chini ya uongozi wa Dr. Dau kwa kazi nzuri anayofanya. Kazi anayoifanya si tu kwa yale majengo ya Chuo Kikuu cha Dodoma, bali pia pale Dar es Salaam mimi niko Kamati ya Nje, Ulinzi na Usalama pale Lugalo amejenga majengo mazuri sana nyumba za askari, Kurasini wamejenga majengo mazuri sana usiku na mchana. Hata nje kwenye Balozi zetu pia *NSSF* wanajenga. Wametujengea jengo la machinga ni *NSSF* kwa hiyo, naomba *NSSF* itujengee viwanda vidogo vidogo viwasaidie wa machinga na vijana wanaokaa vijiweni waweze kuzalisha mali. Hii itatusaidia na hii itaongeza ajira na hii tutaepukana na mambo ya malalamiko na vijana kutumiwa vibaya. Maana yake kukosa kazi ni sehemu kuchukua hata tabia mbaya ambazo hawakuzaliwa nazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nije katika haya masoko madogo madogo katika Mkoa wa Dar es Salaam kuna masoko mengi sana ambayo hayahitaji gharama kubwa. Taasisi zinaweza kuingia ubia na Halmashauri husika wakaboresha yale masoko, yakishaboreshwa vijana wengi na akinamama watapata ajira kupitia eneo hilo, lakini pia na mapato ya Halmashauri yataboreshwa. Lakini sasa hivi majengo yamekaa ovyo ovyo maana unashindwa hata kumwambia lipa hela, utalipaje na jengo lenyewe halina maana? Kwa hiyo, taasisi zetu, mifuko tuliyonayo yote hii itusaidie kuboresha masoko pale Dar es Salaam au nchi nzima katika njia rahisi ili tuweze kuongeza ajira ziweze kutusaidia hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye mafunzo ya vijana. Tunaomba Serikali iendelee kutoa mafunzo kwa vijana ili waweze kuwa imara katika kufanya biashara zao. Nije pia niipongeze *SIDO* na *TIRDO* imekuwa ikitoa mafunzo sana kwa vijana wetu. Lakini naona pia naona haitilii uzito sana hata Bajeti inayopangiwa ni ndogo. Lakini *TIRDO, SIDO* mafunzo yao ni rahisi sana na teknolojia wanayotumia ni rahisi mno. Lakini zina manufaa makubwa. Natoa mfano kuna vijana 100 niliwapeleka pale *TIRDO* Dar es Salaam kusomea chaki siku tano tu wamekuwa watalaam. Mashine zao hizo za kutengenezea zinauzwa laki nane ni ajira tayari. Kuna mafunzo ya kutengeneza mishumaa, mishumaa inatoka China, chaki zinatoka China, lakini hapa tuna uwezo wa kuzitengeneza tukaacha mambo ya kuagiza chaki China tukaweza tukawaambia Halmashauri zetu na shule zetu zinunue chaki kutoka kwa vijana. *(Makofi)*

Sasa ajira zipo nyingi lakini kwa nini hatutumii, kwa nini hatuwi wabunifu, wavivu wa kufikiri, tuwe wabunifu. Lakini hasa hasa naomba tuwe wazalendo, tunaondoka tutaacha vizazi vyetu vikihangaika, nchi hii imelelewa na watu wazalendo ndio maana sisi tuko leo katika nyumba hii. Ni uzalendo wa wale waasisi wa nchi hii na sisi pia tuna dhamana ya kusaidia vizazi vinavyokuja. Tutumie dhamana tuliyopewa na Mwenyezi Mungu kupitia kura za wananchi ili tuweze kuboresha maisha ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Leo umesema kutoka moyoni kweli kweli. Hongera sana na ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika hii hotuba ya Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. *(Makofi)*

Kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri na kwa namna alivyoweza kuiwasilisha tena kwa muda muafaka. Lakini vile vile naomba nichukue nafasi hii kwanza kutoa pole kwa mwenzetu Mheshimiwa Savelina Mwijage, kwa kufiwa na mwanawe ambaye kwa kweli ni imani kwamba msiba huo wengi umetusikitisha kwa sababu umekuwa ni wa ghafla zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tulipo tunazungumzia leo hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. Kwa hiyo, leo kazi yetu tuna kila aina ya sababu ya kuzungumza na kuona ni kwa kiasi gani tutakuwa tayari na Serikali itakuwa tayari kuwasaidia vijana hasa tukikumbuka kwamba vijana ni Taifa ambalo tulikuwa tunawaita Taifa la kesho, siku hizi wanasema ni Taifa la leo, maana inaonekana wamesubiri kesho haifiki. Kutokana na hali hiyo sasa kumbe tunahitaji kuwasaidia kuanzia sasa. Tunapozungumza matatizo ya vijana, vijana wanayo matatizo makubwa mawili, tatizo la kwanza vijana wetu hawana ajira. *(Makofi)*

Lakini tatizo la pili hawana namna ya kupata kipato kwa maana ya biashara. Tunapozungumza ajira ziko ajira za aina mbili, ajira ya kwanza ni ajira ya kujiajiri, lakini ajira ya pili ni ajira ya kuajiriwa. Hii ya kuajiriwa ni ile ambayo mtu anategemea ajiajiriwe Serikalini, aajiriwe na sekta binafsi au aajiriwe viwandani. Sasa tunapozungumzia suala la ajira ya Serikali ni ndogo sana na kwa hali hiyo, watu wengi au vijana wengi hawawezi kupata nafasi hizo.

Lakini hata hizi za kwenye taasisi matatizo makubwa ambayo yanawakumba vijana wetu ni matatizo ya elimu na sisi lazima tukubali kwamba si kwamba hawakuwa na uwezo wa kusoma lakini sisi ndiyo hatuwatengenezea mazingira ya wao kuweza kusoma. Maana wengi walikuwa wanafaulu lakini shule hazikuwepo na kutokana na hali hiyo sasa leo wanapata matatizo ya kuajiriwa kwa sababu kila akiomba ajira anaambiwa lete vyeti na cheti chake cha darasa la saba, kwa hiyo, inakuwa ni tatizo sana au ni kazi kubwa kupata ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ajira zingine ni zile za viwandani na hizi ni ajira ambazo kwa kweli si nzuri sana kwa sababu viwanda vyetu, watoto wengi wanaoajiriwa pale wanaajiriwa kama vibarua. Kwa hiyo, leo akienda anapata kazi, kesho akienda hakuna kazi. Hili ni tatizo kubwa na mimi nitoe ombi maalum ambalo Mheshimiwa Waziri itabidi katika majumuisho yake nitaomba alijibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakuomba kabisa baada ya kikao hiki cha Bunge nakuomba uje katika Mkoa wetu wa Mara katika jimbo langu la Musoma Mjini. Kule yapo matatizo ambayo yanahusiana na watumishi wale wanaofanyakazi viwandani. Matatizo hayo aidha, yanatokana labda kuna mahali ambapo Serikali kidogo ilijikanganya, maana kuna wakati Serikali ilipandisha viwango vya mishahara, lakini

baadaye ikasema imesitisha. Sasa imekuwa ikileta mgongano mkubwa kwa wale watumishi na wale waajiri wa viwanda. Hata baadhi ya viongozi wa Kitaifa wamekuja pale wale watumishi mpaka wakadiriki kuwazomea. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi nakuomba kabisa kwamba uje twende tukae na wale watumishi hasa wale wa viwanda vya samaki pamoja na waajiri wao, waseme matatizo yao na tuone namna ya kuweza kuwasaidia ili kama panahitajika elimu basi tuweze kuwaelimisha na kama waajiri wao nao wanahitaji kuelimishwa basi tuwaelimishe ili *harmony* iendelee kuwepo na vijana wetu wafanyekazi kwa amani na upendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aina nyingine ya ajira kama tulivyosema ni ile ya kujiajiri wenyewe ambayo ni matumaini yangu kwamba hiyo inaweza kupatikana katika biashara mbalimbali ambazo vijana wetu wanaweza wakafanya, ajira zingine zikapatikana katika kilimo, ajira zikapatikana katika uvuvi, ufundi na katika maeneo mbalimbali. Lakini hayo yote naomba tu niseme kwamba vijana wetu wako tayari na wako tayari kujipatia ajira za namna hiyo.

Mimi siku moja nilisikia mtu mmoja anasema humu kwamba vijana wanaogopa kilimo. Mimi naomba niseme si kweli hata kidogo, isipokuwa vijana wanahitaji waandaliwe mazingira ya kuwafanya hata kama ni kwenye kilimo waende basi kwenye kilimo, mfano ambalo Serikali inahitaji ilifanye ni pamoja na kuwaandalia mazingira ya miundombinu. Bahati nzuri maeneo yapo, lakini wawezeshwe walau wapelekewe kule maji ili waweze kulima kwa kutumia kilimo cha umwagiliaji, awe na uhakika wa kulima, awe na uhakika wa kuvuna. Tunadhani kwamba kwa kuwasaidia kwa njia hiyo basi vijana hawa wataweza wakaendelea vizuri zaidi. *(Makofi)*

Lakini hata wale ambao wanajishughulisha na biashara ndogo ndogo nao tatizo kubwa hasa wale ndugu zetu wa mijini tatizo kubwa linalowakabili kwanza ni maeneo ya biashara. Lakini vile vile na mitaji ya kufanyia biashara hizo. Unakuta kwamba kwa sababu kwa bahati mbaya hatujawatengenezea maeneo ya kufanyia biashara hata ule mtaji mdogo alionao yule kijana anayeitwa kwa jina maarufu la machinga akiweka mahali anauza hiyo biashara yake kama ni ya soksi au nini kinachofuatia ni kwamba tunasema *operation* ya kusafisha mji hata kile kidogo alichonacho nacho ananyang'anywa. Sasa anaponyang'anywa maana yake ni kwamba huyu kijana sasa tunamtuma akawe jambazi maana hata alichokuwa nacho, nacho kimeisha au akawe mvuta bangi au aende akawe mcheza *pool*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nadhani kwamba Serikali kabla ya kusema inawahamisha vijana katika maeneo mbalimbali yaliyoko basi ni vizuri tukaweka mipango mizuri ya kuwaandalia maeneo ambayo tunadhani kwamba wanahitaji wapelekwe na huko sasa ndiko tuwaandalie mazingira mazuri ya kuweza kuwasaidia wapate mikopo na hatimaye waweze kujiendeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo tunaweza kuwasaidia vijana wetu ni eneo la ufundi. Tunapozungumza ufundi tunaipongeza kwanza Serikali kwamba imedhamiria kwa dhati kabisa kuhakikisha kwamba vyuo vya *VETA* vinakuwepo vya kutosha katika nchi nzima ambavyo vijana wetu watajifunza useremala, watajifunza

ufundi uashi, watajifunza uma-*mechanical*, pamoja na fani mbalimbali. Sasa ombi langu basi kwa kuwa vyuo hivi tayari kwenye maeneo ambayo yameshaanzishwa ni vizuri vyuo hivi vikapanuliwa ili vichukue wanafunzi wengi zaidi kuliko ilivyo hivi sasa, maana kwa sasa vinachukua wanafunzi wachache na tayari vyuo hivyo vinakuwa vimejaa na wanafunzi wengi wanashindwa kupata nafasi za kujifunza ufundi. Lakini ni ombi langu kwamba na vyuo vingine navyo vingeendelea kutoa elimu ya ufundi hasa hivi vya *certificate* na hivi vingeweza zaidi kuchukua wanafunzi wetu hawa wanaomaliza darasa la saba wanaokosa nafasi ya kujiendeleza lakini na hata wale wa kidato cha nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii itasaidia zaidi kwamba vijana wanapokuwa na maarifa mengi waliyojifunza inawapa nafasi nzuri zaidi ya kuchagua kazi kuliko ilivyo hivi sasa. Labda hilo kwa ushauri wangu ni vizuri kitengo hiki au Wizara hii ya Kazi ingejitahidi sana kuangalia baadhi ya mafunzo ambayo ni haraka ambayo watu wetu wangeweza kujifunza ambavyo kadri tulivyotembea mambo mengi tumeweza kuyaona.

Labda tu nitoe mfano ukienda katika nchi sana sana zile za Asia, maana *Europe* kule wameendelea zaidi. Lakini Asia yapo mambo mengi, viko vitu vingi ambavyo tunavyoweza kuvileta na tukawasaidia watu wetu. Mfano, kule Asia ukienda nchi kama *Thailand*, ukaenda nchi kama China unakuta watu wanafuga ufugaji huu mdogo mdogo wa samaki kama kamba, sasa ukiangalia kuanzia Mtwara mpaka Tanga ukanda wote huo ni ukanda wa bahari ambapo gharama za ufugaji ule wala si kubwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunadhani kwamba kama kungekuwa na kitengo ambacho kinajifunza kule halafu kinayaleta kingeweza kusaidia zaidi watu wetu. Lakini hata wale tulioko kule kando kando ya Ziwa mfano Musoma, Mwanza na kule Kagera pamoja na ndugu zetu wale wa Ukerewe bado tulikuwa na nafasi nzuri ya kuwafundisha uvuvi ambao hauna gharama kubwa, vijana wanajenga madimbwi, ambayo ni madimbwi ya gharama nafuu wakipata ule utalaamu basi wanaweza kufuga samaki kwa njia ambayo ni rahisi na ikawasaidia kuleta kipato chao kuliko wanavyohangaika sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uwezeshaji kwa vijana wetu. Suala hili kwanza tunaishukuru Serikali kwa namna ilivyoleta zile fedha ilivyosisitiza uanzishwaji wa wa *SACCOS*, yapo matatizo mengi ambayo yamejitokeza, namshukuru Waziri Mkuu jana alivyojibu kwamba sasa Serikali imejifunza na imeona kwamba ni kwa kiasi gani sasa inaweza ikaanza tena. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ni vizuri hata ile mikopo ambayo sasa inatolewa ya uwezeshaji ambayo kwa namna moja imekuwa ikilalamikiwa sana kwamba mikopo ile imekuwa ikiwalenga wale watu wenye kipato kikubwa peke yake. Sasa ni vizuri kuwepo na utaratibu ambao utakuwa wa wazi, vile vile vinavyopewa viweze kufahamika kiasi cha fedha kilichotolewa kifahamike. Nadhani kwamba kwa kufanya hivyo sasa kutakuwa na uwazi zaidi hata yale malalamiko yanayotokea na hayo yote yataisha na tunadhani kwamba kwa kufanya hivyo sasa Serikali itakuwa imeongeza uwazi zaidi kwenye upande huo kuliko hali ilivyo sasa ambavyo kwamba fedha zinatoka lakini hazijulikani ni akina nani wamepata na ni kwa kiasi gani fedha hizo zimepatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ombi langu kubwa pamoja na mengine yote ni hilo tatizo kwamba wale vijana ambao wamekuwa wakifukuzwa katika maeneo yao ya biashara hebu basi tatizo hilo kwanza ni vizuri Serikali ihakikishe kwamba inawapatia maeneo ya kufanyia biashara na baada ya hapo sasa ndipo wapelekwe huko kuliko hali hiyo ya kufukuzwa kabla hawajapewa eneo la kufanyia biashara.

Kwa hiyo, naipongeza Wizara, naipongeza Serikali kwa juhudi inazozifanya lakini bado tunasema tunayo kazi ndefu, tuna jukumu kubwa kwa vijana ambalo ndilo Taifa la kesho, tuna jukumu kubwa la kuhakikisha kwamba vijana hawa wanapata maisha bora ili kesho nao waweze kuwa viongozi bora nao waweze kulitumia Taifa lao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii. La kwanza, naunga mkono hoja mia kwa mia. La pili, naomba niwapongeze Waziri Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya na Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga na viongozi wote wa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza kwa msingi mmoja kwamba ukisoma kitabu cha hotuba ya Wizara ni katika hotuba zinazokwambia hapa tumefanya hivi na unakiona pale, wamefanya kile na unakiona, tumejenga hapo na unapaona. Kwa hiyo, ni Wizara kwa kweli inatia moyo katika kutenda na kuweza kwa Kiingereza kusema *to deliver,* siyo wapo tu ili mradi wawepo. Kwa hiyo, naomba niwapongeze, lakini wasije wakawa kama mgema akisifiwa tembo hulitia maji. Nawatakia kila la kheri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine mimi nitajikita katika maeneo matatu, ajira, vijana na *NSSF*. Katika ajira nakumbuka mimi nilikuwa mwanzilishi wa mtandao wa *YES* dunia nzima, na niliporudi hapa nilikuwa wakati huo nimemaliza tu kuandaa mkutano wa *Beijing*. *YES* maana yake *Youth Employment Services* ambapo niliporudi hapa nikaitisha kikao cha vijana waliojitokeza alikuwa ni Mheshimiwa Juma Killimbah ambaye sasa ni Mheshimiwa Mbunge, naomba nimpongeze sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hicho nilikuwa na uchungu ya kwamba tunapotazama masuala ya maendeleo mara nyingi tunatazama watu wazima na hatutizami vijana. Vijana ni kundi kubwa katika nyanja mbalimbali. Lakini kundi hili lina sifa moja, wana nguvu yaani nguvu za vijana siku zote ukiwa una nguvu, wanasema ahaa, una nguvu kama kijana, hawasemi una nguvu kama mzee. Kwa hiyo, sifa moja ni nguvu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kufanya kazi nguvu inahitajika, lakini la pili ni ari, vijana wana ari, kila wanachokifanya, kama atacheza muziki atacheza kwa ari, kama atakunywa pombe atainywa kwa ari, kila jambo analolifanya analifanya kwa moyo wake na sisi tunapaswa kutambua vipaji hivyo vya vijana tuweze kuvitumia katika kuleta maendeleo. Lakini pia tutambue maeneo mbalimbali ya vijana tusije tukaangalia upande mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vijana vijijini, kuna vijana wakulima, kuna vijana wavuvi, kuna vijana wachunga ng'ombe na wafugaji, kuna sehemu za kazi. Hili eneo nalo wakati mwingine tunawasahau. Mimi nimetazama takwimu za walimu katika sekondari za kata walioletwa katika Wilaya ya Ukerewe. Nilikaa na walimu wa Tarafa moja na asilimia 98 ya walimu wale ni vijana chini ya umri wa miaka 30, vijana hao walinitia uchungu nikasema sasa nani anayewasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi vijana wanakuwa ni watu hawaaminiki hata akitafuta nyumba ya kupanga hapewi kwa sababu haaminiki. Akitafuta mkopo haaminiki kwa sababu wanajua hawana fedha. Hivyo pia ndiyo vikwazo ambavyo vijana wanapata. Je, tunawaweka katika fungu gani vijana ambao wapo kazini, lakini bado wanakabiliwa na matatizo makubwa ya maisha na si ajabu wangeweza kufanya vizuri zaidi kama tungewawekea *section* ndogo ya kuangalia na kuwalea vijana ambao wapo kazini, wameanza kazi, hawana vitanda, mishahara yao ya kwanza haijafika, hakuna anayewaangalia hawana mlezi na wakipotoka tunawalaumu vijana hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, kwa vijana ni wale vijana wanawake. Mara nyingi ukisema hata sisi tuliopo kwenye CCM, Umoja wa Vijana basi watu wanaangalia vijana wanaume. Mimi ningependa kuwe na *section* pia ya kuangalia matatizo ya vijana wanawake ili tunapopanga mikakati tunaangalia mahitaji ya vijana kama ni kijijini, kijana mwanamume ana mahitaji gani na kijana mwanamke naye ana mahitaji gani ya kumfanya aweze kujiajiri na asirithi umaskini ambao wamekuwa nao wazazi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa sasa niende kwenye hili suala la *YES*. Mheshimiwa Waziri ninampongeza sana kwamba hata katika hotuba yake ametambua hivyo, na mtandao huu ungekuwa wa muhimu sana katika kusaidia kutafuta ajira milioni moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tukiainisha Wilaya zetu, ajira milioni moja ni sawa sawa na ajira ya vijana 8,000 kwa kila Wilaya, utapata ajira milioni moja. Kwa hiyo, Wizara hii ikigawanya nguvu zake katika kila Wilaya tungeweza kabisa tukazidi hata hiyo ajira milioni moja. Kwa sababu ukishawezesha vijana 8,000 kwa kila Wilaya, basi hao vijana watakuwa *multiply effect*, watasaidia na vijana wengine, na kwa hiyo, itakuwa ni ajira kubwa kuliko ile ambayo tunaipanga kinadharia. Nawakaribisha sana katika Wilaya ya Ukerewe tunayo maeneo wakitusaidia, tunaweza hata tukagonga zaidi ya vijana 100,000 wakapata ajira katika uvuvi na katika *process* nzima ya uvuvi na ufugaji katika Wilaya ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa sasa niende kwenye eneo la *NSSF*. *NSSF* ni Shirika ambalo kwa kweli nalipongeza kwa dhati na Mkurugenzi wake anafanya kazi nzuri. Shirika ambalo linabadilisha maisha ya Watanzania katika kila nyanja. Ukiangalia *Business Park*, *Industrial Parks*, *AFUA Double Housing Scheme*, yote haya wanayafanya na yanaleta mabadiliko makubwa katika maisha ya Watanzania. Ni pamoja na nyumba tunazoishi Waheshimiwa Wabunge hapo *Area D* nadhani zimejengwa na *NSSF*. Labda

siku moja watafikiria kutuuzia ili wajenge nyumba nyingine, sisi tunaoishi humo tumekwishalipa kodi ya kutosha tuuzieni wapate uwezo wajenge sehemu nyingine na waendelee na kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine kubwa zaidi ambalo nataka kulisema mfuko huu sasa usiangalie mambo makubwa tu, nchi hii tunatoka katika sehemu mbalimbali. Mahitaji ya Mafia siyo jengo kama la Kariakoo, Dar es Salaam au kama unatoka sehemu za Rukwa, Kigoma, Kibondo, Ukerewe na Singida huko kwa Mheshimiwa Juma Killimbah ambaye tunashirikiana naye katika kuhakikisha kwamba kuna ajira za vijana. Ukiangalia sisi mahitaji yetu ni tofauti, ukijenga soko zuri na halitumii fedha nyingi, si ajabu soko la mahali kama Nansio, Ukerewe litahitaji labda milioni 200 tu, kunakuwa na soko zuri na mahali pa kuhifadhi samaki, na watu wanaokuja katika Visiwa hivyo wanachukua mazao yale yakiwa katika hali nzuri. Hivyo hivyo na mahali pengine tukijenga masoko itakuwa wakulima hawapati kichwa kumuuma wapi apeleke mazao yake kwa sababu kuna soko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ningependa niseme kuna vikundi vya akinamama. Kwa mfano, kuna kikundi hapa kinaitwa *Faraja Womens Group,* wanahangaika kupata mtu atakayewasaidia wana kiwanja chao kikubwa tu o*pposit*e na *St. Gasper Center* wanataka kuaandaa *center* itakayowawezesha wanawake katika Mkoa huu wa Dodoma na mahali pengine Tanzania kuweza kupata mafunzo mafupi mafupi. *(Makofi)*

Lakini *NSSF* sijui inawafahamu, sijui haiwafahamu, mimi nipo tayari kabisa kumshika Mkurugenzi wa *NSSF* twende wote nikamwonyeshe kwa sababu kazi hizo lazima tuzifanye kwa Majimbo yetu. Lakini unapopata nafasi ya kufanya katika Majimbo mengine pia lazima tuyafanye. Kwa hiyo, mimi nipo tayari kuwapeleka, wale akinamama ukiwaomba *collateral* wataipata wapi, lakini wakishakuwa na *centre* hiyo itahudumia Watanzania na lile jengo linaweza kuwa ni *collateral* ndiyo tunavyopiga hatua hivyo.

Kwa hiyo, mimi natamka hayo kuna sehemu nyingi tu katika nchi hii ukiangalia ambako tungeweza kupeleka nguvu na kusaidia vikundi siyo majengo makubwa tu lakini hata yale majengo ambayo yanaweza kuwa katika sehemu zingine. Mimi natamani tu siku moja *NSSF* mje mnijengee ghorofa nzuri pale Nansio ili tunapokuwa kwenye boti tunaingia walioko kule juu wawe wanatupungia mikono. Naomba mje mbona kwingine mnajenga? Kwa hiyo, ndiyo hivyo nchi inazidi kuboreka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa tu niseme kwamba kwa kweli kazi inayofanywa na *NSSF* ni mfano wa kuigwa na mashirika yote yenye fedha. Kama tungeweza kuwekeza na kuimarisha huduma kama wanavyofanya *NSSF* nchi hii ingesonga mbele. *(Makofi)*

Naomba niishie hapo kwa kuwakaribisha watu *NSSF* Nansio, Ukerewe ambako kuna umoja wa wafanyabiashara wa soko la Nansio, wanahangaika, naomba mje

mtusaidie kidogo hapo tunaahidi tutarudisha bila wasiwasi. Wana uongozi mzuri, wanafanya biashara nzuri na fedha zipo karibuni sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Thomas Mwang'onda, atafuatiwa na Msemaji wetu Ndugu Said Nkumba.

**MHE. THOMAS A. MWANG'ONDA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi muhimu sana ya kuzungumzia kile kilichonileta kwenye hili Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Wakati tumefanyiwa sherehe na Rais Mheshimiwa Jakaya Kikwete pale Ikulu ya Chamwino, nilimnong'oneza kidogo, baba umeniteua, kazi yangu kubwa itakuwa nini? Akaniambia kijana nataka ukatetee vijana. Nashukuru mimi ni kiongozi wa vijana na leo sehemu kubwa ya mchango wangu itagusa sana utetezi wa vijana wenzangu, la sivyo nisije nikaulizwa maswali, ninyi Bungeni mnachukua posho tu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya mchango wangu naomba niungane na Bunge lako Tukufu, familia ya akina Mheshimiwa Savelina Mwijage, wanachama wote wa Chama cha Wananchi *(CUF)* na Watanzania kwa ujumla, kupeleka salaam za rambirambi na kumpa pole Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Savelina Mwijage kwa kumpoteza mwanae nimesikia pamoja na dereva leo hii. Nampa pole sana. Ni majukumu tu yanayotufanya tuwe hapa tunachangia, lakini isingekuwa hivyo tungependa tukaungana naye katika kumpa pole hizi.

Naomba lakini nisiwe mwizi wa fadhila pamoja na msiba uliotupata nitumie fursa hii adimu kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Wizara ambayo nachangia hoja yake hivi sasa, Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya na Naibu wake ambaye nadhani hatunaye leo hii kwa maana yuko kwenye matibabu kidogo. Lakini najua kazi hiyo wamekuwa wakiifanya kwa pamoja.

Lakini pia nitakuwa mwizi wa fadhila nisipotambua kazi kubwa iliyofanywa na vijana wetu wa chini ya umri wa miaka 17. Kazi ya kwenda kutikisa Amerika ya Kusini si kazi ndogo wakarudi na kutupa heshima ambayo tumeipata. Kwa kweli nawapongeza sana kwa maana wale ni vijana, lakini na akina Mheshimiwa Kapteni George Mkuchika na Mheshimiwa Joel Bendera nao nawaomba wasife moyo waendelee hivyo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo utaniwia radhi, lakini lina utaifa ndani yake, naomba niliseme na najua litamgusa sana mtoa hoja Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya ambaye ni mwana Simba mwenzangu. *(Makofi/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Looo!

**MHE. THOMAS A. MWANG'ONDA:** Naomba nimpongeze pia na Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, najua limemgusa. Jana tumewatandika wale Wasomali bao tano kwa bila. Lakini ni sifa ya Taifa letu. Tuna kila sababu ya

kuipongeza *Simba Sports Club.* Yanga naomba msiumie moyo ni suala la Kitaifa. Sasa naanza kuchangia. Mliochukia mnisamehe kidogo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati jana Mheshimiwa Janeth Massaburi anachangia yeye alisema ana masikitiko. Mimi nina kilio lakini labda hakitakuwa na machozi. Kwa sababu nina asili ya udume huu basi nitavumilia ndani kwa ndani. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa mimi nimeteuliwa, lakini mgombea wa Urais wa Chama cha Mapinduzi asingepita, kwa maana Watanzania wasingempigia kura pamoja na Wabunge wenzangu wa Chama cha Mapinduzi leo hii tusingeshika Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naheshimu sana wale wapiga kura ambao wametuingiza hapa. Hata tulioteuliwa tuna deni kubwa sana kwa wapigakura, bila kujali mapenzi yao ya chama gani, huwa hatubagui hivyo. Mimi nimetumwa na wananchi wa Mbeya na wengine hunituma. Lakini leo wananchi wa Mbeya, kuna wananchi wana malalamiko mengi sana hasa kwenye suala la mafao yao, malipo, wanapoachishwa kazi, tunaita *redundancy* ile wengine wanaostaafu, kwa sababu mbalimbali. Wengine wako wananisikiliza kule Mbeya, niliwaambia leo nitajitahidi ujumbe ufike kwa Waziri ili tuone basi Jumatatu wakati anahitimisha ule mjadala anaweza akatusaidiaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Mbeya tuna *Mbeya Industry,* kile kiwanda kilifungwa tangu mwaka 1998 kutokana na kumbukumbu zangu za kuona wananchi pale Mbeya, mwaka huu ni wa 10 sasa. Kuna wafanyakazi pale wanadai shilingi milioni zaidi ya 75 hawajalipwa, hawajui waende wapi na wafanye nini ili waweze kupata zile haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wakati naona haya hata kukanyaga Mbeya, maana sina majibu. Ninamlilia sana leo mwana simba mwenzangu Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya hebu nisaidie pale Jumatatu unapohitimisha. Hebu nipe majibu ya ile *Mbeya Industry* kwamba hawa wananchi, hawa walalahoi tunaowaongelea, hawa waliotupa madaraka, waliotuamini tukaja huku, tunawasaidiaje ili waendelee kuwa na imani na sisi. Naomba sana Mheshimiwa Waziri, ndugu yangu sana, unisaidie ili ninapokwenda kupokea mwenge kule Mbeya niwe na la kujibu watakapokuja nyumbani kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na si hao tu, wala si hayo tu yaliyowapata, wale wananchi waliahidiwa kwamba baadhi ya zile mali au *assets* za kiwanda zikiuzwa wangepata malipo. Sasa yapo malalamiko, ningeomba Wizara inisaidie kuchunguza, kwamba zipo baadhi ya *assets* hizi zimeuzwa. Lakini malipo yale hayafanyiki, zinakwenda wapi zile pesa? Mtu ambaye amegusa Mbeya mzunguko wa fedha ni mdogo sana, ukikosa ajira bwana umekwisha. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana Mheshimiwa Waziri hebu tuangalie nini kinachoendelea pale mwaka wa kumi leo hii na bado wana imani wanaendelea kutupigia kura na kuwa na imani na sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, walipewa mfilisi, lakini mfilisi yule anasema ameshindwa kupata *buyer* kwa maana ya mnunuzi. Kwa hiyo, bado wanasua sua. Ni vizuri kwamba viongozi wa *NSSF* na wa *PPF* kuna suala pia lile la wafanyakazi wa Zana za Kilimo, bado nao wanalalamika kwamba hawajapatiwa malipo kwa mwaka wa nane sasa ya *NSSF* na *PPF* hawajui pa kwenda na nauli ya kuja Dodoma hawana. Nauli yao ni sisi Wabunge wao. Naomba sana Mheshimiwa Waziri unisaidie ili tuweze kujua tunakwendaje kuhakikisha wapiga kura hawa wanaendelea kuwa wetu. Mbeya mjini imeanza kubadilika pale, *NCCR-Mageuzi* waliwahi kushika. Lakini kazi tunayosaidiana na kaka yangu Mheshimiwa Benson Mpesya, tuna uhakika hawataweza kugusa tena. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Kweli.

**MHE. THOMAS A. MWANG'ONDA:** Lakini tunahitaji msaada wako Mheshimiwa Waziri. Nasema mimi nalia, mimi nalia ndani kwa ndani, ndani ya moyo wangu. Kuna *similar situation* kidogo na hawa watu wa Kiwanda cha Saruji cha *Mbeya Cement.* Mimi napokea malalamiko naleta kwako, ni vizuri tukayafanyia kazi kama malalamiko mengine yanayokuja. Wako wanaodai wafanyakazi walipwe malipo nusu, mengine hawajalipwa mpaka leo.

Nilikuwa naomba sana Mheshimiwa Waziri hili nalo hebu tulivalie njuga. Tuzidi kujenga msingi huu wa wapiga kura wetu na mambo yatuendee murua pale mwaka 2010. Kila mtu ana sababu yake, lakini na mimi naguswa sana na kazi kubwa inayofanya na *NSSF*. *(Makofi)*

Naomba kwa nafasi ya pekee kabisa niupongeze utawala au uongozi wa *NSSF* unaongozwa na swahiba wangu Dr. Dau, kina Magori na mwenzao Yunis John, lakini bila kusahau Bodi ya *NSSF* ambayo kama sikosei bado Mwenyekiti ni Ndugu Blandina Nyoni kwa kazi kubwa wanayofanya kuhakikisha maisha ya Mtanzania yanaboreshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jana nilikuwa pale *University of Dodoma (UDOM)* nimejionea maajabu kabisa. Nikajua kumbe Dodoma ni nzuri zaidi ya tunavyoiona, Dodoma inavutia kweli kweli. Kazi kubwa iliyofanywa na *NSSF* ambao kwa maelezo yao ya jana ya Mkurugenzi wao wamewekeza zaidi ya asilimia 50 ya kuhakikisha kwamba mradi ule unakwenda. Tunategemea kuwa na wanafunzi zaidi ya 42,000 maana hiyo ni habari njema za kiuchumi kwa Dodoma. Kazi ile si ya masihara, nina kila sababu ya kujisikia furaha kuona tunachagua viongozi wazuri, kufanya kazi nzuri kwenye taasisi zetu za Serikali. *(Makofi)*

Lakini liko swali linaendelea endelea hapa, tukikutana na wananchi wapiga kura wanauliza na hasa ni suala la miradi hii ni mizuri na kiujumla inafaidisha wananchi wa Tanzania. Lakini je, hakuna namna kukawa na moja ya moja kwa moja au *direct benefiting* ya wananchi labda kwa kupitia hisa ama namna nyingine. Ningeomba hili liwe changamoto. Tusiwe tu tunaona mradi unakwenda, lakini sisi tunaochanga *NSSF*

tulioajiriwa tunafaidikaje moja kwa moja, ndiyo swali wanalouliza wananchi. Naomba iwe changamoto kwa uongozi wa *NSSF* na Waziri wa Wizara husika. *(Makofi)*

Nakupongeza tena Mheshimiwa Waziri kwa kuhakikisha kwamba umefikia asilimia 43.7 kwa maana ya watu laki nne na thelathini na saba elfu ya ahadi tulioitoa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Nikupongeze tena kutokana na hotuba yako wewe mwenyewe kwamba sasa mmeandaa programu ambapo tutavuka hata ile ya watu milioni moja huko baadaye tutakuwa na ajira nyongeza ya watu milioni tano. Hili jambo ni la kuvutia, ni zuri na jema sana. Sasa sijui kama hesabu nimezikosea nilivyokuwa nikiipitia hotuba inasemekana ile sekta ya kilimo inatupa watu asilimia 70. Kwa hesabu za haraka haraka kama tuna watu asilimia 43.7 wamepata ajira kama hesabu zinavyosema ni sawa asilimia 70 ya watu wale wengine wako kwenye kilimo ina maana tumeshavuka. Tuna watu wa milioni tayari. Kama hivyo ndivyo, naomba Mheshimiwa Mizengo Pinda upokee pongezi zangu na uzifikishe kwa Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ina maana Ilani ya Chama cha Mapinduzi tunakwenda vizuri. Lakini tusibweteke, bado vijana wana changamoto nyingi sana katika suala la ajira. Kuna masuala ya UKIMWI, kuna masuala ya dawa ya kulevya. Lakini leo naomba nizamie kwa haraka sana kwenye suala la ajira, maana naona muda unanitupa mkono. Ndugu zangu ukosefu wa ajira kwa vijana unaweza kusema unasababishwa na mambo manne kwa mtazamo wangu makuu. Hali ya uchumi, ukosefu wa kazi, *work experience.* Mafunzo ya kutosha na la mwisho naweza kusema sera ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jana nilipata nafasi ya kuongea na mmojawapo wa waajiri wa Kiwanda cha *Coca Cola* ambao wengine walikuja Bungeni hapa, akaniambia tunapata vijana wazalendo kabisa, wazuri anaweza kuwa siyo *conversant* au mwenye kuweza kuongea lugha ya Kiingereza, lakini ukimpa nafasi ya kuongea Kiswahili, tumechagua. Lakini wengi wanazidiwa na wale waliosoma nje na wanazidiwa kwa sababu hawana uzoefu wa kazi. Ukiangalia kwenye *CV* wewe inakuja una digrii ulifanya kazi wapi? Hana. Kwa hiyo, anapoteza nafasi ingawa ana sifa nzuri sana za kitaaluma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, naomba tuangalie kwa siku za mbele. Hebu tutunge sera ambazo kama wanavyofanya wenzetu wakienda nchi za nje kusoma, utakuta kafanya kazi kwenye *Macdonors,* kafanya kazi hapa na pale, anapata *work experience* (uzoefu wa kazi). Siku anaomba kazi kwenye *CV* mambo mazuri anapata ajira mara moja na ndiyo maana ukichunguza mjini hasa Dar es salaam kuna ajira nyingi ambazo si za kilimo, waliopata kazi ni wengi waliosoma nje, kwa sababu wana *work experience*. Mtoto wa mkulima ambaye kiwanda cha kwetu cha kawaida hapati kazi. Sasa hawa tunawaweka wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka tuwe na majambazi wenye digrii. Kwa hiyo, nilikuwa naomba hili hebu tulifanyie kazi ya haraka sana kuhakikisha linakwenda vizuri. Sera nyingine ambayo naomba tutunge kwa haraka sana, hebu tuone kwa lugha ya kigeni

tunaita *social co-operative responsibility.* Tuone makampuni haya yanawajibikaje, yako makampuni mengi sana tumeyasamehe kodi. Lakini kwa nini hatuyabani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimetembelea kiwanda cha *Tanzania Tea Blenders* nikakuta pale wana mashine ambazo zinafanya kazi kama kwa njia ya *robbot, automated* na nyingine kwa mikono, nikawauliza sasa hapa si mnaingia hasara? Kwa nini mnawaweka hawa mikono, akaniambia hapana. Tumeona tuwe wanadamu, hawa wote wangepoteza ajira. *(Makofi)*

Kwa hiyo, wameamua tu kuwa *responsible* kuwa tu wawajibikaji kwamba wasipoteze ajira za watu, wameamua kuajiri watu tu ili mradi watu wakapata ajira, bila kuwa na sera yoyote inayowasukuma kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hilo, tulitungie sera, tuwalazimishe waajiri hasa hawa tunaowapa kodi makubwa. Kuna makampuni mengi sana ya madini na kadhalika. Hata kazi zingine kama si za mashine au ni za mashine wafanye na zile za mikono ili tuweze kuongeza ajira kwa namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la mafunzo, naomba sana Serikali hebu tuangalie msisitizo katika elimu ya mafunzo *(vocational training),* nadhani ni tafsiri sawa sawa hiyo. Tumeona mafanikio makubwa sana kwenye elimu ya *VETA.* Unakuta mtu amemaliza shule ya msingi, lakini kwa ajili amekwenda *VETA* kwa shilingi 15,000 au 60,000, basi anapata nafasi ya ajira kwenye gereji na kadhalika. Hebu tuweke msisitizo sana vyuo vile havitoshi, *centre* zile hazitoshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kuunga mkono hoja, ingawa nilikuwa bado na mawili, matatu, basi siku nyingine *Inshallah.* *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Maneno huwa hayaishi, yanakuwa mengi tu. Namwita Mheshimiwa Said Nkumba.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini vile vile kama walivyofanya wenzangu, napenda nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Sikonge, nitoe rambirambi zangu za dhati kwa msiba uliompata Mheshimiwa Savelina Mwijage wa kufiwa na ndugu zake wa karibu akiwemo mwanae.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, kaka yangu Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya. Nampongeza sana Mheshimiwa Kapuya na wasaidizi wake wote. Lakini vile vile na Mwenyekiti wa Kamati ambaye kwa kweli amepitia mambo mengi na kuyaleta haya Mheshimiwa Jenista Mhagama. *(Makofi)*

Nirudie kumpongeza sana Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, kwa sababu ya umahiri wake wa kushughulikia matatizo. Anazo sifa nyingi, lakini kushughulikia matatizo hasa ya wafanyakazi na kutatua migogoro mbalimbali. Nakupongeza sana Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nianze moja kwa moja kuhusu sheria za kazi. Mimi ningeomba sheria zetu za kazi nyingi zimepitwa na wakati. Kwa mfano sheria ya kazi ya fidia, mtu ameumia kazini, fidia anayolipwa hailingani na athari ambayo ameipata ya maisha yake yote, kwani amepoteza kiungo, mimi ningeomba sheria hii ije mapema. Kabla hujafa hujaumbika. Tunazungumza hapa sisi hapa, lakini sheria hii inatugusa watu wote sisi. Mimi ningeomba sana sheria hii ije ili iwasaidie watu wanaopata matatizo ya kikazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mikopo kwa vijana, hizi shilingi 50,000/= mnazoleta Mheshimiwa Profesa Kapuya, shilingi 50,000/= unampa, ndiyo maana hata watu hawarejeshi, shilingi 50,000/= atafanyia nini? Kikundi unakipa shilingi 50,000/= watu watano wanafanyia nini? Mambo haya yamepitwa na wakati, mtagawana shilingi 10,000/= hapo mambo yaishe.

Mimi ningeomba sana kwa kweli kama tunataka tuwawezeshe vijana tuwawezeshe kikamilifu, wapewe mtaji ambao wanaweza wakaufanyia vizuri katika kuleta maendeleo ya kiuchumi. Lakini ningeomba vile vile fedha hizi na zile fedha za JK ambazo kwa kweli zilikuwa zinapitia huko, mara benki, sasa zielekezwe kwenye *SACCOS,* huko ndiko vijana ambako wapo, ndiko *SACCOS* hizi ziko karibu sana na vijana. Zitawatambua vijana hawa, ziko vijijini, zitakwenda kuwasaidia vijana waweze kutekeleza wajibu wao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye suala la migogoro kazini. Nilikuwa nasoma humu migogoro kazini kwa mwaka jana wa 2007/2008 karibu 6,000. Ndiyo maana nilikuwa naona Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya hakuwa na kipara cha namna hii, kimeongezeka sana kwa sababu ya migogoro. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilikuwa naomba haya maeneo ya kazi nayo yatambue vyama vya wafanyakazi kwamba ndivyo vyombo vinavyowasimamia wafanyakazi kwa maslahi yao. Kwa hiyo, waajiri wavitambue vyama vya wafanyakazi na wakubali kufanya navyo kazi pamoja kwa maslahi ya wafanyakazi na kwa maslahi ya waajiri. Lakini vile vile maeneo mengine ya viwandani na maeneo mengine tu ya sehemu ya kazi hakuna Mabaraza ya Wafanyakazi. Migogoro na migomo mingi inakuwepo kwa sababu watu hawana mahali pa kupumulia matatizo yao. Ukishawapa nafasi watu wakapata nafasi ya kupumulia matatizo yao utarejesha hali ya amani na watu watasema mambo yao, watajadili matatizo yao, watasonga mbele wakiwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho niseme tu vile vile watumishi nao wakishatambua mamlaka ya ajira watu watakwenda pamoja, watafanyakazi pamoja. *(Makofi)*

Kuhusu kero za wafanyakazi, leo nataka kuzungumza kwa ufupi sana kero za wafanyakazi Shirika la Posta. Shirika hili la Posta limetekelezwa, watumishi wa Posta wana malalamiko. Wana mambo mengi sana hayajatatuliwa. Leo wana mikataba mingi

tu ya ajira, lakini watumishi hawa wa Posta vile vile wana mambo yao mengi tu ambayo kwa kweli wangepaswa wapatiwe ufafanuzi wao wa ajira zao za baadaye. Shirika hili la Posta limetunufaisha wote, hakuna hata mtu mmoja hapa ambaye hakuandika barua enzi zile za zamani akaipeleka Posta, akaiwekea *stamp* akachora na ndege ndani yake, akampelekea mwenzi wake, mwezi nzima ikarejea. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tumedharau Posta kwa sababu ya mambo yaliyopo sasa hivi. Naomba hawa watumishi ambao wamelitumikia Taifa hili kwa uaminifu sana waangaliwe. Posta wamebaki sasa hivi na baada tu ya kuondolewa wenzao wa *TTCL* sasa wao wamebaki pale, ushindani umekuwa mkubwa, wameachwa wako hoi. Naomba sana kwa kweli iangalie matatizo ya watu hawa watumishi wa Shirika la Posta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ujumbe wa mwenge. Ujumbe wa mwenge, kwanza napongeza sana. Mbio hizi za mwenge za kila mwaka zinaongeza chachu ya maendeleo kwa Taifa letu. Mimi naendelea sana kuunga mkono. Lakini zinajenga moyo wa utaifa na hii ni hazina kubwa sana tuliyoachiwa na Marehemu Baba wa Taifa, Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. *(Makofi)*

Sasa kila mwaka tuna ujumbe wa UKIMWI. Tathmini yetu inasema nini. Nikiangalia kwenye vitabu, naona tathmini inatuteremsha kwamba tumetoka sehemu fulani kwenda sehemu fulani na hasa zoezi la Mheshimiwa Rais la kupima kwa hiari. Lakini mimi nataka niseme hapa, UKIMWI upo na unaendelea kutafuna watu kwa kasi kubwa. Kwanza wale wanaopima wengi ni wale wanaojiamini kwamba wako angalau safi. Ndiyo maana mnaona kiwango hiki cha upimaji kinateremka, wale ambao si safi hawaendi kupima. UKIMWI kila siku unasema hapa, bila ya kujipima, kujifahamu huwezi ukafahamu kama umeathirika ama hujaathirika. UKUMWI hauna mnene, maana wengine mnatushangaa shangaa wakiona wembamba mnafikiri ndiyo tuna matatizo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu wengine wanene wana matatizo, UKIMWI haupimwi kwa macho. Kwa hiyo, nilikuwa nasema ndugu zangu, vijana wetu wengi wanaathirika, na mimi naanza kuona huu muingiliano wa dunia huu umekuwa kama kijiji una athari kubwa sana. Nilimsikia Mheshimiwa Hawa Ghasia siku za nyuma huko, haya mavazi yasiyokuwa na nidhamu yasiingie maeneo ya kazi. Huko maeneo ya kazi sasa, je mitaani? Hali ya uvaaji wetu sasa hivi kwa kweli nayo inachochea. Inachochea UKIMWI huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inatisha. Mimi naomba sana Wizara husika, Wizara hii ya Kazi na Wizara zingine zote, Wizara mtambuka, ziangalie kwa kweli mambo haya. Msifikiri utaifa ni jambo muhimu sana, mambo mengi sana tunaacha, tunaiga mambo mengine. Sasa leo watu wanatembea matumbo wazi hapa, kwenye kitovu wametoboa, tunasema ni utamaduni wa kisasa. Kishaufu kinavaliwa kwenye pua, leo kinavaliwa kwenye kitovu, mzazi upo, maadili tunaacha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wanavaa pensi, sisi tunajua mwili wa mwanamke, unasitirika kwenye magoti mwisho, msanii tu anavaa pensi inaishia,

inasikitisha sana. Lakini tunakwenda kwenye madansi na madisko, kwenye dansi na disko mtu amevaa chupi anacheza pale na watu wa heshima wapo. Hivi dansi na disko ya sasa unaweza kwenda na mtoto wako kweli? Hasa kwa mtu mwenye maadili yako. Hata *TV* sasa huwezi ukakaa na mwanao kama mtoto wangu, kama Msindai hapa angekuwa mwanangu siwezi nikakaa naye kuangalia kwa kweli. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utaamua aidha, kama mtoto anakuheshimu baba atoke mwenyewe au wewe utoke uwaache, ni aibu. Sasa tunaona haya ni mabadiliko, ni nini? Naomba sana Serikali iangalie mambo haya yanapotosha na yanaendeleza sana, maana tunasema macho ndiyo yanayoleta mwamsho. Mtu ambaye hajajaliwa macho mpaka asikie sauti, mpaka apapase, lakini mwenye macho akiona tu tayari, mwili unaanza kusisimka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana kwamba masuala haya ya mavazi kwa kweli yaangaliwe kwa ukamilifu kuwajenga vijana wetu katika utamaduni wetu wa awali. Leo nilikuwa nataka kuzungumza mambo machache sana lakini niishie na suala la ajira. Ajira ya vijana mimi nilikuwa naomba sana vijana wetu wengi wanajiingiza katika mambo mengine hayo ya ngono uzembe na dawa za kulevya. Lakini tusiendelee kutegemea sana kwamba vijana wetu wengi watakaomaliza elimu ya sekondari, Vyuo Vikuu watapata ajira za maofisini. Tuwaelekeze katika kuhakikisha kwamba tunawawezesha waende vijijini wakafanye shughuli za kilimo. Hiyo ndiyo ajira kubwa sana kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka mmoja tumeenda na Mheshimiwa Edward Lowassa akiwa Waziri wa Maji, Misri. Tukaambiwa kule kwamba huku tunawawezesha vijana. Wakishamaliza vyuo vikuu tunawapa mikopo wakatumie elimu yao ile vijijini waende wakafanye kazi za kujiajiri vijijini za kilimo. Leo hii vijana wetu wanamaliza, wanazunguka wanatafuta ajira na kwa sababu hawajawezeshwa na Serikali kupata mikopo hii, wataendelea kubaki, wana taaluma zao. Leo pale Chuo cha Kilimo cha Sokoine kuna mambo mazuri sana pale *Sokoine University*. Lakini wale vijana wengi wanaomaliza pale wengine wamekaa wanazunguka. Kuna vijana wetu wengi sana kwa kweli wanamaliza vyuo vikuu lakini naiomba sana Serikali iangalie uwezekano wa kuwawezesha katika suala zima la kuhakikisha kwamba vijana wanapata mikopo ya kutosha kuweza kufanya shughuli zao za ajira huko vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho watu wakishazalisha wanataka masoko. Vijana tunawahimiza, watu tunawahamiza wakajiajiri vijijini, lakini watataka masoko. Sasa masoko haya maeneo mengine inawezekana, kwa sababu barabara zipo. Sasa maeneo kama Tabora pale, unamwambia mtu aende pale akanunue karanga, anafika Sikonge pale gari limezama mwezi nzima, haji na hawa vijana watakuwa wanazalisha hawawezi kupeleka mazao yao katika maeneo mengine sokoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali kupitia Wizara hii na Serikali ndiyo hiyo hiyo moja, tuendeleze juhudi za kuhakikisha tunafungua mikoa yetu yote kwa njia ya barabara. Mtu aweze kutoka Mpanda anapita Sikonge aweze kwenda mpaka Tabora mpaka Kigoma. Aweze kutoka Tabora aje mpaka Singida.

Aweze kutoka maeneo mengine ambayo siwezi nikayataja yote hapa lakini kwa kweli kwa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno haya, sitaki kengele ya pili inigongee, lakini naomba sana Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, ni ndugu yangu, ni kaka yangu, basi haya machache niliyoyasema ni changamoto tu na mimi nitakuunga mkono hapa. Hata kwenye vifungu vya shilingi, naendelea kuwahamasisha wenzanbu hapa tukuunge mkono kwa matatizo makubwa uliyo nayo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, napenda kusema kwamba mjadala huu umeshafungwa kwa sababu wote walioomba na waliokuwemo humu wameshazungumza. Wasiokuwepo na la kwao halipo. Kwa sababu huwezi kuahirisha sasa, wasubiri hawa Jumatatu, inakuwa si sahihi kabisa.

Kwa hiyo, tukija siku ya Jumatatu, baada ya kipindi cha Maswali na Majibu, Mheshimiwa Waziri itabidi aanze kutoa ufafanuzi juu ya hoja zenu mlizofanya na tutakuwa na Kamati ya Matumizi asubuhi ile. Halafu jioni saa 11.00 Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika itabidi atoe hotuba yake.

Kwa hiyo, naagiza Kamati na Kambi ya Upinzani wanaohusika wajiandae, kwa sababu wao hotuba zao pamoja na Waziri wataziweka mezani asubuhi, maana yake Hati tunaweka asubuhi, hatuweki mchana, tunaweka asubuhi. Kwa hiyo, wote hawa hata kama watasoma jioni lakini Hati zitawasilishwa asubuhi mezani. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba Kambi ya Upinzani muwe tayari, Kamati inayohusika iwe tayari, Serikali yenyewe muwe tayari. Kwa hiyo, hiyo ni siku ya Jumatatu. Tutaendelea kwa sababu mnajua wachangiaji wa Wizara hiyo ni wengi, tutaendelea na ratiba kama kawaida, maana itakuwa nayo kusoma jioni, huenda atasoma Waziri, atasoma Mwenyekiti wa Kamati, atasoma Kambi ya Upinzani, itakuwa tumemaliza. Halafu tarehe 22 tunachangia na tarehe 23 tunachangia mpaka asubuhi. Kwa hiyo itakuwa tumejiongezea wenyewe saa chache kwa Wizara hiyo. Lakini ratiba zingine zitaendelea kama kawaida.

Waheshimiwa Wabunge, asubuhi niliwaambia kwamba ule msiba wetu ile asubuhi ulikuwa kwa kweli ndiyo umetokea tu. Hatukuwa na maelezo mengine zaidi ya yale nilivyotangaza. Lakini sasa marehemu wetu wameshakuja wako hapa *motuary* ya hapa Dodoma. Kwa hiyo, waliofariki ni mtoto wa Mheshimiwa Savelina Mwijage, Binti yake Stella Silvanus, alikuwa wa umri wa miaka 18, kwa hiyo, amefariki huyo. Halafu na dereva wake Anderson Kaindoa, mwenye umri wa miaka 40.

Pamoja nao walikuwepo watoto wengine, alikuwepo Gelva Silvanus mtoto wa Mheshimiwa Savelina Mwijage, kulikuwa na mtoto mwingine Sili Silvanus na mtoto mwingine Irene Silvanus. Halafu kulikuwa na mtoto wa Mheshimiwa Meryce Emmanuel, Imelda Mussa. Sasa hawa wamejeruhiwa lakini walipokwenda kuchukuliwa wamepelekwa pale hospitali wamechekiwa, wengine wamekwenda nyumbani lakini

mtoto mdogo wa Mheshimiwa Savelina Mwijage ndiyo ameumia naye yuko hospitali pale *Intesive Care Unit.*

Kwa hiyo, tunategemea kupata ndege kesho na kwamba wataondoka kesho saa 5.00 asubuhi na msiba sasa hivi uko pale anapoishi yeye mwenyewe Mheshimiwa Mbunge, wanaopata nafasi basi wapite wakampe *campany.*

Matangazo mengine, orodha ya watakaokwenda itatangazwa kule kule, kwa sababu hatujakaa na kusema nani watakwenda kusindikiza, itatangazwa kule kule.

Lakini pia ningependa kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge tarehe 22 Julai, 2008 asubuhi Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa atakuwa Dodoma. Kwa hiyo, atakuwa pia ni mgeni wetu. Ratiba yake ni ya siku moja ama tuseme siku mbili maana atafika tarehe 22 na kuondoka 23 Julai, 2008. Kwa hiyo, Wabunge wote tutakuwa na mazungumzo naye siku hiyo ya tarehe 22 Julai na wakati tutaambiwa. Itakuwa vizuri zaidi tukikusanyika wote, maswali mnayomuulizaga Waziri Mkuu kuhusu mambo mengine mnaweza pia mkamuuliza. Kwa hiyo, itakuwa vizuri, tutawaambia wakati siku ya Jumatatu ni saa ngapi. *(Makofi)*

Naomba Wabunge wote waweze kuhudhuria kipindi hicho. Tutawaambia Jumatatu. Halafu kuanzia tarehe 22 Julai, 2008 jioni wataingia Wabunge wa Bunge la Uingereza. Hawa ni wale wanachama wa *CPA* toka tarehe 22 mpaka 24 Julai, 2008 watakuwa wageni wetu hapa. Malengo yao watazungumza na makundi mbalimbali ya Wabunge, wanakuja kwa mambo yafuatayo, kujifunza masuala ya kisiasa kwa kuzingatia masuala yafuatayo, maana yake watu wanashangaa nchi hii, ina dini zote, ina watu wa aina zote lakini bado wanaishi pamoja. Sasa hili nalo wanaliona sio la kawaida. Wanakuja kujifunza. *(Makofi)*

Halafu wanajifunza pia Tanzania tumeingia kwenye siasa ya vyama vingi na bado tunaishi na tunaenda pamoja. Halafu kuna Zanzibar na Bara pamoja nayo pia wanataka kujifunza. Unajua ni nchi ndogo lakini watu wengi wanapenda kujifunza kwa sababu mahusiano haya ya watu na watu wa aina mbalimbali, nchi nyingine haikaliki. Kwa hiyo, pia hayo wanakuja kujifunza. *(Makofi)*

Kwa hiyo, na wageni wakija namna hiyo, uzalendo lazima utawale. Sio mtu mahusiano yake, matatizo yake binafsi anaanza kuona kama ndiyo msimamo wa nchi. Kwa hiyo, naomba mtakapokuwa mnazungumza na watu mbalimbali mjue pia na uzalendo wetu utawale. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wanakuja pia kujifunza juu ya changamoto kubwa zinazoikabili Tanzania hususan kwenye masuala ya misaada hii kama tunapata faida au vipi. Wanakuja kujifunza elimu, mnakumbuka wakati fulani tumewaambieni mwaka jana Mheshimiwa Rais wetu alipata medali ya Kimataifa kuhusu namna alivyoweza kuanzisha elimu kwa watu wote wa Tanzania mpaka kiwango cha sekondari. Tanzania ni ya kwanza katika nchi hii. Sawa ubora ni kitu kingine lakini unaanza wapi, unaanza kuku au yai? Ndiyo tatizo hilo, ubora ni kitu kingine. Lakini dunia nyingine watu

hawajui neno linaitwa shule wala shule hazipo, huo ni ukweli kabisa. Kwa hiyo, amepata medali kabisa ya Kimataifa kwa sababu hiyo. Kwa hiyo, wanakuja kujifunza hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu wanakuja kuzungumza na sisi kuhusu mambo ya *HIV/AIDS* na mambo mengine kwa ujumla yanayohusu mambo haya ya *HIV/AIDS* na hiyo pia ni kweli kwa sababu Bara letu la Afrika ndiyo linaloongoza kwa wagonjwa wengi wa *HIV/AIDS.* Tanzania haiwezi kuwa ni tofauti. Lakini ni tofauti kidogo safari hii tumepunguza maambukizi. Kama tutaendelea namna hiyo pengine na sisi tunawapiku hata wenzetu wa Uganda. Lakini Mkoani kwangu ndiyo sisemi, ovyo kabisa, hali ni mbaya. Maambukizi yanafika mpaka asilimia 15 wakati mahali pengine ni wastani wa asilimia tano. Halafu wakitoka hapa wale Waingereza wanakwenda Zanzibar, kule watakwenda kati ya tarehe 24 na 25 Julai. Kwa hiyo, tuna ugeni lakini tutaweza kuwamudu na tumekuwa na wageni kipindi hiki chote. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, matangazo mengine mimi sina. Semina najua ipo ya wafugaji kesho, tunaambiwa kwamba wenyewe wamepeana barua. Kwa hiyo, wanafahamiana na mengine sina. Jumapili mimi sifahamu semina kama ipo. Basi mtatangaziwa huko huko, maana yake semina itasikika tu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hivyo kama nilivyosema mkumbuke kwamba, aah hii semina ni ya tarehe 20 Julai. Hii ya wafugaji pia ni tarehe 20 Julai, lakini nadhani kuna watu maalum. Siyo kila mtu. *(Makofi)*

Baada ya kusema hivyo Waheshimiwa Wabunge, napenda kuahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya Jumatatu saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 01.10 usiku Bunge liliahirishwa hadi siku Jamatatu,*
*Tarehe 21 Julai, 2008 saa tatu asubuhi)*